

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 16 Aprili, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na kikao chetu, leo ni Kikao cha Kumi na Moja katika Mkutano wetu huu wa Tatu. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLYANGO - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri, TAMISEMI.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLYANGO - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa huko huko swali la Mheshimiwa Charles Mguta Kajege, Mbunge wa Mwibara uliza swali lako. Mheshimiwa Kajege.

Na. 84

**Ukarabati Barabara za Jimbo la Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEJE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazikarabati barabara za Jimbo la Mwibara ambazo zimeharibika sana ili kuruhusu mawasiliano kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo tafadhali, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mugeta Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina majimbo mawili ya Uchaguzi ambayo ni Bunda Vijijiini na Mwibara yenye mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 527.55. Serikali imekuwa ikitenga fedha za matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 shilingi milioni 546.87 zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara na shilingi bilioni 708.56 zimeidhinishwa katika mwaka wa

fedha 2020/21 kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha miundombinu ya barabara katika jimbo la Mwibara katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imefanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 28.2 na makalvati 11 kwa gharama ya shilingi milioni 237. 43. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21 shilingi milioni 460.44 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu kilomita 54.5 na makalvati 29 ambapo utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi na matengenezo ya barabara za Wilaya ya Bunda na nchini kote kadiri wa upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:- Kwa kuwa barabara za Bugoma kwenda Mchigondo barabara ya Igundu kwenda Bulomba na barabara ya kutoka Mranda kwenda Mwiliruma hazipitiki kabisa kwa muda mrefu.

Je Serikali iko tayari kutengeneza barabara hizo kwa kutumia hata mfuko wa maafa?

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuona ni kuamini yaani *seeing is believing* je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya kikao hiki tuongozane nae ili akajionee mwenyewe hali ilivyo katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hizi ambazo

Mheshimiwa Kajege amezitaja katika Jimbo la Bunda zimeharibika kufuatia mvua nyingi sana ambazo zimeendelea kunyesha kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mpango muhususi wa kwenda kuhakikisha barabara hizi ambazo zimeharibiwa na mvua na hazipitiki zinatengenezwa mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kusafirisha lakini na kusafiri katika huduma mbalimbali za kiuchumi, na kijamii. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha katika mpango uliopo tunatoa kipaumbele cha hali ya juu katika barabara hizi zilizopo katika Jimbo la Mwibara

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI tuko tayari wakati wowote kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge na kufuatana nao katika majimbo hayo ili tuendeleo kuwahudumia wananchi. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Kajege kwamba niko tayari baada ya kikao hiki tutapanga tuone ratiba nzuri ya kwenda katika Jimbo lake ili kuendelea kuwahudumia wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace V. Tendega nilikuona Mwenyekiti wa LAAC uliza swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika Ahsante sana kwa kuniona changamoto ya barabara katika Jimbo la Mwibara ni sawasawa kabisa na changamoto za barabara katika Jimbo la Kalenga Mkoani Iringa. Kumekuwa na changamoto kubwa sana na barabara ya kutoka Iringa Mjini kuelekea Kata za Muhota na Magulilwa kutoka Kijiji cha Kitayawa kwenda Nyabula ambako kuna Hospitali ya Misheni ambako wananchi wanatibiwa barabara imekatika kabisa haipitiki imekatika daraja limekatika

Je! Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa jimbo hili la Kalenga hususani wale wale wa...

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa kidogo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** ...Kata ya Mpota wanaweza wakapata mahitaji ya barabara.

**SPIKA:** Taarifa ya nini yuko wapi anayesema taarifa?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Samahani unjuka ndio unaotusumbua Kiswaga hapa. (Kicheko/Makofi)

**SPIKA:** Ndio Mheshimiwa Kiswaga!

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Ni unjuka tu unatusumbua lakini kama unaniruhusu nitasema neno moja. (Kicheko)

**SPIKA:** Karibu nakuruhusu.

## T A A R I F A

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA,** Mheshimiwa Spika, ahsante sana hiyo barabara ya kutoka Kitayao kwenda Nyabula tayari nimeshafanya mpango nimeongea na TARURA na sasa tumeshaweka mabomba hilo daraja linaanza kujengwa hivi karibuni ahsante sana tulipata fedha ya dharula nakushukuru. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega unapokea hiyo taarifa? Halafu tuendelee na swali lako lipi sasa baada ya taarifa hiyo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, kwa uchungu kabisa ninazungumza hapa sipokei taarifa hiyo wananchi wale wanapata shida sana hakuna chochote anachokisema kimefanyika pale barabara imekatika na wananchi awapati huduma kwa hiyo naomba swali langu lijibiwe. (Makofi)

Ni lini Serikali itahakikisha wananchi hawa wanapata huduma ya barabara waweze kupata huduma zingine na matibabu na kiuchumi?

**SPIKA:** Ahsante majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Dugange Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Kiswaga Mbunge wa Jimbo la Kalenga kwa juhudi kubwa sana anazozifanya kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Kalenga wanapata barabara bora na hivyo wanaendelea na shughuli za kiuchumi na kijaamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisema barabara hii ya kutoka Iringa Mjini kwenda Kata ya Maguliwa na maeneo haya kuna hospitali Serikali imeendelea kuhakikisha inatoa kipaumbele kwenye barabara ambazo zinapeleka huduma za jamii kwa wananchi, zikiwemo hospitali, shule na maeneo mengine yenye huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotanguliwa kusema tumepata baraka ya mvua mwaka huu, lakini tunafahamu baraka hiyo imeambatana na uharibifu wa baadhi ya madaraja, ma-calvati na barabara zetu. Naomba nimuhakikishie kwamba Serikali inaendelea kuweka mipango ya haraka ikwezekanavyo kuhakikisha barabara ile aliyoisema inakwenda kutengenezwa na hilo daraja lifanyiwa matengenezo ili wananchi waweze kupita na kupata huduma hizo za afya na huduma nyingine. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hilo linafanyiwa kazi na Serikali.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata baada ya hili la Mheshimiwa Kajenge ni swali linakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na litaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki.

Na. 85

**Hitaji la Taa za Barabara**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka taa katika barabara kuu ya Mji wa Maswa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi Eng. Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:- Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*) ilishaanza kazi ya uwekaji taa katika barabara kuu ya Mwigumbi hadi Maswa eneo la Maswa Mjini katika mwaka wa fedha 2020/2021. Jumla ya taa za barabarani 18 zimeshawekwa ambazo zimegharimu jumla ya Shilingi milioni 81.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini *TANROADS*, imepanga kuendelea na uwekaji wa taa katika barabara kuu katika Mji wa Maswa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Haroon swali la nyongeza

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa majibu ya Serikali, na niwapongeza Serikali kwa kuanza kufanya mradi huu kwa kuweka taa za barabara kuu za Mji wa Maswa. Ninachosikitika ni kwamba mradi huu umekwenda nusunusu sasa naomba Mheshimiwa anipe majibu ya kweli wameweka taa 18

Je, wana mpango wa kuweka taa ngapi ambazo zitatoa kuanzia Mwigumbi kwenda njia panda.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa Maswa wanapata shida barabara hiyo zinapopita gari kwa kasi

kubwa watu wanapata ajali na wengine wanapoteza maisha na kuna mpango wa kutengeneza *bypass road* kuzunguka Mji wa Maswa.

Je, barabara hiyo nayo itajengwa lini? Ahsante sana.  
(Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika barabara zote za sasa ambazo zinatengenezwa imekuwa ni sehemu ya mkataba kwamba pale ambapo barabara zinapita kwenye Miji, moja ya eneo ambalo lazima lishughulikiwe na Wakandarasi ni kuweka taa za barabarani ikiwemo Mji wa Maswa. Taa sizopungua 60 zitaweka katika Mji wa Maswa ili kukamilisha Mji wote kwenye barabara ile kuu, swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, *bypass road* ya Maswa itajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha ipo kwenye mpango na itajengwa mara tu Serikali itakapokuwa imepata fedha ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe nilikuona uliza swali.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Maswa ina umuhimu sana sawasawa na barabara ya watu wa Kibiti kutoka Kibiti Dimani kwenda Mloka kule ambako kuna ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, na kwa kuwa Mheshimiwa Rais mama yetu Samia wakati anainadi ilani ya Chama Cha Mapinduzi aliahidi kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami.



Je, ni lini Serikali itatenga fedha ili shughuli za awali za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zianze mara moja katika barabara hiyo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi mheshimiwa *Engineer* Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Kibiti ni moja ya barabara muhimu sana ambayo ni moja ya njia inayofika kwenye Bwawa la Nyerere, na barabara hii ni ahadi ya viongozi wetu wa Kitaifa.

Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti, kwamba barabara hii ipo kwenye mpango na itajengwa kwa kiwango cha lami kama viongozi ambavyo wametoa ahadi na kama ambavyo inaonekana kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi ahsante.

**SPIKA:** Bado tupo kwenye Wizara hii swali linalofuata litaulizwa na Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Iddi Iddi.

Na. 86

### Ujenzi Barabara ya Geita

**MHE. IDD K. IDDI** aliuliza:-

Je, nili ni Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Geita – Bukoli hadi Kahama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Bado tuko kwako *Engineer* Msongwe majibu ya swali hilo la watu wa Msalala tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasimu Iddi Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Geita – Bukoli hadi Kahama yenye urefu wa kilomita 139 inayounganisha mikoa ya Geita na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ilifanywa na Mhandisi Mshauri *ENV Consult (T) Ltd* kwa gharama ya Shilingi milioni 440. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Aidha, Kampuni ya Uchimbaji Madini *BARRICK* imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Kahama – Bulyanhkulu – Geita yenye urefu wa kilometa 120.2. Kwa sasa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Madini zinaendelea na mazungumzo na Kampuni ya *BARRICK* kuhusu utaratibu wa ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi wa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha Wizara yangu inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha huu wa 2020/2021, jumla ya shilingi milioni 872.966 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

Aidha, ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufuku kuwa ili ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ufanyike, hatua mbalimbali hufuatwa ambazo ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina. Utayarishaji wa Nyaraka za zabuni na taratibu za ununuzi za kumpata mkandarasi wa ujenzi. Hivyo, kukamilika kwa hatua tajwa, maana yake nikuanza kwa mradi husika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Kasimu Iddi Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Msalala, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi, hususan wa Kata za Segese, Shilela, Ngaya na Bugarama. Barabara hii imeahidiwa kiasi cha dola milioni 40 kwa ajili ya kutengenezwa na Mgodu wa Barrick na imekuwa ni kero kubwa sana kwani inasababisha wakazi wa maeneo haya ambayo nimeyataja kuhama makazi yao asubuhi na kurudi jioni kutokana na vumbi kali kwa sababu inatumiwa na magari makubwa. Je, ni lini sasa Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Madini watakwenda kwa Waziri wa Fedha ili wamwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kutekeleza mkataba na makubaliano walioingia baina ya Serikali na Mgodu ili Mgodu uanze kutengeneza barabara hii mara moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini sasa Serikali itaanza kufikiria ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara inayotoka Kahama kupita Kata ya Busangi kwenda Nyang’hwale na kutokea Busisi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huko Msalala mnataka barabara zote ziwe za lami, wenzenu je? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Msalala kwamba katika jibu langu la msingi nimesema Mgodu wa Barrick wameonesha nia maana yake ni kwamba tayari timu ya majadiliano imeundwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Madini, lakini kwa sababu tunayojadili ni masuala ya fedha timu hiyo imejuimuisha pia Wizara yenyewe ya Fedha. Kwa hiyo, *once* majadiliano yatakapokuwa yamekamilika na kupata utaratibu sahihi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo itaanza kujengwa ili

kuwapunguzia adha wananchi wake wa Lunguya, Segese, Ntobo hadi Bukoli na Geita ambao wako Mkoa wa Geita. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba Serikali itafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Nyang'hwale kwenda Busisi, naomba pia nimhakikishie kwamba ipo kwenye mipango, ipo kwenye Ilani na tuna mpango wa miaka mitano ambao nina hakika katika kipindi hiki barabara hiyo pia itajengwa kadiri fedha zitakavyopatikana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unaona barabara hizo? Mheshimiwa Babu Tale nimekuona, twende Morogoro.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli, alipopita kwenye Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki alituahidi barabara ya Bigwa – Kisaki. Naomba kuiuliza Serikali barabara hii itaanza lini kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Barabara hii pia ni muhimu sana kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya Msongwe. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Babu Tale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipotembelea Mkoa wa Morogoro, moja ya ahadi alizotoa na ilikuwa ni maagizo kwamba barabara hii ijengwe haraka kwa kiwango cha lami. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Babu Tale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki na wananchi anaowaongoza wa Jimbo lake kwamba barabara hii kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia kilometa 50. Kama navyoongea naye mara kwa mara, nimhakikishie kwamba

barabara hii itakuwa ni kati ya barabara ambazo zitatangazwa muda si mrefu kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hiihii ya barabara, tuchukue swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini. Mheshimiwa Mwakamo tafadhali.

Na. 87

### **Ujenzi Barabara ya Makofia – Mlandizi – Kisarawe**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Makofia kupitia Mlandizi hadi Vikumbulu Kisarawe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumbulu yenye urefu wa kilometa 135.97 ni barabara ya mkoa inayounganisha Wilaya za Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uhakiki wa mali zitakazoathiriwa na mradi sehemu ya Makofia – Mlandizi – Maneromango yenye urefu wa kilometa 100 umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza baada ya kupata fedha ambazo Serikali inaendelea kutafuta.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara yangu inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika Mwaka huu wa Fedha wa 2020/21 jumla ya shilingi 1,524.000.07 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri juu ya ujenzi wa barabara hiyo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu wa kilometa hizo 100 ambazo zinatokea Makofia kuendelea Kisarawe, je, ni lini Serikali italipa fidia wananchi hawa ili kupisha ujenzi huo uendelee kwa sababu ni wa muda mrefu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hii; na kwenye majibu yake anakiri kwamba ametenga pesa ya kufanyia ukarabati wa muda wakati wakisubiri tukipata pesa, naomba niifahamishe Serikali kwamba kwa sasa barabara hii haijafanyiwa ukarabati huo kwa miaka mingi. Kwa kuwa pesa hizi zimepangwa mwaka huu wa bajeti, je, Serikali haioni sasa ni muda sahihi kutafuta fedha za haraka kuzifanyia ukarabati barabara hizo kwa sasa kwani kipande cha kutoka Mlandizi kwenda Mzenga kina mashimo makubwa utadhani mabwawa ya kuvulia samaki? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kila hatua inayofanyika ndiyo ujenzi wenyewe wa barabara ya lami unavyoendelea. Barabara hii haitaanza kujengwa mpaka kwanza fidia ya wananchi hawa ambao bahati nzuri tayari wameshatathminiwa watakapolipwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mwakamo kwamba wananchi hawa watalipwa fidia pale tu ambapo Serikali itapata fedha. Jitihada kubwa zinafanywa na Serikali kuhakikisha kwamba tunapata fedha ili tuweze kuwalipa hao wananchi ambao tayari wameshaainishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kwamba barabara hii haijafanyiwa matengenezo; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia Bunge hili naomba kumuagiza Meneja wa Barabara Mkoa wa Pwani aweze kutembelea barabara hiyo na kuangalia upungufu uliopo aweze kuikarabati kwa sababu fedha imetengwa ili wananchi waendeleo kupata huduma ya barabara hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tu tuendeleo na Wizara ya Kilimo kwa sababu ya muda.

Ninazo taarifa kwa vile swali hili linahusu barabara kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanakuja Bungeni kwa usafiri ule mzuri kabisa wa wananchi, usafiri wa bodaboda na kurudi kwa usafiri huo. Ni usafiri mzuri, sina shida nao, lakini basi nawaomba umakini na kuwa na uhakika na huyo dereva wa bodaboda, maana kupatikana kwenu jamani ni kwa gharama kubwa. Nadhani mmenisoma? Pia ni vizuri kuelewa wananchi wako wakikuona huko watatafsiri vipi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest.

Na. 88

## **Kubadili Mfumo wa Ununuzi wa Kahawa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Pamoja na Kyerwa kuwa na wakulima wengi wa kahawa bado soko linakuwa gumu.

Je, ni lini Serikali itafikiria kubadilisha mfumo wa ununuzi wa kahawa kwa wakulima?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo namba 88, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutoka tani 47,000 kwa mwaka 2016/2017 mpaka tani 59,000 kwa mwaka 2019/2020. Aidha, katika msimu wa 2020/2021 lengo la uzalishaji ni tani 70,000 za kahawa safi, ambapo hadi kufikia Machi, 2021 uzalishaji umefikia tani 67,676 sawa na asilimia 96.7 ya lengo. Kati ya hizo, Mkoa wa Kagera pekee unazalisha tani 39,667 ambayo ni sawa na asilimia 58.8 ya uzalishaji wa nchi nzima na Wilaya ya Kyerwa inazalisha tani 19,000 kati ya 39,000 zinazozalishwa na Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2020/2021 mifumo ya masoko inayotumika ni soko la awali, mnada na soko la moja kwa moja. Katika mifumo yote, wakulima hucusanya kahawa yao kupitia vyama vya ushirika. Mifumo hiyo inalenga kuondoa biashara ya kahawa isiyo rasmi inayotumiwa na walanguzi maarufu kwa majina ya butura (Kagera), Njemke au kata kichwa kwenye mikoa mingine ikiwemo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.



Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2020/2021 tani 67,676 zilizozalishwa tayari zimeuzwa kufikia Machi, 2021, tani 20,296 zenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 53.5 sawa na asilimia 30 za mauzo yote zimeuzwa kwa njia ya mnada. Kadhalika, kufikia Machi mwaka huu jumla ya tani 47,108 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 79.2 sawa na asilimia 69.9 ya kahawa yote iliyouzwa zimeuzwa kwa njia ya minada.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inaamini mifumo ya masoko inayotumika ni mizuri na itaendelea kuboreshwa kulingana na mahitaji yanavyojitokeza ili kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika na yanayotoa bei nzuri. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa kwa sasa ni kuimarisha bei za kahawa kwa kuongeza ubora kuanzia shambani hadi sokoni, kuongeza tija ili wakulima waongeze kipato na kuimarisha vyama vya ushirika. Hatua nyingine ni kuendeleza viwanda vya ndani vya kuongeza thamani na kutafuta masoko mapya ikiwemo kuingia mikataba na nchi au wanunuzi wenye uhitaji mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika majibu aliyotoa Naibu Waziri, anaeleza mifumo yote ya ununuzi inahusisha kukusanya kahawa katika maghala kwa sababu moja tu ya kuzuia butura. Serikali kushindwa kuzuia butura na kuleta sababu ya kukusanya kupitia maghala ni kutesa wakulima.

**SPIKA:** Butura ndiyo nini?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, butura ni mfumo ambao wafanyabiashara wanakwenda kwa wakulima kabla ya msimu wanawapa fedha halafu baadaye msimu ukifika wanawapa kahawa.

**SPIKA:** Ni kama kwenye korosho kangomba.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, sawa. Wamekuwa wakifanya hivyo siyo kwa sababu

wanapenda, kwa sababu hela ya kahawa inaletwa ikiwa imechelewa. Sasa nataka niulize swali; ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kuruhusu wafanyabiashara wakanunua moja kwa moja na Serikali ikasimamia kuzuia butura? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama Serikali ikiruhusu *KDCU* au vyama vya ushirika kukusanya kahawa ije sasa na mkakati wa kuwawezesha kupata fedha ili walipe wakulima mwanzoni mwa msimu kwa sababu inahitajika fedha kwa ajili ya kuandaa mashamba; katikati ya msimu inahitajika fedha kuvuna kahawa na baadaye mwishoni wakiwa wamemaliza kuuza. Nataka nijue Serikali imejipangaje kuhakikisha wakulima wanapata fedha katika awamu tatu na siyo kusubiria baadaye kama wanavyofanya sasa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatopia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba iingie tu *on record* vilevile *concern* ya Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera katika ku-*perfect* mfumo wa ulipaji ni *concern genuine* ambayo tunaifanyia kazi kama Serikali. Hata hivyo, niseme kitu kimoja; mfumo wa ushirika ni *basic principle* ambayo kwanza imeelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, pili, ndiyo mfumo sahihi wa *aggregation* kwa wakulima wadogowadogo unaoweza kuwalinda. Kwa hiyo, kuondoa mfumo wa ushirika tutakuwa tunatenda dhambi kubwa kabisa ya kuwalinda wakulima wadogowadogo. Tunachotakiwa kufanya ni ku-*perfect* na tumefanya hivyo katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera, Chama cha *KDCU* na Chama cha *KCU* katika kipindi cha miaka miwili hii ndiyo vyama pekee ambavyo tumevipatia fedha kupitia Benki ya Maendeleo ya Wakulima kwa riba isiyozidi asilimia tisa. Tunaelewa kuna tatizo la ucheleweshaji wa malipo lakini

hatuwezi kufananisha tatizo lililokuwepo miaka miwli iliyopita na msimu huu. Tuwe wakweli na tuseme ukweli mbele ya Mwenyezi Mungu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanunuzi kwenda kwa wakulima moja kwa moja; hatumkatalii mfanyabiashara yeyote anayetaka kununua kahawa ya wakulima lakini hatutamruhusu kwenda kumpa mkulima wakati ana shida ya hela kwa shilingi 200 halafu aende akaivune kahawa ikiwa haijakomaa. Wanataka kununua kahawa, waje na leo mimi nina kikao na wewe Mheshimiwa Mbunge nakukaribisha, tutakuwa na kikao cha kahawa tunajadili mfumo na tutawapa leseni mapema. Waseme wazi wanataka kununua kahawa ya wakulima kwa bei gani na *volume* gani, tutawapeleka kwenye vyama vya msingi lakini *direct* kwenda shambani hatutaruhusu hilo.

**SPIKA:** Baada ya swali hilo la Mheshimiwa Anatropia Theonest, sasa Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, uliza swali lako. (*Kicheko*)

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayosababisha wakulima wasipate bei nzuri ya kahawa ni kupeleka kahawa ghafi nje. Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vikubwa ambavyo vitachakata hii kahawa ili kuongeza thamani mkulima aweze kupata bei nzuri ya kahawa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia unaona Mbunge wa Jimbo anavyouliza maswali ya maana? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza tunayoichukua *specifically* kwa Mkoa wa Kagera, sasa hivi kiwanda ambacho kinamilikiwa na wakulima wa Mkoa wa Kagera cha *TANICA*, *installed capacity* yao ni tani 3,000. Sasa hivi tunavyoendelea walikuwa wanadaiwa madeni mengi, tumeshachukua hatua ya kwanza kuhakikisha kwamba *TADB* inafanya *intervention* kuweza kuyaondoa yale madeni na kuyachukua wao kwa sababu madeni yale walikuwa wanaidawa na benki za kibiashara ambazo zilikuwa zinachaji riba kubwa.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, tunakifanyia sasa hivi kiwanda cha *TANICA feasibility study* ili tuweze ku-*expand* uwezo wake wa kuchakata kahawa ya wakulima wa Kagera ili kupitia kiwanda chao cha *TANICA* waweze ku-*process* na kuuza kahawa iliyochakatwa kama *finished product*. Vilevile tunafanya maongozi na wafanyabiashara kikiwepo kiwanda kikubwa kilichopo Kagera ambacho kina matatizo na *Tanzania Investment Bank* ili tuweze kukisaidia kuki-*bail out* kiwanda kile kiweze na chenyewe kuchakata kahawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwelekeo wa Serikali cha kwanza ni ku-*perfect* mfumo wa soko kuhakikisha wakulima wanalipwa kwanza malipo yao vizuri. Hatua ya pili ni *expansion* ya *TANICA* ili Mkoa wa Kagera waweze kuuza kahawa yao ikiwa *processed*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo tu na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati tafadhali.

Na. 89

**Mradi wa Kuendeleza Maliasili na Kukuza  
Utalii – REGROW**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini utekelezaji wa mradi wa kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (*REGROW*) utaanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (*REGROW*) tayari umeanza kutekelezwa tangu mwaka 2017. Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia katika maeneo ya kipaumbele zikiwemo Hifadhi nne za Taifa ambazo ni Hifadhi ya Taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere, Milima Udzungwa na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo pamoja na eneo la chanzo cha maji cha Mto *Great Ruaha*. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2017 - 2023.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2021, mradi huu umeendelea kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa ambapo kazi zifuatazo zimetekelwa: ununuzi wa vifaa vya doria vimeshanunuliwa, magari 44 yameshanunuliwa, mitambo mikubwa mitatu kati ya 18 inayotarajiwa kununuliwa, pia mradi umeajiri kampuni sita ambazo zinaendelea na usanifu wa majengo, barabara na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali kama vile majadiliano ya utekelezaji wa mradi huu katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, mradi ulichelewa kuanza utekelezaji wake kwa takribani miezi 17.

Aidha, uwepo wa ugonjwa wa *Covid - 19* umechangia kwa kiasi kikubwa kuendelea kuchelewesha utekelezaji wa mradi huu. Kutokana na kazi nyingi kusimama, mradi huu sasa umeshaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zote ambazo zilijitokeza, mradi umefanyiwa mapitio ya kati ambapo miongoni mwa mambo mengine ni kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi huu hadi mwaka 2025 ili kufidia muda uliopotea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama una swali.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali. Naomba niulize maswali madogo mawili. Kutokana na Mradi huu wa *REGROW* tulitegemea sasa wananchi wa Mikoa ya Kusini kuanza kutengeneza ajira nyingi sana kupitia utalii na kuongeza pato la mikoa hii; na tulitegemea sasa ujenzi wa Vyuo vya Utalii Nyanda za Juu Kusini katika eneo la Kihesa Kilolo na Makao Makuu.

Je, ni elimu kiasi gani imetolewa kwa wananchi wa mikoa hii ili kuwajengea uwezo katika kuupokea mradi huu?  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Biashara ni matangazo. Kwa kuwa mikoa yetu hii ya kusini tunavyo vivutio vingi na vizuri vikiwemo Mbunga za Wanyama *Ruaha National Park* ambapo ni Mbuga ya pili kwa ukubwa katika Afrika; tunavyo vivutio vingine kwa mfano pale Kihesa kuna Gangilonga, jiwe lililokuwa linaongea, lakini tuna Kitanzini ambayo ni sehemu ambayo watu walikuwa wanajinyongea; na vile vile tunalo fuvu la Mtwi Mkwawa ambalo lipo pale Kalenga...

**SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa kuvitangaza hivi vivutio vya kusini ili kupata angalau tupate watalii wa ndani na kuongeza mapato?  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, mwanawane.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ritta kwa swali lake zuri, maana hii ni kwa manufaa ya Mikoa yote ya Kusini mwa Tanzania. Mradi huu ni faida kubwa sana kwa wananchi na mikoa ya kusini mwa Tanzania kwani Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha ambao ni mkopo.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi la Mheshimiwa Ritta ameuliza kwamba tuna mkakati gani kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha pindi wanapopokea huu mradi? Pia na namna ambavyo wataenda kutelekeleza.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina mpango mkubwa wa kuanzisha vyo ambavyoo vitakuwa ni *campus*. Tunaanzisha *campus* ya Mweka na pia kutakuwa na Chuo cha Mambo ya Utalii ambacho kitaanzishwa kama *Campus* ya Iringa. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kwamba wananchi wa kusini mwa Tanzania wataweza kuelimika. Pia tutahamasisha utalii kupitia elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake lingine alisema biashara ni matangazo. Ni kweli bila kutangaza vivutio vyetu tulivyonavyo hapa nchini, utalii hauwezi kuendelea. Kipindi cha mpango huu wa bajeti, tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 46.5 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba utangazaji wa vivutio tulivyonavyo hapa nchini unafanyika kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye utangazaji bila kuimarisha miundombinu inakuwa ni changamoto; na hilo nimtoe wasiwasi kwamba tumetenga shilingi bilioni 75.4 ambazo zitaimarisha miundombinu iliyoko kwenye hifadhi hizo ili tuimarisha na kutangaza kwa bidii. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda tuendeleo, bado tupo Wizara hii hii ya Maliasili. Swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali. Mheshimiwa Mtega tafadhali.

Na. 90

**Kutatua migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji  
Dhidi ya Hifadhi ya Ruaha**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani wa kumaliza mgogoro kati ya Hifadhi ya Ruaha na Wakulima na Wafugaji wanaozunguka Hifadhi hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Mtega, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda Kamati iliyojumuisha Mawaziri kutoka Wizara nane kwa ajili ya kufuatilia na kutatua migogoro ya ardhi nchini. Migogoro hiyo iliyofanyiwa kazi na Kamati husika ni pamoja na migogoro kati ya wakulima na wafugaji wanaozunguka Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo imefanya tathmini ya migogoro hiyo na kutoa mapendekezo ambayo yameshatolewa maamuzi na Baraza la Mawaziri kwa ajili ya utekelezaji utakaoanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine na wananchi ambao maeneo yao yana changamoto za migogoro hiyo kutoa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa sababu ya muda tunaendelea na... Ooh, bado Mheshimiwa Mtega, swali la nyongeza tafadhali. (*Kicheko*)

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja, hivi tunavyoongea, juzi makundi makubwa ya tembo wamevamia vijiji vyote vitano vya Kata ya Igava na wameshambulia mazao yote; mahindi, mpunga na maboga. Sasa wananchi wale wapo hatarini kupata janga la njaa. Ni lini Serikali itawalipa fidia wale wananchi kuwanusuru wasipatwe na janga la njaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa ng'ombe wakiingia hifadhini kwa bahati mbaya, ng'ombe mmoja huwa anatozwa shilingi 100,000/=, sasa makundi ya tembo wale wametetekeza mazao yote na nimeenda juzi nimekuta ni mashimo matupu mashambani: ni kigezo gani au ni thamani gani watalipwa wale wahanga ambao ni wafugaji na wakulima wa sehemu ile? (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja. Ng'ombe akiingia ni laki, tembo akienda kwa mwananchi bei gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusu fidia, tumekuwa tukifanya uthamini pale ambapo kunatokea changamoto hiyo ya tembo kuingia kwenye maeneo ya kilimo na tunapofanya uthamini tuna-*compensate* wananchi kulingana na uthamini ulivyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna uthamini wa aina mbalimbali; kuna mwananchi kuwa amepoteza Maisha, na upande mwingine kupoteza mazao na pia wananchi kujeruhiwa. Kwa hiyo, tunalipa fidia kulingana na athari ilivyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu changamoto ya namna ambavyo tunatoza ng'ombe shilingi 100,000/=; kwanza naomba sana wananchi watambue kwamba sisi tupo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hifadhi hizi zinalindwa na zinatunzwa kwa ajili ya manufaa ya nchi kwa ujumla na wananchi waliopo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi kumekuwa na sintofahamu hasa kwa wafugaji kwamba wanaingiza ng'ombe zao kwenye hifadhi kwa makubaliano ya watumishi walioko kwenye maeneo husika na matokeo yake wanyama ambao wanahifadhiwa kwenye maeneo yale wanakutana na changamoto za magonjwa. Sasa Serikali inajikuta inagharamia gharama kubwa kufanya utafiti wa gonjwa lililoingia kwenye hao wanyama na kuwatibu. Kwa hiyo, tunajitahidi sana kuzuia wafugaji wasiingize mifugo yao kwenye maeneo ya hifadhi. Tutambue kwamba sheria ni sisi wenyewe tulizitunga, kwa hiyo, sisi ni watekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki kipo kwenye sheria, siyo kwamba sisi tumekiamua; kipo kwenye sheria ya Wanyama kwamba wananchi wanapoingiza mifugo yao kwenye maeneo ya hifadhi, basi tunatumia hiyo sheria kuhakikisha kwamba inatumika sawa sawa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa kwa sababu ya muda mkiangalia pale bado dakika kumi tu na tuna maswali matatu. Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mbunge wa Kwahani.

Na. 91

**Kumalizia Ujenzi wa Kituo cha Polisi Ghorofa  
Moja – Chukwani**

**MHE. AHMED YAHYA ABULWAKIL** aliuza:-

Je, ni lini Serikali itawaunga mkono wananchi wa Chukwani waliojitolea kujenga Kituo cha Polisi cha ghorofa moja kwa kumalizia ujenzi wa kituo hicho?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tafadhali, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil Mbunge wa Kwahani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Polisi Chukwani ulianza mwaka 2015 na unatekelezwa kwa mchango wa nguvu za wananchi na wadau werevu wa Ulinzi na Usalama huku Jeshi la Polisi likitoa wataalam wa ushauri na usimamizi kwa mafundi wake. Gharama ya ujenzi inatarajia kufikia kiasi cha shilingi 98,000,000/= hadi kukamilika kwake. Kwa sasa ujenzi umefikia hatua ya kumaliza (*finishing*) na gharama za kumaliza zinahitajika shilingi 40,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya utaratibu wa kutumia fedha za mfuko wa Tuzo na Tozo ili kumaliza ujenzi wa vituo mbalimbali vilivyosimama katika ujenzi kutokana na kukosa fedha kikiwemo Kituo cha Polisi Chukwani. Hata hivyo, kwa kushirikiana na wananchi na wadau werevu, Kituo hiki kitaendelea kukamilishwa ili kianze kazi ya kuwahudumia wananchi wa eneo hili na maeneo jirani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Abulwakil.

**MHE. AHMED YAHYA ABULWAKIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na yenye tija, naipongeza Serikali kwamba hivi karibuni itapata kituo kile na kuondokana na gharika ya majambazi waliovamia miaka ya nyuma. Kwa sababu hiyo, nashawishika kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Kwahani Eneo la Ng'ambo Jimbo la Kwahani ni Kituo cha Polisi cha muda mrefu tangu ukoloni; na kwa sasa hakikidhi mahitaji kuhudumia wananchi wakati huu: Je, Serikali ina

mpango gani wa kukitanua ili maofisa wetu waweze kufanya kazi kwa utulivu na ufasaha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amezindua soko jipya la kisasa eneo la Kibanda Maiti au tunaweza kusema Kibanda cha Demokrasia; linahudumia zaidi ya watu 10,000 usiku na mchana: Je, Wizara yako ina mpango gani kulinda usalama wa raia na mali zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu ya maswali hayo mawili tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi kubwa na wananchi wake hawakukosea kumchagua. Ninafahamu Mheshimiwa Mbunge amekuwa mstari wa mbele kwenye kuchangia maendeleo iwe kwenye elimu au vituo hivi vya Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali lake, ninafahamu pia kwamba hii miji inapanuka na ongezeko la watu linakuwa kubwa. Ongezeko hili linaendana na changamoto mbalimbali zikiwemo za ulinzi. Kwa hiyo, niendeleo tu kumsihi Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla tuendeleo kuhamasisha wananchi kwamba jukumu la ulinzi ni letu wote ili tuweze kushirikiana kwanza kuhakikisha kwamba tunafanya maboresho makubwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Serikali imefanyika; yako maeneo mbalimbali ambayo ujenzi umeendelea kukamilishwa na kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba Mfuko huu wa Tuzo na Tozo umefanya kazi kubwa. Katika mwaka 2020/2021 peke yake zaidi ya nyumba 431 zimekamilishwa ili kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira mazuri ya askari wetu kufanya kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Mbunge tuendelee kuhamasisha wananchi na Serikali kupitia mfuko huu tutaendelea kufanya maboresho makubwa.

Mheshimiwa Spika, mkakati tunaoufanya katika eneo hili la Kibanda Mauti, ni kweli kwamba kuna doria zinafanyika, wale wanaojihusisha na uhalifu wanaendelea kukamatwa na kufikishwa kwenye taratibu zetu za kisheria, lakini pia tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi, tunaendelea kuwashirikisha wananchi ili waweze kusaidia katika ulinzi na tunaendelea pia kushirikiana na vyombo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo kwa Jeshi la Polisi kule Zanzibar, washirikiane na Uongozi wa Soko katika eneo Mheshimiwa Mbunge amelitaja ili tupate eneo ambalo sasa tutaanza mkakati wa kujenga kituo katika eneo hili kwa sababu changamoto zimeongezeka na idadi kubwa ya watu katika maeneo haya na kuwepo kwa soko kunahitaji ulinzi madhubuti. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdulwakil usishangae, Mheshimiwa Naibu Waziri Mnyamwezi, badala ya Kibanda Maiti yeye kasema Kibanda Mauti. Mtani wangu huyu. *(Kicheko)*

Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 92

### **Kupitia Upya Sera na Sheria ya Uvuvi Nchini**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kupitia Sera na Sheria ya Uvuvi nchini ambayo inaonekana kutokidhi mahitaji ya wavuvi wadogo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kupitia Sera na Sheria ya Uvuvi nchini na katika kulitekeleza hilo, Wizara imekuwa ikifanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi ili ziweze kuendana na mahitaji halisi ya wakati husika na imekuwa ikifanya hivyo mara kwa mara. Kwa mfano, Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya Mwaka 1997 na kutunga Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 ambayo imezingatia mahitaji ya wadau wa Sekta ya Uvuvi na Uendelevu wa Rasilimali za Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ilifanya mapitio ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 6 ya Mwaka 1980 na kutunga Sheria Na. 11 ya Mwaka 2016 ili kuimarisha shughuli za utafiti nchini. Pia, katika mwaka 2020 Wizara ilifanya marekebisho madogo kwa maana *Miscellaneous amendments* kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 ili kuimarisha shughuli za ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kufanya maboresho makubwa kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 ili izeze kuendana na mahitaji halisi ya sasa ya kisekta ikiwemo kutatua kero mbalimbali za wadau wa Sekta ya Uvuvi hususan wavuvi wadogo na wakuzaji viumbe maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema K. Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika nashukuru, pamoja na jitihada kubwa na nzuri za Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, bado wavuvi wadogo hususan wa kutoka Mkoa wa Kagera, Geita, Mwanza, hawanufaiki ipasavyo hususan katika uuzwaji wa samaki aina ya sangara. Nasema hivi kwa sababu, mvuvi anapouza sangara kwenye viwanda vya kuchakata wanauza sangara

pamoja na mabondo ambayo yanakuwa ndani ya sangara kwa Sh.4,500 mpaka Sh.8,000 kwa kilo. Mabondo haya yana wastani wa bei kidunia kati ya Sh.1,000,000 mpaka Sh.2,000,000 kwa kilo. Kwa hiyo ningependa kufahamu, je, ni lini Serikali itaweka kisheria kuhusiana na bei ya sangara na bei ya mabondo iwe tofauti ili wavuvi wadogo wa kutoka kata...

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema K. Lugangira mabondo ni nini?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, mabondo ni mfuko wa hewa ambao unakuwa ndani ya mdomo wa samaki unamsaidia samaki kuelea, lakini mabondo hayo yanatumika kama chakula kwa wenzetu kule wa Asia, lakini pia mabondo haya yanatumika kutengeneza vipuri vya ndege, yanatumika viwandani, inatengeneza mpaka nyuzi kwa ajili ya operesheni au mtu anapoumia. Zaidi ya hapo, mabondo hayo pia yanatumika kutengeneza plastiki mbalimbali, ndio maana yanakuwa na thamani kubwa sana.

Mheshimiwa spika, kwa hiyo kwa jinsi sheria ilivyo sasa hivi, mvuvi anapokwenda kuuza samaki aina ya sangara, anauza sangara pamoja na mabondo yake ndani kwa bei ya Sh.4,500 mpaka Sh.8,000. Wakati haya mabondo peke yake yanaingizia Serikali kiwango kikubwa cha fedha kwa sababu bei ya kidunia kilo moja ya mabondo ni kati ya sh.1,000,000 mpaka Sh.2,000,000. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia suala hili kisheria ili yule sangara anapouzwa bei iwe tofauti kwa sangara na bei iwe tofauti kwa mabondo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni kwamba katika sekta ya uvuvi lipo kundi maalum la wanawake. Wanawake wana mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa Taifa letu, lakini bado kumekuwa na changamoto kubwa ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake wanaojihusisha na sekta hii ya uvuvi. Wengi wao tukiwaliuza wanasema changamoto hii inatokana na kwamba wanawake hawana

mitaji ya kutosha ya kuendesha kambi. Kule kwenye kambi wanakuwepo wanawake wanajihusisha na shughuli za uvuvi, lakini kuna ukatili wa kijinsia mkubwa sana unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kuiuliza Serikali, je haioni iko haja ya kutenga angalau asilimia 20 kutoka Mfuko wa Kuendeleza Uvuvi Nchini kwa ajili ya wanawake wanaojihusisha katika zao la samaki? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Maswali yako yameeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabondo ni kweli, ni boya, lililoko tumboni mwa samaki linalo msaidia katika zoezi zima la kuelea. Kwa miaka ya hivi karibuni biashara ya mabondo imekuwa ni biashara mpya, ambayo imeonekana kuwa na soko kubwa katika Nchi za Asia. Sheria na Kanuni tulizonazo hivi sasa, mabondo ni zao linalotokana baada ya kuchakatwa samaki. Kwa hiyo, kiwanda ambacho kinachakata samaki anapelekwa samaki akiwa mzima mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Sheria za Usalama wa Chakula na Ubora wake, ni lazima yule samaki anavyofikishwa pale kiwandani apelekwe akiwa mzima mzima katika umbile lake lote. Kwa hiyo, baada ya kumchakata, ndio sasa yanapatikana mabondo na mazao mengine ambayo yote sisi katika Sheria ya Uvuvi tunayatambua ikiwemo ile *skeleton*, lakini vilevile kichwa, mikia, ngozi na hata mafuta ya samaki yanayopatikana katika mwili wake.

Mheshimiwa Spika, mabondo yanachukua kati ya asilimia 1.8 mpaka asilimia 2.0 ya uzito mzima wa yule Samaki. Kwa hiyo, ili upate kilo moja ya mabondo inakuhusu uwe na



samaki zaidi ya mmoja, watatu, wanne hadi watano, ndio utapata kilo moja ya mabondo. Yenyewe ukubwa wake yanatokana na ukubwa wa yule samaki mwenyewe. Hata hivyo, niseme tu kwamba, rai na ushauri wa Mheshimiwa Neema Lugangira ni mzuri. Kwa kuwa sasa tupo katika utaratibu wa kuboresha sheria yetu, jambo hili ni jema, tunalichukua na sisi Serikalini tutakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, amezungumzia juu ya wanawake wachakataji na wafanyabiashara ya samaki na ukatili wanaofanyiwa katika shughuli zao hizo.

Kwanza, Sheria yetu ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, Kipengele cha 29 kinakubali na kinatoa mamlaka kwa Wizara kuunda Mfuko wa Kusaidia Uvuvi, kwa maana hiyo pia, vilevile, sera yetu ya Uvuvi ya mwaka 2015, tumeiboresha na katika kuboresha kwetu tumeweka jambo maalum la kuwasaidia wanawake na kwa hiyo, tutakuwa na jukwaa la kusaidia wanawake. Vilevile kama hiyo haitoshi, tutatambua moja kwa moja wanawake hawa wachakataji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimpongeze vilevile Mheshimiwa Neema Lugangira kwa kuwa akinamama hawa wanaoshughulika na shughuli za uvuvi na uchakati na wafanyabiashara wa samaki ni miongoni mwa wapiga kura waliopiga kura kuhakikisha kwamba yeye na Wabunge wengine akinamama wanaingia humu Bungeni na kwa hivyo amechukua jukumu la kutukumbusha kama Serikali na tutalifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuwa muda haupo upande wetu kabisa, tuchukue swali la mwisho la siku ya leo la Wizara ya Maji. Swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki. Mheshimiwa Mariki.

Na. 93

### **Tatizo la Maji Mkoa wa Katavi**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya maji katika Mkoa wa Katavi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Wilfred Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Mkoa wa Katavi ni asilimia 70. Serikali kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mpanda inatekeleza miradi miwili ya maji ambayo ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji na imeshaanza kutoa huduma ya maji. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa banio, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 24 kutoka katika chanzo cha maji lkolongo II na ujenzi wa tenki la lita milioni moja kwa ujumla wa mradi, unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa Manispaa ya Mpanda ambapo mji huo ni miongoni mwa miji 28 itakayonufanika na utekelezaji wa mradi wa maji kupitia fedha za mkopo kutoka Serikali ya India. Kazi hii inatarajiwa kuanza hivi karibuni na itachukua miezi 24. Aidha kupitia *RUWASA* utekelezaji wa miradi 30 unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021. Miradi hii, ikikamilika jumla ya vijiji 138 vya Mkoa wa Katavi vitakuwa na huduma ya maji ya uhakika, hivyo kutoa nafasi kwa wananchi kufanya kazi za maendeleo.

**SPIKA:** Muuliza swali, Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Naibu Waziri wa Maji kwa kutoa majibu

mazuri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga pesa nyingi sana kwenda katika miradi mbalimbali katika Mkoa wetu wa Katavi na miradi hiyo huonekana kwamba haikidhi kutokana na ongezeko kubwa la watu katika Mkoa wa Katavi hususan Wilaya ya Mpanda. Je, ni lini Serikali itatoa maji kutoka chanzo cha uhakika cha Ziwa Tanganyika ili kukidhi mahitaji ya maji ya watu katika Mkoa wetu wa Katavi hususan Mji wa Mpanda ambao unaongezeko kubwa sana la wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na Serikali ilitenga fedha nyingi sana kwenda katika Mradi wa Mamba katika Wilaya ya Mlele, Jimbo la Kavuu na mradi huo umekamilika, lakini mradi huo umekamilika kwa kuacha baadhi ya vijiji vingi sana kupata maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kuja kufanya ziara katika Mkoa wetu wa Katavi, kujionea jinsi gani Serikali imetenga pesa nyingi, lakini mradi huo umeonekana uko chini ya kiwango kwa baadhi ya vijiji vingi sana kutokupata maji? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Swali lake la kwanza, lini Serikali itatumia Ziwa Tanganyika kupeleleka maji katika Mji wa Mpanda na Mkoa wa Katavi? Wizara imeshakamilisha usanifu wa miradi yote mikubwa ambayo itatokana na maziwa yetu makuu, ikiwemo Ziwa Tanganyika. Hivyo, kwa mwaka ujao wa fedha tunatarajiwa kuanza kazi hizi endapo kadri namna ambavyo tutakuwa tunapata fedha ndivyo namna ambavyo miradi hii ya Maziwa Makuu itakuwa inatekelezwa. Hivyo, hata kwa Mkoa wa Katavi nao tutauangalia kwa jicho la kipekee kabisa kwa umuhimu wake na niendeleo kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa

Katavi hasa Mheshimiwa Martha akiwa Mbunge wa Viti Maalum ameweza kuwajibika mara nyingi sana kufuatilia suala hili na sisi kama Wizara hatutamwangusha Mheshimiwa Martha pamoja na Wabunge wote wanaotoka ukanda ule.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema mradi umekamilika lakini baadhi ya maeneo maji hayatoki, anatumani mimi niweze kufika huko. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili la Bajeti, tutapanga pamoja ratiba ambayo itakuwa rafiki kwetu sote ili niweze kufika Mpanda nijionee na kabla ya mimi kusubiri hadi Mwezi Julai huko, nitaagiza wahusika pale tuna *Managing Director* wa Mamlaka ya Maji.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tuna *RM* wa pale, nitawaagiza waanze kufuatilia ili mpaka mimi nitakapokuwa naelekea huko kwa ajili ya ziara ikiwezekana wawe wameshafanya marekebicho na maji yaweze kutoka. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuokoa muda, wageni walioko Bungeni asubuhi hii ni mgeni wa Mheshimiwa Aida J. Khenani, ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoani Iringa, Ndugu Edson Chidawali. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Mchungaji na Mwimbaji wa nyimbo za Injili wa Kanisa la Victory, kutoka Mkoani Iringa ambaye ni Mchungaji Dustan Mtoi. Mchungaji Mtoi karibu, amefuatana na Ndugu Mercy Chengula, mwimbaji wa nyimbo za Injili. Karibu sana Mercy Chengula. (*Makofi*)

Wageni 27 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni timu ya mpira wa miguu ya *Sahare All-stars* kutoka Hai, Mkoani Kilimanjaro, wakiongozwa na Mchungaji Yohana Mwampamba. Karibuni sana Sahare. Kumbe kule Hai kuna

na timu za mpira? Hongereni sana Sahare, tulikuwa hatujapa wageni wa kutoka Hai wa mpira wa miguu. *(Makofi)*

Kwa kweli Jimbo la Hai mna kila sababu ya kujivunia Mbunge wenu, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. Mbunge mpya huyu anachapa kazi, sio kama zamani kule. Wananichokoza wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Humphrey Polepole, anasema Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, mkutane mara baada ya maswali, katika Ukumbi wa Msekwa D. Serikali za Mitaa na Utawala, Kamati ya Mheshimiwa Humphrey Polepole, mkutane baada ya Maswali kule Msekwa D.

Katibu wa Bunge anapenda kuwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba kutakuwa na Kongamano na hili mlisikilize vizuri, kutakuwa na Kongamano linaloandaliwa na Viongozi wa Dini mbalimbali litakalofanyika katika ukumbi wa Chimwaga, Chuo Kikuu cha Dodoma, Siku ya Jumapili tarehe 18 Aprili, 2021, kuanzia saa nane mchana.

Aidha, Kongamano hilo litahudhuriwa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta binafsi. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote, mnaalikwa kushiriki kongamano hilo muhimu na mtatakiwa muwe mmeketi katika Ukumbi wa Chimwaga saa sita kamili.

Kwa hiyo ofisi itaandaa usafiri wa mabasi, yatakayoondoka kwenye Viwanja vya Bunge saa tano asubuhi. Wote Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kushiriki katika kongamano hilo. Mheshimiwa Rais ndio mgeni rasmi katika kongamano hilo. Waheshimiwa Wabunge wote, Jumapili saa nane mchana. Huo ndio mwisho wa matangazo yetu. Katibu.

**NDUGU STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI  
MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea tutakuwa na wachangiaji wachache, baada ya hapo tutaanza kusikia uchangiaji upande wa Serikali, ambapo Manaibu Mawaziri wataanza, wakihitimishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Geoffrey I. Mwambe.

Kwa sasa basi tuanze na Mheshimiwa Rose Busiga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mheshimiwa Rose Busiga, dakika kumi haraka haraka.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza kwenye Bunge hili Tukufu. Naomba kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameendelea kutulinda, lakini pia kulitetea Taifa la Tanzania kutokana na msiba mkubwa wa baba yetu, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Baada ya kupata msiba huo nilikuwa na huzuni kubwa sana na nililia kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu baba yetu alitupenda kutoka moyoni. Baba yule alikuwa na upendo usiokuwa na kifani, alikuwa na upendo ambao hauwezi kulinganishwa na mtu yoyote hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejifunza mambo mengi kutoka kwa baba yetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Moja ambalo nililojifunza kubwa sana, nimejifunza kwa namna alivyoweza kusimama na kutusaidia sisi wanawake kupata

nafasi katika Serikali hii ya Tanzania. Nitaendelea kumuenzi baba yetu kwa upendo mkubwa na ndio maana akaamua kumteua mama yetu Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wake kwa mara kwanza Tanzania ikapata Makamu wa Rais mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, safari yake ya miaka mitano ilikuwa ni safari yenye mafanikio sana na hatimaye tukauona uwezo wa mama yetu Samia Suluhu Hassan na mara tu baada ya matatizo kutokea mimi kama Mbunge wa Mkoa wa Geita, nilivyopata tatizo hilo nililia kwa huzuni sana, lakini nikajitia moyo nikasema, Wana wa Israel walipokuwa wakienda wakisafiri kwenye Nchi ya Kanaani, walikuwa na Mussa lakini hawakuweza kuifikia ile Nchi ya Kanaani, hatimaye Joshua ndiye aliyeweza kuwafikisha katika Nchi ya Kanaani. Hivyo nikaamini kabisa kwa matumaini yangu makubwa kuwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan atatufikisha kwenye Nchi ya Kanaani, nchi ya asali na maziwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze hili kwa uchungu mkubwa sana. Nasikitika na maumivu makali sana ambapo ninapooni wanambeza baba yetu aliyetusaidia mpaka leo sisi wanawake tunachangia hotuba nikiwa nina imani kabisa ya kuwa ninaweza kutoa mchango wangu na wananchi wangu wakanisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie kwenye hoja moja kwa moja katika Wizara ya Afya. Tumeona Serikali imeweza kufanya vizuri kwa kujenga Hospitali za Wilaya 99 lakini pia, tumeona imejenga Hospitali za Rufaa 10 na za Kanda tatu sambamba na hivyo imejenga zahanati 1,198 na Vituo vya Afya 487. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kufanya vizuri lakini pia, ninaiomba Serikali yangu kwasababu ni sikivu kuna maboma ambayo yapo ambayo wananchi wamechangia fedha zao za mfukoni wakajenga maboma yale na wanaisubiri Serikali iweze kumaliza. Nikitoa mfano, katika Wilaya ya Mbogwe kuna Kituo cha Afya kinaitwa Nghomolwa

wananchi wamekijenga kwa muda mrefu sana kituo kile cha afya kimeshafikia hatua ya ukamilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunao watendaji wetu wa kata, ndio wanaosimamia miradi hii ya ujenzi wa zahanati, ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini watendaji hawa wa kata wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kazi. Lakini, watendaji hawa hawa wa kata hata sisi Wabunge tukienda kwenye shughuli zetu za Kibunge, hawa hawa tunafika kwenye ofisi zao, ofisi zao hazifai, ofisi zao haziendani na yale ambayo wanatutendea sisi kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali sasa, waone haja ya kuwasaidia watendaji wa kata waweze kupata usafiri wa kufanyia kazi zao ili kuleta maendeleo kwenye kata zao. Lakini pia, niombe Serikali yangu kwa sababu ni sikivu iweze kuwasaidia watendaji hawa wa kata hata motisha tu inatosha... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, *caucus* imeamua iwe dakika tano tano kwa hiyo, sio uamuzi wangu nakushukuru. Imeamua hivyo kwasababu dakika ni chache ili... *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ROSE VICENT BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini naomba watendaji wa kata wafikiriwe kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi kwa wakati mgumu. *(Makofi)*

**MHE. SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji sasa ni tano tano upande wa CCM.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kufika hatua hii kama Bunge letu Tukufu. Lakini pia, kwa kutupitisha Taifa letu katika mtihani mzito tuliopita, lakini tumepita salama kama Taifa. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, naomba pia, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili, niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoza kwa kuniadini tena kwa mara nyingine na kunirejesha Bungeni kwa kura za kishindo. Wale waliojaribu kuchezea jimbo lile waliona moto walioupata na naomba wasiendelee kusogelea lile jimbo niko imara na wananchi wananiadini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyowasilisha, wakati akiwasilisha makadirio ya bajeti ya ofisi yake pamoja na Taasisi zilizo chini ya ofisi yake. Ninapompongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu natambua usaidizi mkubwa anaoupata kwa wasaidizi wake hasa dada yetu, mimi binti yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, hongera sana mwanangu unachapa kazi vizuri, unatuheshimisha wanawake hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dakika chache naomba niseme mambo machache sana nayo ni; kwa nini Tanzania tumeingia uchumi wa kati miaka mitano kabla ya muda tuliojipangia? Tumeingia uchumi wa kati kwasababu ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Taifa letu, chini ya uongozi makini wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu amefanya uwekezaji kwenye miradi mikubwa na ukisoma taarifa ile ya Benki ya Dunia wameeleza wazi ni kwanini Taifa letu tumeweza kupiga hatua hii kubwa? Kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali yetu na nitoe pongezi sana, kwa Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mwongozo sahihi kwamba, miradi yote mikubwa inakwenda kutekelezwa mpaka ikamilike, pongezi sana kwa Serikali yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi mkubwa anaoufanya kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapompongeza hili niombe sana sana, watanzania tuwe makini na tunachokiongea katika muda huu. Tunapoanza kubeza miradi iliyowekezwa na Serikali yetu ya awamu ya tano tunamuudhi Mwenyezi

Mungu. Naomba tusimame kwa pamoja na tutambue kwamba wapo wenzetu ambao walifanikiwa kuvuka kutoka kwenye *level* ndogo ya uchumi kwenda kwenye *level* kubwa ya uchumi lakini walianguka na wakarudi kwenye uchumi wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Taifa letu tunapanda kuingia kwenye uchumi wa kipato cha kati, tulishuhudia dunia kuna nchi tatu zilishuka kutoka uchumi wa juu kuja uchumi wa chini, makosa yaliyofanyika ni haya tunayoyaona watanzania tunafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge sisi ni viongozi, tuonyeshe mshikamano dhahiri, mshikamano wa kuyaendeleza yote mazuri ambayo yalianzishwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mengi mazuri yaliyotendwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano, ni kuleta makao makuu kwa vitendo Jijini Dodoma. Niombe sana tunapokwenda sasa kuanza utekelezaji wa bajeti yetu hii, tuone miradi mikubwa iliyokuwa inaletwa Dodoma na Serikali ya Awamu ya Tano inakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan ametoa muelekeo, uwanja wa ndege wa Msalato utekelezwe kwa haraka. Tumenunua ndege nyingi... (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, dakika tano zimeisha

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Awack.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kuniona na kunipa nafasi hii awali ya yote

nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uzima na tunaendelea na shughuli zetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yake. Lakini niipongeze kazi nzuri inayofanywa na Serikali yangu, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ukiangalia kazi iliyofanywa na Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanga tunauona, miradi ni mingi imetekelezwa na Awamu ya Sita sera yetu kazi inaendelea, maana yake tunaenda kukamilisha miradi ile yote. Na sisi tuna Imani na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwamba, tutaenda kwa kasi zaidi kwani alikuwepo kwenye maandalizi yote na ile awamu ya tano kazi walifanya vizuri pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye eneo la ajira. Hasa suala la ajira kwa vijana, vijana wetu wengi wamemaliza shule wako mtaani hawana kazi na tumekuwa na mjadala mkubwa kwenye eneo la elimu, kama elimu yetu kweli inaendana na mazingira ya kwetu.

Mheshimiwa Spika, lakini, vijana wengi kuanzia wale ambao hawajakanyaga darasani na wengine wana *masters* wanafanya kazi ya bodaboda. Ninachoomba Serikali yangu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi kundi hili limekuwa kubwa, lina watu wa aina mbalimbali tujielekeze. Ile mifuko ya maendeleo ya vijana iangalie kundi hili muhimu na vijana hawa wa bodaboda ambao ni kundi kubwa kwa sasa, tuwatengenezee utaratibu maalum wa kuwatoa kwenye kazi ile ya bodaboda na hatimaye nao wapate uchumi kupitia kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, tuwajenge ili waelewe kwamba kazi ya bodaboda ni sehemu ya ajira, lakini wanahitaji kuendelezwa kutoka hapo. Kwenye zile asilimia 4 za vijana zilizoko kwenye halmashauri, tuwaangalie hao ambao tayari wameshaanza kujishughulisha. Fungu lile la mfuko wa vijana ambao uko chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, tuangalie hili kundi ambalo limeshaanza kujishughulisha, ili hatimaye waweze

kupata shughuli zilizo imara ambazo zinaweza zikawaingizia kipato. Kwani kwa sasa, kundi lile linaonekana kama kundi la watu ambao hawana nidhamu kihivyo katika uendeshaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, hawafuati sheria, wakati mwingine nao wana hasira na jamii nyingine. Ukiona kijana wa bodaboda ukimgusa tu, wanakusanyika utafikiri ni vita kwasababu, watu wamekosa amani. Sasa, tutengeneze mfumo ambao unaweza kuwatoa kwenye kazi ile wanayoifanya. Kazi ya bodaboda ukiifanya miaka miwili kifua hakifai kwasababu, wanavyoendesha hawafuati sheria. Hawachukui tahadhari, hawajilindi na pia wanakimbizana na polisi sana. Sasa badala ya kukimbizana na vijana hao tuwatengenezee utaratibu mahsusi wa namna ya kuwafundisha kufata sheria na zile shughuli zao ziweze kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema suala la vijana hasa na kwa eneo la kuwawezesha lakini pia tunalo eneo la ardhi. Ardhi imekuwa changamoto kubwa na sababu kubwa ni kwamba, ardhi tuliyonayo haiongezeki na sisi tunaongezeka. Na ukiangalia wengi ambao wana ardhi zilizo kubwa yawezekana ni wazee wetu ambao hawakwenda shule sana, au wakati mwingine hawajapata bahati na hizo ardhi wamepata kwa njia zile za asili. Sasa hivi watu wanaohitaji ardhi kidogo wameanza kuwa na elimu elimu kwasababu, ardhi yetu haijapimwa yote kumekuwa na dhuluma sana kwenye eneo la ardhi. Ninachoomba Serikali yangu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi tujielekeze kwenye eneo la ardhi. Tuhakikishe watu tunawamilikisha ardhi zao kwa mujibu wa sheria, ili kuondoa migogoro mingi iliyojaa kwenye ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ofisi za Wabunge nina uhakika wenzangu pia mnapata tatizo kama mimi, kuna malalamiko mengi ya wazee wetu kudhulumiwa ardhi zao. Na ukifuatilia, mzee utakuta hana nyaraka atakuambia mwaka sabini na ngapi aligawiwa ardhi hiyo, sasa mtu amechukua na kwasababu anajua jua kidogo taratibu,

inakuwa ngumu sasa kubatilisha kwamba hajaipata kisheria. Na ardhi ni chanzo kizuri cha mapato, tukiipima ni imani yangu malalamiko ambayo tunayo kwenye upande wa *TARURA* tutapata fedha hapa. Kwani watu wataanza kulipa kodi za ardhi. Ninachoomba eneo hili tuliangalie kwa umakini mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo eneo la miundombinu kwasababu ni changamoto ya kila sehemu. Tumeongea sana namna ya kupata fedha ili angalau *TARURA* iweze...

**SPIKA:** Ahsante sana

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Samweli Hhayuma. Nishakutaja Mheshimiwa Daniel Awack na utafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupigania uhai sote tukiwa salama ndani ya ukumbi huu. Awali ya yote nishukuru sana Chama changu lakini vile vile nishukuru sana Serikali ya awamu ya tano, kwa kazi kubwa sana waliyofanya kazi hiyo kubwa waliyofanya imeweza kuleta Wabunge asilimia kubwa ndani ya ukumbi huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wana CCM waliopitia Chama Cha Mapinduzi wanajua kwamba, chama chetu mwaka wa 2010 ilikuwa na hali gani? Lakini vile vile, unajua changamoto tuliyokuwa nayo mwaka 2015. Lakini baada ya jemedari Hayati Dkt. Magufuli kuingia madarakani mwaka wa 2015 na ndio matunda sasa yameonekana kwa watanania, kuamini Chama Cha Mapinduzi mwaka wa 2020 kwa kazi kubwa iliyofanyika chini ya jemedari na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nishukuru sana Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Dkt. Bashiru Ally kwa kusimamia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Mbunge wa Jimbo la Karatu ni takribani miaka 25 Jimbo hili halijaweza kuleta Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo, usimamizi mzuri wa Serikali ya awamu ya tano watanzania wengi walikiamini Chama Cha Mapinduzi kwasababu, kuna muda ulifikia kwamba, watanzania walifikiri kwenda kutafuta chama mbadala nje ya Chama Cha Mapinduzi. Lakini mwaka wa 2015 Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoingia madarakani sasa watanzania walio wengi wakaamini kwamba, Chama Cha Mapinduzi kwamba ni chama cha kimbilio ya walio wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme eneo la fidia, katika Jimbo langu la Karatu pale kuna uwanja wa ndege wa *Lake Manyara*, pale Serikali iliwaambia itawapa fidia takribani sasa miaka sita wananchi wale hawajaweza kupata fidia. Nilikuwa naomba Serikali katika bajeti hii ya ofisi ya Waziri Mkuu, waangalie maeneo haya. Serikali yetu wanaweza kusema tunatoa fidia lakini baadae inaweza kuchukua miaka sita wananchi wale hawaruhusiwi kufanya jambo lolote katika eneo hili la *Lake Manyara*.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri ifikie muda kwamba, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na nafikiri ni sikivu, waweze kuangalia maeneo haya ya fidia. Wananchi wetu wanateseka na wakati huo ukifika kwenye haya kama Mbunge, unakutana na maswali magumu kweli na unashindwa kutoa majibu kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikihama kutoka eneo hili la fidia niende kwenye eneo la maji pale Jimboni kwangu Karatu. Pale Jimboni kwangu Karatu Waziri Mkuu ni shahidi alitembelea lile Jimbo la Karatu, pale kuna bodi mbili za maji, kuna bodi ya KARUWASA, na kuna bodi ya KAFIWASA, wana wachaji wananchi wale wa jimbo lile kwa bei tofauti. Hawa KAFIWASA wanachaji bei ya shilingi 3,500/= kwa *unit* KARUWASA, wanachaji shilingi 1,700/= kwa *unit*. Na wakati

Waziri Mkuu alitembelea jimbo lile wakati akijinadi yeye ni mgombea wa Chama Cha Mapinduzi kwa wakati huo, lakini vile vile na Rais wa Jamhuri ya Muungano tarehe 24 mwezi wa 10 alikuja jimboni Karatu na akasema hili halimshindi kurudisha bei moja ya shilingi 1,700/=.

Mheshimiwa Spika, kwasababu hawa watu wa KAFIWASA hata hawakaguliwi na Serikali wanajiendesha wenyewe, wanakusanya hela wenyewe, lakini wakati huo wakichaji/wakiwaonea wananchi kwa shilingi 3,500/=. Na hili tumelilalamikia kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka 15 imekuwa ngumu kutekelezwa kwa Serikali, sijajua ni kwa nini? Kwamba, hawa watu wanaweza kunyonya wananchi wa Jimbo la Karatu kwa shilingi 3,500/= kwa *unit* halafu hakuna jambo lolote na hatua yoyote inayochukuliwa kupitia Wizara husika katika eneo hili la bei kubadilishwa, kuwa na bei moja katika Jimbo lile la Karatu kwasababu, kuna bei ya shilingi 3,500/= kwa *unit* na kuna bei ya shilingi 1,700/= kwa *unit* na inashindikana kuja bei ya shilingi 1,700/= kwa *unit* sijajua shida ni nini katika Wizara hii ya Maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengi wameongelea suala la tembo, kwa Jimbo langu nimezungukwa na hifadhi mbili, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya *Lake Manyara* lakini watu wanasema kwenye Wizara ng'ombe akiingia ni shilingi 100,000/= lakini...

**SPIKA:** Tayari Mheshimiwa

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Tupange kwenye Bunge hili tembo wakiingia kwenye eneo la wananchi ni shilingi ngapi?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikutaja Mheshimiwa Halima Mdee, ni dakika 10.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii, la kwanza, mchango wangu utajikita kwa Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria, kuhusiana na Hifadhi ya Jamii na niipongeze sana kamati kwa kufanya kazi nzuri na nitaongezea hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi imeanzishwa sababu moja kubwa, ni kuangalia mustakabali wa wafanyakazi wetu pale wanapokuwa watu wazima na kustaafu na kulinda maslahi yao baada ya umri wa kustaafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini mifuko hii iliwekwa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutambua nafasi ya Waziri Mkuu mwenyewe na unyeti wa mifuko hii na ikitarajiwa, Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake waweze kusimama kidete, ili kulinda mifuko kwasababu ukilinda mifuko, umelinda watumishi wa Taifa hili. Tunavyozungumza Hifadhi ya Jamii na hii Mifuko maana yake tunazungumzia watumishi wa sekta ya umma na tunazungumzia watumishi wa sekta binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa mifuko huwa inafanya uwekezaji, na mifuko duniani kote inawajibu wa msingi wa kuisaidia Serikali kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo. Hilo halina ubishi duniani kote, lakini, changamoto iliyokuwa hapa kwetu Tanzania na ambayo ninaomba sana, Mheshimiwa Jenista utujibu sio umjibu Halima hapana, jibu wafanyakazi wa Taifa hili ili wapate matumaini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwanini? Mifuko inawekeza katika mazingira mawili, zingira la kwanza kuikopesha Serikali na Taasisi zake kwa riba. Serikali inakopa kwa ajili ya kuingiza kwenye shughuli za maendeleo inadhamini Taasisi zake zinakopa, inatakiwa ilipe kwa riba. Lakini la pili, inashiriki katika uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya ujenzi ama wao binafsi ama kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. (Makofi)



Mheshimiwa Spika, mdudu mkubwa, donda ndugu, zito, ilililo sugu kabisa ni upande wa Serikali. Pesa inazokopa, inazotakiwa ilipe kwa riba, pesa ambazo Serikali inadhamini taasisi zake zikope kwenye Mifuko ya Hifadhi ambayo inatakiwa ilipe, hailipi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018, mtanisahihisha kama nimekosea, tuliunganisha mifuko tukaambiwa kwamba hii mifuko inaunganishwa ili ufanisi uwe bora zaidi. Nimeona hotuba ya Waziri Mkuu imesema wamepunguza gharama za uendeshaji, *yes!* Lazima ipungue kwa sababu watu wamekuwa wachache, mifuko ni miwili lakini usugu upo! Zile fedha mlizokopa mna kigugumizi gani kurudisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester Bulaya amezungumza juzi, kwamba madeni yale ya kawaida kwa taarifa zenu wenyewe kupitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni 2.7 trilioni. Pia mnafahamu kuna fedha zingine shilingi trilioni 7.1 ambazo pia *PSPF* walipewa jukumu kulipa wastaafu ambao walikuwa wamekidhi umri lakini hawajachangiwa, *almost ten trillion!* Kwenye mifuko hatulipi. Kama Serikali ina uwezo kila Mwaka wa Fedha kutenga shilingi trilioni 8 mpaka 10 kulipa madeni ya nje ya Serikali ama ya mabenki, tuna ugonjwa gani kushindwa kutenga hata shilingi trilioni moja moja basi kila mwaka tuisaidie mifuko yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana na inauma madeni mengine yalikuwa yameiva toka 2007, 2008, 2010, 2014 Serikali inatoa ahadi hapa, haitekelezi! *PSPF* ikachoka, ikafilisika, tukaunganisha ili kuziba mashimo. Hatuwezi kwenda hivi!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niombe...

## TAARIFA

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, mimi ningeshukuru au ningemuomba Mbunge anayezungumza aelewe kwamba Serikali ni mdhamini wa mifuko hii. Serikali ina namna nyingi ya kupata fedha wakati wowote, hawezi kusema kwamba hii mifuko imefilisika. Haiwezi kufilisika kwa sababu Serikali ina uwezo wa kutengeneza fedha saa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie kwamba deni analosema yeye hamna tofauti na deni ambalo linalipwa kwa wakati na Serikali ina namna yake kwa sababu inaweza ikatu-*tax* sisi saa yoyote ile. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuogopa kwamba iko siku Serikali itashindwa kulipa hiyo mifuko. Hivyo ndivyo ilivyo duniani kote kwamba fedha ya mifuko inatumika na njia salama kabisa kutumia fedha ya mifuko ni kwa Serikali kutumia zile fedha kwa kufanya miradi ya muda mrefu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Serikali haikosei chochote.

**SPIKA:** Ahsante sana. Taarifa hiyo ipokee Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ninamheshimu sana Mheshimiwa Kimei na ametumikia nchi hii muda mrefu sana. Sitaki kumjibu kwa sababu nikimjibu naweza, ngoja niendele. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Msamehe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Namsamehe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme hivi, Serikali imekopa fedha, iliingia makubaliano na mifuko, tutakopa hizi fedha, tutarudisha ndani ya muda fulani, tutakopa hizi fedha kwa kuzidhamini taasisi tutarudisha ndani ya muda fulani tena kwa riba. Navyozungumza Mkurugenzi mstaafu mpaka sasa

Serikali inadaiwa zaidi ya shilingi trilioni 10 kwa vitabu vyenu wenyewe! Sasa hiyo shilingi trilioni 10 basi hata lipa kidogo kidogo watu wapate matumaini, hulipi unakauka tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajenga nyumba moja, yaani wala tusigombeo fito. Tunawakilisha wastaafu wa nchi hii. Leo Mbunge aniambie kwenye Jimbo lake sasa hivi kutokana na Serikali kutokurudisha fedha, kuna matatizo makubwa sana kwa wastaafu kulipwa ndani ya muda. Zamani ilikuwa mtu anastaafu, ndani ya miezi sita pesa zimeshaingia. Sasa hivi kuna wengine wanastaafu mpaka wanakufa fedha hazijaingia. Hii mifuko ingekuwa ina hela mambo yangeenda mswano. Nashauri Mheshimiwa Kimei akasome...

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mzee naomba utulie basi.  
*Please!*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa tena. Hilo analosema lote ni sehemu ya Deni la Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kimei sijakuruhusu bado. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nachoshauri...

**SPIKA:** Sasa nakuruhusu Mheshimiwa Kimei.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa. (*Kicheko*)

## T A A R I F A

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimuelimishe kwamba hilo analosema kwamba Serikali haijalipa ni sehemu ya Deni la Taifa ambalo kila siku tunasema linakua. Ukweli ni kwamba Deni la Taifa ni kidogo sana kwa sababu ya *assets* Serikali ilizoweka. *Net worth*

ya Serikali ni kubwa hasa ukiangalia miradi hii ya muda mrefu ya kujenga reli, kununua ndege na kadhalika hizo ni *assets* zipo. Ukweli ni kwamba ukiondoa *liability* na *assets* tulizonazo ni kama zina-*balance*. Kwa hiyo, hakuna tatizo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima pokea Taarifa hiyo, hakuna tatizo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, napokeaje? Tatizo lipo kwa sababu yeye anasema haya madeni ni sehemu ya Deni la Taifa, si ndiyo? Deni la Taifa hapa kila mwaka na mtaona kwenye bajeti ya mwaka huu maana naye ni mpya, sitaki kutumia lile jina lingine, utaona katika bajeti ya mwaka huu tunatenga shilingi trilioni 8 mpaka 10 lakini ujulize...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nimekuona, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kwamba ningesubiri wakati wa kujibu hoja na nilikuwa nimejipanga kutoa maelezo ambayo yangeweza kusaidia Bunge lako Tukufu na wafanyakazi kuendelea kuwa na matumaini na usimamizi wa sekta kiujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi lakini nitakuja kutoa maelezo baadaye, tunakubaliana na utaratibu wa Kiserikali wa CAG (Mdhibiti wa Fedha za Serikali) kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya hali ya sekta zote ikiwemo sekta hii ya Hifadhi ya Jamii. Hayo madeni anayoyasema Mheshimiwa Halima, yako madeni ambayo yana uhalali, yanajionesha wazi lakini anapooengeza yale madeni mengine yanayofika karibu kama shilingi trilioni kama saba anazosisema nadhani angerudi akafanye uhakiki vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini nachotaka kusema hapa tulipoamua kufanya *merging* ya mifuko ilikuwa ni kazi ya Serikali kwa sababu iligundua kuna tatizo kwenye sekta na ndiyo maana ikaamua kufanya *merging* ya mifuko. Kama Serikali iliona kuna tatizo na kufanya *merging* nadhani ilikuwa ni hatua mojawapo ya kusaidia na anachokizungumza Halima ni ile *pre 99* ili isiue sekta nzima ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie sasa hivi tumeamua kutekeleza takwa la kisheria la kufanya *actuarial* ili kupata taarifa sahihi za hali ya mifuko jinsi ilivyo. *Actuarial* ndiyo itakayotusaidia kujua hali ya mifuko na nini kifanyike kwenye madai, madeni na kuboresha sekta ili iweze kuwa *sustainable*.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya haraka haraka tu, wastaafu wa *PSSF* ambao ni takriban kama 132,670 wamekwishakulipwa mafao na tulitoa taarifa kwenye Kamati. Tunabakiwa na hayo madeni ya nyuma ya wastaafu kama 6,793. Kwa hiyo, hao sasa ndiyo tunaendelea nao. Juzi Hazina wametupa shilingi billioni moja ili tuweze ku-*clear* hawa wengine waliobakia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo matatizo yapo lakini yako *manageable* kwa sababu Serikali inasimamia na kuhakikisha kwamba inatafuta suluhu.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima, pokea Taarifa hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista amesema anakubaliana na lile la shilingi trilioni 2.7, hili la shilingi trilioni 7.1 ana mashaka nalo. Namshauri mambo yafuatayo, nenda kasome Ripoti ya Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2013/2014 labda nirejee. Ukurasa wa 96, inasema hivi; kwa mujibu wa Ripoti ya Kikosi Kazi na Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *TK/02/Januari 2015* ya mwaka unaoishia tarehe Juni 2013, Deni la Serikali ni shilingi za Kitanzania, kwa kipindi hicho kabla halijafika sasa hivi shilingi trilioni 2.7 lilikuwa shilingi trilioni 1.8. Anasema deni hilo

halijajumuisha jumla ya shilingi za Kitanzania trilioni 7.1 ambalo ni deni la Serikali linalodaiwa na *PSPF* tangu 1999 ambapo *PSPF* iliwalipa mafao wastaafu waliokuwa hawachangii lakini wanatakiwa kulipwa mafao kwa mujibu wa sheria. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Mkaguzi Mkuu na hizi shilingi trilioni 7.1 hamjawahi kuzilipa. Mimi ni mkongwe nimekuwa kwenye hili Bunge na ripoti hizi za *CAG* ni endelevu. Hamuwezi kutuambia ripoti ya mwaka huu inaziba ile nyingine wakati hamkutekeleza ile nyingine. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, Taarifa ndogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Waziri amesimama tena.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Halima kwamba hiyo ripoti amesema ni ya mwaka 2013/2014. Ndiyo maana tuliamua mwaka 2016, 2017 na 2018 ili kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la *pre 99* hiyo anayoizungumza kwa kufanya *merging*. Unapofanya *merging* unaunganisha mifuko, *assets* zote na kila kitu. Ukishaunganisha hiyo mifuko inakusaidia sasa ku-*treat* yale matatizo ambayo yalikuwa siku za nyuma. Mheshimiwa Halima *essence* ya kufanya *merging* ilikuwa ni *sustainability* ya sekta kwa kuzingatia hiyo *pre 99* ambayo umesema ni Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachotaka kumshauri, aache tufanye hiyo *actuarial valuation*, itatusaidia kujua hayo yote yameshafanyika kiasi gani? Naomba niliambie Bunge lako Tukufu tayari *PSSF* imeshafanyiwa utathmini na ripoti sasa hivi ndiyo inaletwa Serikalini ili iweze kusomwa na kuona hayo mawanda yote na namna sasa ya kuweza kuitendea kazi ripoti hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa pokea taarifa hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kukiri kwamba ile shilingi trilioni 7.1 ilikuwepo lakini yeye anafikiria kwa ku-*merge* ndiyo unaondoa tatizo. Unapo-*merge* kitu unachukua zile *assets* na *liabilities*. Sasa moja kati ya *liabilities* zilikuwa ni madeni ya shilingi trilioni 7.1. Jamani, kiroho safi tu, yaani mimi hapa wala sina *beef* na mtu, nachotaka ni tuangalie kwa namna gani mifuko yetu hii, nakiri kwamba Serikali haiwezi kulipa kwa mkupuo lakini basi turudishe kidogo kidogo ili kuifanya iwe *sustainable*. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, leo Kamati inatuambia, kuna miradi ya ujenzi zaidi ya minne ya Tungi, Tuangoma, Kijichi, Mzizima /na // ambayo inagharimu shilingi bilioni 495 za wastaafu wetu watarajiwa zimekuwa *injected* ile miradi imeshindwa kuonesha *multiplier effect*. Nyumba zimejengwa, hakuna nyumba iliyouzwa tunaishia kupangisha tena tunapangisha bila mikataba ambapo haikuwa lengo. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, leo kaka yangu Wakili kapendekeza tunaomba kuja na mkakati tufanye *mortgage financing*, tushirikiane na *BoT* ambayo ndiyo ina jukumu la kusimamia masuala ya uwekezaji kwa kushauriana na hii mifuko. Tushirikiane na *BoT* na mabenki, uzuri Tanzania tuna sheria ya *mortgage financing*, tufanye huo utaratibu, wananchi waweze kukopeshwa na mabenki kununua zile nyumba, zile nyumba zitumike kama *collateral*. Jambo limeshatokea kama tulivyosema juzi kwenye *ATCL*, zimeshakuja hatuwezi kuzichoma lazima tupange utaratibu wa kufanya mambo yaboreke zaidi. Kwa hili naomba tuangalie utaratibu wa *mortgage financing*, tushirikiane na *BoT* kwa sababu inasimamia mabenki yetu, wananchi wapate nyumba kwa sababu sekta ya nyumba kwa Tanzania bado iko chini sana; Serikali ipate na mashirika yetu yaweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tupate majibu, siyo kwa sababu Halima amezungumza bali tupate majibu

wa nini muelekeo wa mifuko yetu kwa mustakabali wa Taifa na watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini sio kwa umuhimu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tayari muda umekwisha.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Toufiq Turkey. Mheshimiwa Mwakasaka dakika tano.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA;** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nichangie kidogo kwenye hii bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dakika ni chache sana na mimi nitaongea machache mengi wengi wameshazungumza. Kwanza, naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naomba kama mimi binafsi au mtu wa maadili nitoe ushauri kidogo. Kuna madeni mengi ambayo yamekuwa yakizungumzwa; madeni ya wakandarasi mbalimbali ambayo yanaongezeka kila siku kwenye sekta ya ujenzi waangalie namna gani watapunguza madeni haya kwa sababu kila siku kuna shida lakini Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nilisema nitatoa ushauri wa kimaadili kidogo. Ni vizuri kumsema mtu akiwa yupo ili aweze kujibu lakini unapomsema mtu hayupo na hawezi kujibu kunakuwa na mashaka na ndimi mbili huwa si nzuri. Nchi sasa hivi imetulia sana huko nje maana yake wananchi wana imani na Serikali iliyopo ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Sasa wanaanza kutokea baadhi ya Waheshimiwa



wenzetu kuponda vitu ambavyo vilifanywa katika awamu iliyopita, si vizuri. Kama kitu ulikisifia jana, leo ukaanza tena kukiponda wananchi wanachanganyikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, miradi yote hii iliyoanzishwa ndiyo ilitufanya Wabunge wengi turudi leo humu Bungeni nikiwemo na mimi. Unafahamu kwamba Tabora Mjini haijawahi kurudisha Mbunge mara mbili ni mimi niliyesimama hapa Mwakasaka, ni kwa sababu ya mafanikio ya Awamu iliyopita chini ya Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli pamoja na Mheshimiwa Mama Samia. Miradi ile ile iliyotupitisha leo tunapoanza kuiponda tunawachanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tusiwe na ndimi mbili na hata kwenye Biblia sijafahamu ni kitabu gani lakini nadhani ni Mithali, Mwenyezi Mungu anasema kheri uwe moto au baridi, ukiwa uvuguvugu utatapikwa maana yake huna msimamo. Tuwe na msimamo, wananchi wana imani na Serikali iliyopo ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, tusiwachanganye kwenye miradi ambayo inaendelea. Bahati nzuri Mheshimiwa Samia ana uwezo mkubwa, miradi hii itaendelea na tuna imani kabisa kwamba nchi yetu itasonga mbele. Tuache kuwachanganya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni machache tu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq Turkey, dakika tano.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan tungali sote salama. Pia tuwatakie rehema waliotutangulia mbele za haki wazee wetu hususan Hayati Rais mpendwa wetu Magufuli.

Mheshimiwa Spika, haijapata kutokea mabadiliko ya Serikali ya namna hii na sisi wananchi na Serikali kwa ujumla, sote tukawa kitu kimoja. Lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu

*Subhanah-Waatalah.* Pia na Waheshimiwa wengine tukawa tunajiliza, Hayati Dkt. Magufuli Waziri Mkuu alimtolea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika kubarikiwa huku, tumebarikiwa kupata kiongozi aliyekuwa mtumishi mtiifu mno. Katika kubadilika kwa Serikali hii, kiungo kikubwa bado kingalipo. Kwa hiyo, tuendeleeni, ilikuwa Bunge hili hili tukampitisha kwa kura zote kabisa, kwa heshima zote kabisa, kwa hiyo, tuendeleo kushikamana na Serikali yetu kuhakikisha uchumi wetu unaendelea kuwa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumwombe sana Rais wetu wa sasa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu ampe hekima, busara na maono (maana viongozi huwa wanapata maono) yale ya kuipeleka Tanzania yetu mbele kama waasisi wa nchi hii walivyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuongelea kwa uchache katika suala zima la uwekezaji. Uwekezaji hauwezi kupatikana ndani ya nchi yetu kama elimu hatujaipa kipaumbele. Hivi karibuni nilipata bahati ya kwenda Kenya nikakaa na viongozi wa pale, katika masuala waliyokuwa wanaongelea wakasema Tanzania sisi tunaionea wivu sana, kwa sababu wana rasilimali za kila aina kuliko sisi; lakini sisi tuna rasilimali moja ambayo Afrika nzima hawana, ni rasilimali nguvu watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *literate level* ya Kenya ni 93%. Vile vile elimu yao wanasema ni tofauti na elimu ya watu wengi sana. Afrika watu husoma kwa ku-*pass*, sisi tunasomesha vijana wetu kwa kufahamu. Mara nyingi sana, ndiyo maana utaona Tanzania hapa tuna ma-*degree*, wengine wana *Masters*, wengine Ma-*professor*, lakini inapokuja katika uelewa na katika suala zima la dunia inavyoenda, *exposure* ni tofauti. *Attitude* yetu iko mbali. Ndiyo maana katika suala zima la uwekezaji, watu wanatafuta ma-*expatriates*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona Wabunge tunavutana sana katika suala la kwa nini tunachukua watu kutoka nje? Hakuna

mtu anataka kutoa gharama mara tatu, mara nne, mara tano kuwalipa watu wa nje na wakati Watanzania wapo, lakini bado vijana wetu wako nyuma mno kielimu. Tunafanyaje sasa katika suala hili? Ni lazima turudi tena, tutazame namna gani tunaweza kuwasaidia wanafunzi wetu kuhakikisha wanaendana na matakwa ya dunia ya sasa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Armania ni *Eastern Europe Country*, sasa hivi kuanzia Darasa la Sita wanafundisha *subject* ya *coding*; masuala ya *software*. Miradi yote karibu sasa hivi watu wanasema tunataka sisi tuwe na mfumo, lakini mifumo yote inatoka nje ya nchi. Hizo ndio ajira za baadaye. Watu duniani wanakadiria, ndani ya miaka 10 ijayo akili zetu zitakuwa hazifanyi tena kazi, itakuwa ni suala zima la *artificial intelligence*. Vijana wetu tumewatayarisha vipi kuhakikisha ajira za baadaye hatuzikosi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ajira za mwanzo zilikuwa za viwanda, tunatafuta watu wa kulima. Ajira za pili zikaja kuwa ni masuala mazima ya vibarua kwa ajili ya viwanda. Ajira za tatu zimekuja katika kutengeneza viwanda. Ajira zijazo ni namna gani dunia itaenda ki-*ICT only*; *Artificial intelligence*? Vijana wetu tuwatayarisheni katika ajira za baadaye. Hizo milioni nane zitakuwa ndoto. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Toufiq Turkey. Niliangalia muda, unaanza kwenda. Mheshimiwa Dkt. Alice Kajage, atafuatiwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mohamed Kigua.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote ambao Wizara zao ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Watendaji na Wajumbe wa Kamati wote wanaohusika na Wizara hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali, kwa maana ya kupambana na masuala ya *HIV/AIDS* mahali pa kazi, pia kuna mipango mingi sana ambayo imeendelea kutekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuendelea kupambana na masuala haya sehemu za kazi. Kuna mpango unaoitwa Mpango wa Utatu unaoshughulikia masuala ya *HIV/AIDS* mahali pa kazi. Mpango huu umekuwepo toka mwaka 2008. Kwa hiyo, nashauri kama inawezekana, mpango huu ufanyiwe tathmini kwa jinsi ambavyo umefanya kazi kwa nia njema tu ya kuuboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima la zile Kamati za UKIMWI mahali pa kazi pamoja na elimisharika. Naishauri Serikali ifanye usimamizi mzuri, Kamati ziwe *active* mahali pa kazi. Zitasaidia wale waathirika watoe hali zao za afya yao kwa waajiri wao wawe wawazi wapate huduma, lishe, wapunguziwe majukumu ya kiutendaji mahali pa kazi kama ambavyo Mwongozo wa Utumishi wa Umma Namba 2 wa 2006 unavyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ila suala la saratani ya mlango wa uzazi, linahusiana sana na suala la *HIV/AIDS* kwa akina mama. Kwa sababu, ugonjwa huu asilimia 70 unasababishwa na mdudu anaitwa *Papillomavirus 15 and 16*. Pia sababu kubwa sana ya ugonjwa huu au *virus* hao kuambukiza ni kwa kujamiiana kwa njia ambayo siyo salama kama ambavyo UKIMWI kwa asilimia kubwa unaambukiza. Tumeona katika kituo cha huduma kule Tunduma, wanawake wamefanyiwa vipimo hivi 2900, kati yao 70 wamekutwa na viashiria vya saratani ya mlango wa uzazi na kati yao 43 wamepeleka kabisa kwa maana ya rufaa kupimwa.

Mheshimiwa Spika, pia pale Mbeya kati ya wagonjwa nane waliopimwa saratani ya mlango wa uzazi ambao ni waathirika na wasio waathirika, sita wamekutwa ni wale waathirika, kabisa wana saratani ya malngo wa uzazi, wawili ndio sio waathirika. Kwa hiyo, unaona jinsi ambavyo hivi vitu vinaoana. Tunashauri Serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, hivi vituo vyetu vinavyohusika na masuala ya *HIV/AIDS*

waongezewe sehemu ya kufanyia upembuzi wa saratani. Najua Serikali inafanya sehemu nyingine, lakini pia huku tunawapata wagonjwa mapema. Hawa wamama wakipatikana mapema, tiba yao ikiwa mapema wanapona kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Tume ya Udhibiti wa Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya. Chombo hiki kimeendelea kutoa elimu ya biashara ya dawa za kulevya kama ambavyo inaonekana katika sheria yake Na. 5 ya Mwaka 2015. Naungana na wenzangu wengi ambao wamesema jamani chombo hiki kitengewe fungu la maendeleo. Kwa nini? Kitengo hiki, mbali ya uraibu, hawa sasa hivi wana changamoto kubwa sana ya kupata magonjwa ya afya ya akili yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, tumeona pale Gereza la Ruanga, Mbeya, wametenga wodi moja kabisa kwa ajili ya wafungwa na mahabusu ambao wamepata magonjwa ya afya ya akili kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, ninasema waongezewe fungu la maendeleo Na. 2 kwa sababu gani? Wanakuwa na wigo mdogo sana kwa ajili ya huduma ya utengamano wa tiba kwa hawa waraibu. Hii inaathiri sana kasi yao ya matibabu. Pia, nasema watengewe kwa sababu kiliniki za urahibu ambazo ziko mpaka sasa hivi ni chache kutokana na fungu dogo kwenye chombo hiki cha kudhibiti UKIMWI, lakini imeonesha matokeo chanya sana. Kwa sababu hawa waraibu wameimarika, wamekuwa na afya bora na pia wanapata huduma ya magonjwa ambatana, kama vile magonjwa ya UKIMWI, magonjwa mbalimbali ya zinaa na TB. Hawa waraibu ambao wana-*attend* kliniki ambazo ni chache, haya matatizo yamepungua miongoni mwao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage. Kabla hujakaa, Mheshimiwa unajua Kiswahili kigumu; waraibu ni watu gani?

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, waraibu ni wale ambao wameathirika na madawa ya kulevya ambao wako kwenye matibabu ya *Methadone*. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Hivi viswahili hivi, vigumu hivi!

Kabla ya Mheshimiwa Mohamed Kigua - Makamu wa Mwenyekiti, nimpe Mheshimiwa Stella Fiyao dakika tano.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, najua wazi kabisa kwamba moja ya majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuwa kiunganishi baina ya Serikali na vyama vya siasa, lakini ajabu ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu haijatekeleza jukumu hili la kuhakikisha inaviunganisha vyama vya siasa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahusiano kati ya Serikali na Vyama vya Siasa, hususan Vyama vya Upinzani yamekuwa na uhasama na uadui mkubwa kwa kipindi chote cha miaka mitano. Ndani ya miaka mitano tumeshuhudia mambo kadhaa yakiendelea kutokea ndani ya Taifa letu...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella, pokea Taarifa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, maneno yanayosemwa na Mheshimiwa Mbunge siyo sahihi. Kama Serikali na Vyama vya Siasa tungekuwa na uhasama mkubwa, usingeshuhudia Vyama vya Siasa vikienda kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vimekuwa vikitoka hadharani na kuthibitisha kwamba kwa kweli, katika kujenga demokrasia na ujenzi wa ustawi wa Watanzania, kazi ya Serikali inaungwa mkono na Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa vimekuwa vikitoka hadharani katika maadhimisho ya shughuli mbalimbali za Kitaifa na kuthibitishia Watanzania kwa umoja wao kama vyama vya siasa vinakubali kwamba Serikali imesimama na inatekeleza majukumu yake sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo, ni mifano michache ya kuonesha kwamba Serikali na vyama vya siasa vimekuwa na mahusiano ya karibu na mmekuwa mkishuhudia katika matukio mbalimbali Serikali iko na vyama vya siasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Stella Fiyao, Taarifa unayopewa ndiyo hiyo. Kwamba ushirikiano upo isipokuwa chama ambacho chenyewe hakitaki tu.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitano tumeshuhudia mambo mengi katika Serikali yakiendelea, ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa kuzuiliwa mikutano ya hadhara, jambo ambalo liko kikatiba na katika Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitano tumeshuhudia viongozi wa vyama vya siasa na wanachama,

hususan wa vyama vya upinzani, wakikamatwa, wakishitakiwa na Serikali na kupewa kesi mbalimbali zikiwemo kesi za uhujumu uchumi, kesi za uchochezi na wakati mwingine kupewa hata *fine* kubwa ambazo haziko kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka mitano...

**SPIKA:** Niliona taarifa, wapi? (Kicheko)

Aah, endelea Mheshimiwa Stella Fiyao. Aah, Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (Kicheko)

## T A A R I F A

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu na nchi nyingi ambazo hazijaendelea, tunaongea sana siasa badala ya uchumi. Hata tukiwa hapa kwetu nchini tunawatoa Watanzania wetu ku-*concentrate* kwenye masuala ya uchumi na kulenga zaidi siasa.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Rais ametoa kauli ambayo ni njema sana kwamba kesi zote ambazo hazina *base* zifutwe. Kwa kauli ya aina hiyo, ni nia ya dhati sana ya kiongozi wa kisiasa kusema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu, kwa sababu tunajadili masuala ya kibajeti na tumetoka kujadili mpango, Waheshimiwa Wabunge, hebu tuchukue mwelekeo huo. Hata viongozi wa kisiasa ambao wako nje ya nchi, warudi tujenge nchi yetu, tujenge uchumi. Hata viongozi wa kisiasa ambao wako hapa wanajadili vitu ambavyo vinawatoa wananchi wetu kwenye umoja, tufuate kauli ya Mheshimiwa Rais ambayo ameonesha nia ya dhati. Tusimtoe kwenye dira hiyo ili tujenge uchumi.

Mheshimiwa Spika, tuna dola 1,080 tu, bado tuna deni la karibu dola 2,090 kufikia dola 3,000 ambayo ni lengo la



uchumi wa kati wa kiwango cha juu ili tuweze kutafuta uchumi wa juu zaidi. Nawasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella, taarifa hiyo unapewa kwamba siasa zote baada ya uchaguzi ni hapa mjengoni. Unapokea?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, tunasubiri utekelezaji wa hicho alichokisema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho pia tumeshuhudia Miswada Miswada ya Sheria za Vyama Vya Siasa ikiletwa ndani ya Bunge. Miswada hiyo ilikuwa na masharti magumu kwa vyama vya siasa ikiwa ni pamoja na kuvidhibiti, lakini mbaya zaidi ni kuingilia chaguzi za ndani za vyama vya siasa. Vyama vya siasa vilipotoa wito kwa Serikali wa kufanya maridhiano ya kujenga umoja wa Kitaifa, Serikali ilinyamaza kimya, mpaka sasa haijasema chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya vyama vingi, tumetengeneza hofu kubwa sana kwa wananchi. Tumezalisha hofu kubwa, hasa kwa wafuasi wa vyama vya upinzani kwani, wafuasi wengi wa vyama upinzani sasa hivi hawana amani kwa kuwa tu wako vyama vya upinzani. Mfano mzuri ni katika Mkoa wa Songwe, Jimbo la Tunduma...

**SPIKA:** Mheshimiwa Fiyao subiri. Mheshimiwa Katambi ulikuwa umesimama, taarifa. (*Kicheko*)

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwa Mzungumzaji kwamba katika Katiba yetu, Ibara ya 107(a) inasema kwamba chombo pekee cha utoaji haki kitakuwa ni Mahakama. Kwa msingi huo, mpaka sasa ninavyozungumza, nimefanya mawasiliano na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, amethibitisha kwamba hakuna *electoral petition* yoyote ambayo imepelekwa kwa maana ya

kwamba wakati wa uchaguzi kama kuna mtu aliumizwa angeweza kutumia *avenue* ya kisheria. Katika hilo nimpe Taarifa pia, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watu wote wana usawa, kwa mujibu wa Ibara ya 13. Usawa huu mbele ya sheria, haiangalii chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa Taarifa ninayompa, katika kipindi chote, hata wakati fulani ambapo tulijaribu kwenda kuzurura hivi, kuna kesi ambazo wakishinda upande mwingine, wataona Mahakama imetenda haki; wakishindwa kesi hiyo, inaonekana kwamba Mahakama haziko huru. Vilevile kwenye uchaguzi, wakishinda uchaguzi kama alivyoshinda pale Nkasi, Tume ilikuwa huru, lakini wakishindwa uchaguzi, Tume haiko huru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jean-Jacques Rousseau na *Montesqueus* walitoa msingi wa *separation of power* kwamba kutakuwa na Bunge, Serikali na Mahakama. Katika hivi, kuna *institutional separation* na *functionale separation* na *personale separation*. Kwa msingi huo, maana yake vyombo hivi vinasimamiana na ndiyo maana leo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko huru, chaguzi zinafanyika kwa uhuru na hakuna kesi yoyote iliyopelekwa Mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilipenda nimpe Mheshimiwa Mbunge taarifa hiyo. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Fiyao shule hiyo umeielewa kidogo?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea. Mfano mzuri ni kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe, Jimbo la Tunduma ambao wanaishi mpakani. Leo hii wananchi asilimia kubwa wanakimbilia nchi jirani ya Zambia kutokana na hofu kubwa kwa kutishiwa na Madiwani ambao wamepita, wako madarakani, wameendelea kuwatisha wananchi wakiwapa kesi za kuwasingizia na zisizokuwa na dhamana. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, hata wakipewa kesi zenye dhamana Watendaji wa Kata na Mitaa wamekataa kutoa barua kwa kusingizia kwamba wanatishiwa na Wakuu wa Wilaya kutoa barua za dhamana.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella dakika zako zimeisha.  
*(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, muda wangu ulikuwa bado.

**SPIKA:** Dakika zako zimeisha. Sasa anaendelea Mheshimiwa Mohamed Kigua. Tulianza na Mwenyekiti wa bajeti, sasa mjadala wetu unamalizwa na Makamu Mwenyekiti wa Bajeti.

Baada ya hapo, Mheshimiwa Olenasha; ni Olenasha eeh? Mheshimiwa Olenasha yupu? Hayupo eeh? Basi baada ya hapo, atafuata Mheshimiwa Katambi katika upande wa Mawaziri. Mheshimiwa Kigua tuhitimishie, dakika tano hizo hizo.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kusema neno kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya bajeti yake.

Pia nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Manaibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache. Katika maendeleo duniani kote, tafiti na maendeleo ni kitu muhimu sana, kwa maana ya *research and development*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama hapa wakizungumzia kwamba, nchi yetu inaelekea kwenye maendeleo na sehemu ambayo Watanzania walio wengi wapo kwenye kilimo. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Wizara ya Kilimo tuwekeze fedha nyingi sana kwenye Sekta ya Kilimo kwa sababu ndio Watanzania wengi wanaitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la amani na migogoro katika nchi yetu limetapaa kila sehemu. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa akisimamia maeneo haya kwa weledi wa hali ya juu sana. Mwaka 2017 Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara kwenye mpaka wa Jimbo letu la Kilindi na Wilaya ya Kiteto. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu alitumia saa nane kwa ajili ya kutatua mgogoro baina ya wilaya hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu umechukua miaka takribani 30 na wananchi wamekuwa hawafanyi shughuli za maendeleo kwa sababu ya migogoro ambayo kwa kweli haiishi. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo, watalaam wakaja wakapitia mpaka ule, kilichobaki ni kuweka alama.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa maeneo haya, mpaka huu ambao unajumuisha Kata nane wananchi hawafanyi shughuli za kilimo, hawafanyi shughuli za maendeleo; na wapo Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, wanashindwa kusimamia kwamba agizo lako la kuweka alama bado halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ana-*wind-up* asiseme neno lolote na atoe maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa; Mkoa wa Tanga na Manyara; na Wakuu wa Wilaya wa Kilindi na Kiteto

wahakikishe kwamba wananchi wanafanya shughuli zao kwa usalama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu umechukua miaka takriban 30 na wananchi wamekuwa hawafanyi shughuli za maendeleo kwa sababu ya migogoro ambayo haiishi. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo wataalam wakaja, wakapitia mpaka ule kilichobaki ni kuweka alama. Wananchi wa maeneo haya katika mpaka huu ambao unajumuisha kata nane, wananchi hawafanyi shughuli za kilimo wala shughuli za maendeleo na wapo Wakuu Wilaya, Wakuu wa Mikoa wanashindwa kusimamia na kwamba agizo lako la kuweka alama bado halijatekelezwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ana *wind-up* aseme neno lolote na atoe maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, Mkoa wa Tanga na Manyara na Wakuu wa Wilaya ya Kilindi na Kiteto wahakikishe kwamba wananchi wanafanya shughuli zao kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie suala la barabara ya kuanzia Handeni - Kibirashi - Kiteto hadi Singida ambapo ndipo bomba la mafuta litokalo Hoima Uganda litakwenda hadi Tanga.

Sasa nafahamu fika na ndio ukweli kwamba barabara hii itakuwa na shughuli nyingi kutokana na ujenzi wa bomba la mafuta, lakini barabara hii haijajengwa kwa kiwango cha lami. Naomba sana eneo au kipande kilichobaki ni cha kilometa 460 tu kuanzia Singida - Manyara hadi Handeni, kuna umuhimu barabara hii ikajengwa kwa haraka sana ili wakati wa ujenzi wa bomba la mafuta wenzetu ambao wameamua ku-*invest* fedha nyingi sana, wasipate usumbufu wakati wa ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Katambi, Naibu Waziri wa Kazi, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Umy Nderiananga, dakika tano pia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini zaidi nami nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania kwa msiba mkubwa uliotufika wa kumpoteza aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Zaidi ya hapo nimpe pole Mheshimiwa Rais, lakini sambamba na hilo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini tena katika nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda, niende moja kwa moja na kujielekeza katika wasilisho la bajeti la Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ofisi yake hasa kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge, lakini pia Kamati zimegusia. Nianze katika eneo moja la ajira, mchango wa ajira au nafasi zinazopatikana katika ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019 kwa maana ya kipindi cha mwaka 2015 - 2020 taarifa na maswali mengi yalikuwa yanaulizwa kuhusiana na ajira milioni nane ni kama hazipo. Sasa niwape taarifa rasmi kwamba, kwa idadi ya ajira zilizopatikana kwa awamu ya kwanza vijana kati ya umri wa miaka 15 hadi 35 ni 11,891,057 ambayo ni sawa na asilimia 52.96.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia upande wa wenye umri zaidi ya miaka 36 kwenda juu ni sawa na 10,560,488 sawa na asilimia 47.4, hii inatokana na ripoti ya taarifa ya mchanganuo wa ajira kwa shughuli na umri ya mwaka 2019 ambapo pia katika upande wa Wizara ya Fedha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wakati huo ambaye sasa ni Mheshimiwa Makamu wa Rais wetu, aliziandikia Wizara zote barua kuweza kutoa taarifa za kuhusiana na ajira. Hizi ndio takwimu kama zinavyojionesha hapo, kwa maana hiyo kwa kipindi hicho chote tulifanikiwa kupata ajira ya zile ambazo zilikuwa zimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa nyingine pia ambayo ni muhimu katika upande wetu maeneo ambayo mengi yameuliziwa zaidi ni kuhusiana na fursa ambazo vijana wetu

wamekuwa wakipewa chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika kipindi hicho tumekuwa tukitoa mafunzo yaani *internship* kwa *graduates* zaidi ya 5,975 walikuwa wanufaika, *program* ya mafunzo ya ufundi stadi zaidi ya wanufaika 28,941 waliweza kupatiwa mafunzo hayo ya kujenga ujuzi na kuongeza stadi za kazi kupitia mafunzo ya uanagenzi. Pia katika *program* ya urasimishaji ujuzi, zaidi ya wanufaika 19,462 nao pia waliweza kunufaika na mpango huo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mafunzo ya kilimo cha kisasa, hapa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilifanikiwa kupeleka vijana 136 nchi ya *Israel*/kujifunza namna ya kuweza kufanya kilimo cha kisasa. Hao tunakwenda kuwatumia pia kama *trainer*, *training* ilikuwa kama *training of trainers* ambao nao pia tutawatengenezea utaratibu wa kuweza kupata ajira kwa maana ya kujajiri na kupewa vifaa au mikopo ili waweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mafunzo ya *greenhouse* nchini kote kati ya mikoa ambayo ilinufaika, mikoa 12 zaidi ya Watanzania vijana 8,980 nao waliweza kupatiwa mafunzo hayo. *Program* hizi ni endelevu ikiwa sambamba na Mfuko wa Kukuza Ujuzi (*skills development*) zaidi ya wanufaika 1,550 wamepata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa pili kwa kujali zaidi muda nijielekeze katika eneo hili la fursa ambazo zilipatikana za moja kwa moja. Fursa za moja kwa moja za ajira zilipatikana kwa mujibu wa taarifa iliyotoka Wizara ya Fedha, baada ya kuwasiliana na Wizara zote, ni zaidi ya 11,891,772 ikiwa ni ulinganifu wa fursa za ajira zisizo za moja kwa moja 881,354...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi. Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wenye Ulemavu, una dakika tano pia. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI WA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha leo hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Vile vile niwatakie mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan Waislam wote duniani na katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuniamini ili niwatumikie Watanzania katika nafasi hii ya Naibu Waziri, Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuamini katika uwezo wangu na kuweza kunibakiza ili niweze kutumikia watu wenye ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwakuwa sisi ni watu wenye ulemavu, napenda niendeleo kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwateua wenzangu wenye ulemavu kuwa Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu na katika maeneo mengine. Tunamhakikishia tutaendelea kuchapa kazi kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kujibu maswali ambayo yaliulizwa, mojawapo likiwa ni suala la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu na kutatua migogoro yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumetambua vyama 14 vya watu wenye ulemavu wa aina tofauti na tunaendelea kufanya nao kazi kwa karibu kuhakikisha kwamba migogoro haipo.



Mheshimiwa Spika, vile vile tumefanya chaguzi na tumevisimamia vyama hivi viweze kuiendesha vizuri. Hali kadhalika nimefanya ziara katika mikoa takribani tisa ambapo nimefanya vikao vya kujengeana uwezo na viongozi wa vyama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo pia swali liliulizwa na Kamati kuhusu Mfuko. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa maelekezo ya kuhusu Mfuko, tutaleta pia maelekezo ya ziada hapo ambapo tutakuwa tumepata utathmini utakaoturuhusu sasa kuzindua Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu na tutawakaribisha pia wadau waweze kuchangia katika Mfuko huu ili tuweze kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la *register* ya watu wenye ulemavu na ni eneo ambalo tuliona ni la muhimu sana, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa haraka sana tumefanya utambuzi wa watoto wenye ulemavu ambao mpaka sasa tumefanya utambuzi wa watoto 28,698 wenye ulemavu, ambao wengi wao walikuwa wamefichwa ndani na sasa wametolewa na tutahakikisha wanasoma kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuwepo kwa mwongozo wa utambuzi wa watu wenye ulemavu ambao ni *register* maalum sasa kwa wale ambao wana umri mkubwa wa ujana na kuendelea, tumeshatoa maelekezo kupitia TAMISEMI tarehe 8 Aprili, 2021 wameshateremshiwa viongozi ili wayafanyie kazi. Nitoe rai waendeleo kukusanya takwimu hizo na nitakuwa nafuatilia kwa ukaribu sana katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile suala la asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu; baada ya kufanya tathmini ya kina na kuzunguka katika Mikoa hii niliyoitaja, ya Simiyu, Mara, Dar es Salaam, Kilimajaro na kadhalika. Tumepata maoni ya watu wenye ulemavu na tukaona kwa haraka sana sisi ndani ya Serikali tubadilisha pia kanuni. Hivyo, tumebadilisha kanuni na kwa sasa watu wenye ulemavu zile asilimia mbili zao wataweza kupata kwa mtu mmoja mmoja na wakitaka

kikundi mwisho ni watu wawili, wakitaka zaidi sawa, lakini kikubwa sisi tunatii kiu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili tutaendelea kujipima kuona namna ambavyo fedha hizi zinakuwa na ufanisi. Mimi binafsi nitoe rai watu wenye ulemavu wapewe fedha ambazo zinaweza kuwaletea matokeo badala ya kupewa fedha kidogo kidogo, wasaidiwe kupata miradi ambayo ni mizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la ajira, mwezi Januari na Februari tuliajiri Walimu 243 wenye ulemavu. Vilevile upande wa *Internship* tumeingiza Walimu 100. Niseme kwamba, tutaendelea kusimamia upande wa Serikali ajira zote zinazotoka, kipaumbele kiwe ni kwa watu wenye ulemavu na tutawaingiza kwa wingi na kwa kadri ambavyo ajira hizo zitatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa taasisi binafsi na mashirika kuendelea kuajiri na kuwaamini watu wenye ulemavu kama sisi ambavyo tumeaminiwa hapa na tunafanya kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu hususan kwenye eneo la elimu, liliulizwa swali hili. Napenda niseme kwamba, Serikali tunaweka mkazo sana katika kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata elimu. Kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 tumeshanunua vifaa saidizi 51,339 na tumevigawa katika shule za msingi na sekondari na tutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni suala hili la unyanyapaa na ubaguzi. Tutaendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara kuhakikisha hakuna mtu anayewanyanyapaa na kuwatumikisha watu wenye ulemavu kama tukio lililotokea Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Makofi hayo hayatoshi Waheshimiwa. Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, hasa eneo la wenye Ulemavu. Mheshimiwa Ummy kwa siku zijazo nakuruhusu ukichagua kuongea umekaa, ukisimama *its your option*, ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, utakuwa na dakika 15, karibu sana hapa mbele, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama pia atakuwa na robo saa, halafu Mheshimiwa Waziri Mkuu utakuwa na saa moja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia siku hii ya leo. Kikubwa zaidi ningependa sana kuwashukuru viongozi wetu wa kitaifa, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, lakini pia na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isidor Mpango na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia na Baraza la Mawaziri lote kwa kuendeleza majukumu ambayo tumekuwa nayo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nisingependa kutoka hivi hivi bila kuzungumza tatizo ambalo limetupata kitaifa, kutoa pole kwako lakini pia na familia ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, lakini pia na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na kipenzi chetu, jemedari, kiongozi mwenye maono na hatimaye kumfikisha kwenye nyumba yake ya milele kule Chato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa sana kutoa shukrani zangu kwa kamati mbili za Utawala na Serikali za Mitaa, kwa maoni yao ambayo yalikuwa ni mapana, *very extensive*. Tunashukuru sana na yale maoni tumeyachukua yote na tuwahakikishe kwamba tunakwenda kuyafanyia kazi, kuhusiana na namna ambavyo tutakuza uwekezaji kwenye nchi yetu. Pia Kamati ya Katiba na Sheria ambayo pia imetoa maoni mengi, lakini kipekee Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wameweza kutoa maoni mengi, kwa sababu

tunafahamu suala la uwekezaji ni suala pana suala kubwa na ndio linajenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi hoja kubwa ilikuwa ni kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Pia kuwa na mtazamo chanya kuhusu masuala ya uwekezaji kwenye nchi yetu na kwa kutambua kwamba kila taasisi isijiangalie peke yake, lazima itambue kwamba tuna sababu nyingi za kuvutia uwekezaji kwenye nchi yetu. Eneo la kwanza ni ajira kwa vijana wetu, tunafahamu kwamba Ilani ya CCM ya Uchaguzi lakini pia kwenye Mpango wetu wa Maendeleo tumepanga kutengeneza fursa za ajira zaidi ya milioni nane.

Mheshimiwa Spika, pia tunataka ukuaji wa uchumi wetu ambao ni mkusanyiko wa shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zinafanywa na sekta binafsi lakini na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ziweze kufikia angalau asilimia nane kwa kila mwaka. Tafsiri yake ni kwamba uzalishaji wote wa mwaka huu ukitoa uzalishaji wa mwaka jana ukigawanya kwa uzalishaji wa mwaka jana ukizidisha mara 100 basi ikupe asilimia nane ndio tafsiri yake, lakini pia tunafahamu kwamba tumeingia kwenye uchumi wa kati kabla muda wetu ambao tuliupanga mwaka 2025 na hili ni moja ya mafanikio makubwa sana ambayo sijui kwa nini hayazungumzwi kwa uzito.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kufanikiwa kuingia kwenye uchumi wa kati mapema zaidi kwa sababu ya juhudi kubwa tulizoziweka kwenye maeneo mbalimbali ya uzalishaji ikiwemo kuvutia uwekezaji. Tafsiri yake labda tuweze kuiweka vizuri tu, kuna kitu tunaita *GNI* ambayo ni *GDP* unaiweka kwenye *market prices* ambayo unapata *gross national income*, ukigawanya kwa idadi ya watu ndio unapata *per capital income* ambayo sasa ile ndio imetufikisha pale kwenye 1,080 ambayo ni kiwango cha mwanzo cha kuingilia ngazi ya uchumi wa kati.

Kwa hiyo hata baadhi ya michango tulikuwa tunaisikia hapa tumeingia kwenye uchumi wa kati lakini kule vijijini hatuoni, tafsiri yake sio hiyo.

Mheshimiwa Spika, kule vijijini kimsingi tunaona kwamba badala mtu kutembea kilometa tano kufuata zahanati, basi anatembea kilometa moja au mita 500 kwa sababu zahanati imejengwa kwenye kituo chake cha makazi. Pia huduma nyinginezo za usafiri ambazo zamani ulikuwa uamke saa 10 uweze kupata gari, lakini sasa hivi gari unasimama tu popote unaweza kupata. Vile vile miundombinu yetu imeboreshwa sana. Sasa hivi kila familia ina angalau pikipiki na gari, vitu ambavyo zamani tulikuwa tunasema ni *luxury* sasa hivi tumevichukua kama ni *necessity* na ndio maana mahitaji ya maendeleo yetu yanakuwa yanaongezeka kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kweli tumepiga hatua kubwa. Haya yote yametokana na uamuzi wa Serikali kuweza kufungua fursa za uwekezaji kwenye nchi yetu, kuruhusu *private sector* lakini pia kuruhusu Serikali yenyewe kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nijielekeze kwenye maeneo ya uwekezaji hususan yake ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge hapa.

Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, kwamba mikakati na mipango ambayo iliwekwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akiwa na msaidizi wake wakati huo, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan walifanya wote, nalichukulia ni kama vile uendeshaji wa ndege, ndege zina *Pilot* na *co-pilot*, tuna bahati kwamba sasa hivi aliyekuwa *co-pilot* wakati ule ambaye alishiriki kwenye program za *manifesto* kuangalia *manifesto* ya ndege, kutengeneza *mission plan* ya kwamba turuke twende *destination* gani, tupitie *route* ipi, hali ya hewa ikoje, walipanga wote wawili, ndio maana kuna mwendelezo na pia tumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusema kwamba kazi iendee sio ianze upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale wote wanaojaribu kuutoa ushauri wa hapa na pale kuhusiana na nini akifanye, natamani sana wampe nafasi, afanye kazi yake kwa sababu anaifahamu, alikuwepo kwenye kupanga mipango na yeye ni sehemu ya mipango hii ambayo tunaitekeleza kwa sasa. Ushauri mwingi ambao unatolewa, ningependa sana kuwashukuru lakini tumuache Mheshimiwa Rais, anafahamu wapi ataifikisha nchi yetu kwa sababu tunayo Dira ya Maendeleo ya Taifa, tunayo Ilani ya CCM, tunao Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano awamu ya tatu, ile awamu ya pili yeye mwenyewe alishikiri, lakini hii Ilani ya CCM yeye alishiriki kuipitisha kama Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, lakini pia kama msimamizi wa shughuli za Serikali pia akiwa kama ni Makamu wa Rais, kwa hiyo anafahamu wapi anataka kuipeleka nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie mageuzi makubwa ambayo yamefanywa kwenye nchi yetu kwa upande wa uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuunda Wizara ya Uwekezaji, walifanya wote hayati Dkt. John Pombe Magufuli akiwa na Mama Samia Suluhu Hassan kama Makamu wake. Pia na kitendo cha yeye si tu kuamua kuibakiza Wizara ya Uwekezaji, lakini kuipa hata Katibu Mkuu na iwe Wizara Kamili, ni uthibitisho tosha kwamba amedhamiria kukuza mazingira ya uwekezaji nchini, lakini pia kuhakikisha kwamba tunakuza shughuli mbalimbali za uwekezaji kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji, Sera yetu hii ni ya siku nyingi, ni ya mwaka 1996, kwa hiyo kwa kiasi kikubwa ni kama inahitaji maboresho, inahitaji kuhuishwa ili mambo mapya na changamoto ambazo tumezipata kwenye utekelezaji wa sera ile ya zamani tuweze kuyaingiza kwenye sera mpya na ituongoze vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia kuna sheria yenyewe ya uwekezaji, baada ya kupitisha Sera ya Uwekezaji mwaka 1996, mwaka 1997 Bunge lako Tukufu likapitisha Sheria Na. 38 ili iweze kutuongoza sasa katika utekelezaji wa ile sera kwa upande wa sheria. Hiyo tunafanya mapitio na tumefikia hatua ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, nafikiri muda siyo mrefu Bunge lako Tukufu litapata nafasi ya kuipitia hiyo sheria ya uwekezaji na ikiwezekana tupate hiyo sheria mpya ya uwekezaji ambayo itabeba mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza. Kwasababu wakati mwingine tulikuwa tunakwazwa na sheria yenyewe huwezi kufanya zaidi ya pale.

Mheshimiwa Spika, pia kuna eneo la maboresho kutokana na taarifa ambazo zinatolewa na *International Finance Cooperation (IFC)* ambayo ni sehemu ya *World Bank Group* hii Benki ya Dunia ambayo inatupima sisi Tanzania na nchi zingine 192 duniani namna gani mazingira yetu ni wezeshi kwa upande ufanyaji wa biashara ile *easy of doing business* ambako tumekuwa *rent* kwenye *numbers* ambazo siyo nzuri sana ambazo sisi tungetamani tubadilike kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tangu mwaka 2010 baada ya sisi kuingizwa kwenye huo mpango Serikali imekuwa ikifanya mapitio kupitia mpango wa maboresho ili kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yanaainishwa ambayo ni maeneo 11 kuanzia unaposajili kampuni *BRELA* mpaka unapofunga kampuni *BRELA*, na hapa katikati kuna vigezo vingi namna ya kupata umeme kupata mikopo na ulipaji wa kodi na mazingira kama hayo kwa hiyo, vigezo vyote vinaangaliwa lakini pia na *blue print*.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka mwezi Mei 2019 Baraza la Mawaziri lilipitisha *blue print* ni maarufu kama *blue print* lakini ni mpango wa maboresho ya mazingira ya ufanyaji biashara kwenye nchi yetu na hii ni mpango wetu sisi *is a home grown program* ni ya kwetu sisi hakuna Benki ya Dunia, hakuna *IMF* waliyotuletea ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo Mama Samia Suluhu Hassan kama Makamu wa Rais wa wakati huo naye alikuwa ni sehemu ya huo mpango walipitisha na kuhakikisha kwamba tunaitekeleza ipasavyo na nikuhakikishie sana na Bunge lako Tukufu kwamba tunaenda kuisimamia hilo na tuhakikishe kwamba tunaitekeleza ipasavyo na kujenga mazingira wezeshi kwa upande wa biashara.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mabadiliko ya sera na sheria mbalimbali za kifedha na kikodi Bunge lako tukufu limekuwa likipitisha hapa *finance act* kuangalia maeneo yale ambayo yametajwa kodi tozo mbalimbali ambazo zinachajiwa na taasisi na halmashauri zetu za wilaya au Serikali za Mitaa ili tuhakikishe kwamba tunajenga mazingira wezeshi kwa upande wa maeneo ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pia yako maboresho ya utendaji wa kituo chetu cha uwekezaji kuna mambo mengi ambayo yamefanyika ingawa majukumu yake ya kisheria yanatakiwa yatimizwe kulingana na sheria inavyotaka. Pale kwenye kituo cha uwekezaji tumetengeneza *well stop facilitation center* ambako watumishi wa taasisi mbalimbali sasa hivi wako taasisi 14 pale kuna watumishi kama 25 ambao wanakaa pale kuna watumishi wa *TRA*, kuna watumishi wa *BRELA*, watumishi wa Uhamiaji, kuna watumishi wa Idara ya Kazi. Lakini pia watumishi wa *NEMC*, watumishi wa *OSHA* wa *NIDA* wako pale wanatimiza majukumu ya taasisi zao katika kufanikisha uwekezaji lakini wakitokea ndani ya kituo cha uwekezaji na hii yote ilikuwa ni katika kujenga mazingira wezeshi na kutoa usumbufu kwa upande wa uwekezaji kuzunguka kwenye hizo na kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyokuwepo ni kwamba kuimarisha na kuhakikisha kwamba tunakuwa na watumishi ambao wanamaamuzi pale ndani ya taasisi hilo tunaenda kulifanya na tunataka hii sheria yetu ikipita mpya tuhakikishe kwamba wanaokaa pale ni watu wenye maamuzi siyo tena watumishi ambao wanatakiwa kila mara kupiga simu kwenye taasisi zao kuandika *email* au kupeleka mafaili kwa hiyo itachelewesha kwenye biashara zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mfumo tuliuweka wa *National Investment Facilitation Committee* ambao wakuu wa taasisi zote ambazo kwa namna moja au nyingine huduma zao zinagusa wawekezaji wanakutana chini ya uwenyekiti wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji na kupitia changamoto mbalimbali na naomba nikuhakikishie kupitia *Forum* hii changamoto 53 zilitatuliwa na



mojawapo ilikuwa ni kiwango cha utozaji wa ada wa *NEMC* pale ambapo mtu anataka au mwekezaji anataka kupata cheti cha *NEMC* anatakiwa alipie zamani ilikuwa ni asilimia ya mtaji lakini baadaye kupitia kikao hiki tukaja kubaini hapana huwezi kufanya asilimia ya mtaji tafsiri yake mtu kama anawekeza bilioni 100 basi ana 0.03 ya bilioni 100 ni hela nyingi sana kwa hiyo kupitishie *EIA* ripoti yake apate *certificate*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukakubaliana kwamba watengeneze *regulation* upya na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa wakati huo akaisaini wakatengeneza *band* ya maeneo kama 14 ambayo yanasema tu kwamba kuanzia mtaji 0 mpaka labda milioni 5 basi utalipia shilingi 50,000 tu. Kwa hiyo, katika milioni 5 mpaka labda milioni 20 utalipia labda 100,000 tu. Tulipata mafanikio sana kupitia huu mfumo na tutaendelea kuboresha ikiwemo mfumo unaotumika kwaajili ya vibali vya kazi ni mfumo ambao umetengenezwa pale *TIC* kwaajili ya kufanikisha hii na ni imani yetu kwamba tutaendelea kutengeneza mifumo mingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ilikuwa ni uanzishaji na uendelezaji wa *land bank* au akiba ya ardhi ya uwekezaji. Uwekezaji wote unafanywa kwenye ardhi changamoto kubwa imekuwa ni kupata ardhi kwa wakati. Lakini pia na mchakato wa uhulishaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna maeneo mawili moja watu binafsi na Serikali kuhakikisha kwamba ikiwemo Tawala za Mikoa na Halmashauri zetu kupima maeneo ya ardhi na kuhakikisha kwamba ile ardhi tunaileta kwenye kituo cha uwekezaji ili tuweze kuinadi kwa wawekezaji uweze kupata urahisi wa kuipata urahisi wa kuipata ile lakini gharama zote za ulipaji na nini atalipa huyo mwekezaji kikubwa Zaidi ni kwamba asipate muda mrefu wa kuipata hiyo ardhi.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine tuna *National Land Allocation Committee* ambayo inaratibiwa na Wizara ya Ardhi ambayo imekuwa ikigawa hii ardhi kulingana na mahitaji kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu kuondoa urasimu na kufanikisha uwekezaji. Hili Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amezungumza kwa kauli nzito angetamani na angependa tuondoe urasimu kwenye maeneo yetu tutambue wajibu wetu kama watendaji kama watumishi na sisi kama Wizara ya Uwekezaji lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu, tutaenda kufanya, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo msimamizi wa shughuli za Serikali tutaendelea kusisitiza hili tuwajibike kwa kujua kwamba tutaisaidia nchi yetu kwenye kufikia kwenye malengo yale yaliyoainishwa kwenye dira ya maendeleo ya miaka 25 lakini pia na mipango yetu ya maendeleo ya miaka mitano mitano ambayo sasa hivi tuko kwenye mwaka wa tatu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kutambua kwamba tuna ajira kwa vijana lazima tutengeneze ajira kwa vijana lakini pia kuna kutengeneza soko la haraka la wakulima wetu. Kwahiyu tukifanikisha uwekezaji maana yake tunasababisha wakulima hawa wapate soko la haraka kwasababu kutakuwa na wanunuzi hapa ndani. Lakini pia tunahitaji fedha za kigeni ili uchumi wetu uwe imara.

Mheshimiwa Spika, *reserve* ya fedha za kigeni ni muhimu sana ili iweze kushikilia thamani ya shilingi la sivyo tutakuwa tukihitaji kulipia huko nje kama ni madeni ama au ni uagizaji wa vitu ni lazima tutoe fedha nyingi za Kitanzania tupate dola moja na kufanya sasa ile *exchange rate* kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuwa na pesa ambayo iko tayari kuweza kulipia hizo *external obligations* kwa hiyo kuna haja sana ya kuvutia uwekezaji tupate fedha za kigeni lakini pia tuweze ku-*export* hivi vitu vyetu lakini pia kuna masoko ya kikanda na kimataifa ambayo tumesainiwa iko *EAC, SADC and International, AGOA* ambayo tumesaini kwa hiyo, naomba sana niwahakikishie Bunge lako tukufu kwamba tunaenda kuweka juhudi kubwa sisi kama...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):**

Mheshimiwa Spika, napenda sana kukushukuru napenda kuunga hoja mkono ahsante sana (*makofi*).

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Geoffrey Idelphonse Mwambe Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu karibu sana Mheshimiwa una dakika 15

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru sana nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kuliongoza Bunge letu vizuri tunakupongeza sana na hasa kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika. Lakini tunampongeza pia Naibu Spika wako kwa kazi nzuri mnayoifanya tunawaomba kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi ya pekee kabisa kumpongeza Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kupata kibali mbele ya Mwenyezi Mungu kuliongoza Taifa letu la Tanzania hatuna mashaka naye na sisi wengine ambao tumefanya naye kazi tunajua udhibiti na umahiri wa uongozi wa Mama Samia kwahiyu tunamtakia kila la kheri na tutamuunga mkono sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kitu kimoja kipekee kabisa sifa ya ziada aliyonayo Mama Samia toka tumepata uhuru katika Taifa letu hatujawahi kupata Rais mwanamke kwahiyu ana sifa ya ziada na sifa hiyo hata kama kuna mtu mwingine yoyote angetamani hawezi kupata sifa ya kuwa mwanamke na kuongoza sasa Taifa letu. Kwa hiyo sisi tunaamini kabisa atatuvusha vizuri lakini kwa kweli niungane na watanzania wote kupeana pole kwa msiba mzito wa Hayati Dkt John Pombe Magufuli Rais wetu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, nitaendelea kumkumbuka nina heshimu uteuzi wake alionipatia katika kipindi cha miaka mitano lakini kwa moyo wa shukrani sana ninamshukuru mama yetu Samia Rais wetu kwa kuendelea

kuniamini na kuniacha nimsaidie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Wizara hii namuahidi utumishi uliotukuta na nitatekeleza majukumu yangu sawasawa. *(Makofi)*

Kwa kweli nitakuwa sijajitendea haki kama sitompongeza kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kuaminiwa kuwa kwenye nafasi hiyo. Lakini vilevile ninamshukuru sana mimi najua ni kwa kiasi gani Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa ni mwalimu wangu kwenye kazi hii ambayo ninaifanya chini ya Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana na ninakuombea dua kwa Mwenyezi Mungu na ninaomba niwaambie watanzania na Waheshimiwa Wabunge hakika ndugu yetu Kassim Majaliwa Majaliwa ana kitu cha ziada katika moyo wake ana kitu cha ziada katika utumishi wake na ninaamini Mwenyezi Mungu alitupatia Waziri Mkuu huyu kwa makusudi maalum. Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakushukuru sana, nakushukuru na ninaomba nikuhakikishie nitaendelea kuwa msaidizi wako nikizingatia miongozo na taratibu zote ambazo umekuwa ukitupatia katika kukusaidia ili haya mambo yote unayoyasimamia yafanikiwe ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze Makamu wa Rais ana sifa na vigezo vyote tulivisema ndani ya Bunge sitaki kuvirudia. Lakini kwa namna ya pekee niwashukuru watendaji wote Ofisi ya Waziri Mkuu Makatibu Wakuu, Manaibu na Makatibu Wakuu ambao tulifanya nao kazi kwa bajeti hii tunayoimaliza kwa sasa ninawashukuru sana. Lakini kwa namna ya pekee nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kweli kwa kuamua kunitewa kugombea nafasi ya Ubunge kwenye Jimbo la Peramiho naishukuru Kamati Kuu, iliyoongozwa na Hayati Dkt John Pombe Magufuli lakini nashukuru Sekretarieti iliyoongozwa na Dkt Bashiru, lakini nashukuru pia Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi ilinithibitisha lakini nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Peramiho kazi inaendelea ahsanteni sana kwa kunirudisha tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Kamati zote tatu ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu tunafanya nao kazi kamati ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa ndugu yangu Omary Mchengerwa ambaye sasa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora walifanyakazi kubwa sana ya kutushauri katika kipindi hiki chote akisaidiwa na Makamu wake ndugu yangu Najma na Wajumbe wote wa kamati. Lakini kwa kweli Kamati ya Bajeti Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti tulipitisha fungu la Bunge kwa kweli tunawashukuru sana na Kamati ya masuala ya Ukimwi na Dawa za Kulevya ninawashukuru sana kwa miongozo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wabunge kazi ya kushughulikia masuala ya Bunge si ndogo unakutana na Wabunge wenzako kila siku lakini kwa kweli ninawashukuru sana ninawaahidi utumishi wa unyenyekevu ushirikiano katika kila siku ili kuweza kuyatekeleza majukumu haya sawasawa. Nawashukuru Manaibu Mawaziri ambao nafanya nao kazi.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi ambayo tunatakiwa kuyajibu kwenye mkutano wako huu wa leo lakini naomba tu niseme kwamba tumepokea hoja za Wabunge zote na tutajitahidi kuzijibu kwa maandishi na kila hoja zote tutaziwasilisha kwenu Wabunge wote kwa maandishi ili angalau muweze kuona tumeweza kufanya nini katika kipindi hiki chote ambacho tumetekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa moja kabla sijaingia katika mambo mengine naungana mkono na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi lakini vilevile na Waziri mwenzangu wa masuala ya Uwekezaji na hasa kuitikia wito wa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira bora ya uwekezaji nchini na kuondoa vikwazo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa ambacho kiko katika Ofisi yetu ni mfumo huu wa kuratibu vibali vya ajira za wageni. Kwahiyo jambo hili sisi tumelichukulia kwa uzito mkubwa kwanza tunafikiri ni lazima tufanye mabadiliko ya

sheria. Sheria ya uwekezaji na sheria ya vibali vya ajira za wageni ziweze kusomana vizuri, na Wabunge mmetushauri vizuri sana hapa tuone je sheria hizi mbili kwa mazingira tuliyonayo sasa kweli ni sheria Rafiki? Zinaweza kutusaidia kweli kuruhusu uwekezaji ninaomba nilihakikishie Bunge lako kwamba kazi hiyo tumeshaianza na tunataka tuwe na mfumo mzuri wa kuharakisha vibali vya ajira za wageni bila kuzuia ajira za watanzania wenyewe. Kwahiyo jambo hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili tumefikiri tuwe na mfumo kwasababu utoaji wa vibali huu umeambatana na mazingira ya rushwa sana kwahiyo tumeshatengeneza mfumo shirikishi ambao utajumuisha watu wa Uhamiaji, wenzetu wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye tunasimamia vibali hivyo vya ajira za wageni tutakuwa tunasoma vile vibali *on line* kila kibali kwahiyo hakuna tena *temptation* ya rushwa na tutauzindua mfumo huo haraka sana iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine tumesema kwamba tunazungumza tatizo la ajira katika Taifa letu lakini ni lazima tujue tunahitaji nini ili watanzania na hasa vijana waajiriwe. Tumeamua kufanya tafiti kubwa mbili ambazo tumeanza kuzifanya, utafiti wa kwanza tunataka kufanya utafiti wa hali ya nguvu kazi tuliyonayo nchini je inaendana na mahitaji tuliyonayo sasa? Na kazi hiyo tumeanza kuifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mmeona kama wenzetu TAMISEMI wanabadilisha tahsusi (*combinations*) ambazo zinatakiwa zianze kusomwa na vijana wetu. Lakini ni lazima tunapobadilisha hizo *combination* ama tahsusi ziendane na mahitaji ya ujuzi kwa sasa ndani ya Taifa letu kusudi watoto wa Kitanzania kama ana *opt* kusoma kitu fulani kiendane na mahitaji ambayo yanahitajika ya ujuzi kwenye Taifa letu. Kwahiyo tunafanya hizo tafiti ili tuende sambamba lakini tumekubaliana na Waziri wa Elimu pia na yeye tutafanya naye tafiti zetu tutakwenda kukaa nao kusudi tujue tuwafundishe nini vijana wa Tanzania elimu ambayo inatakiwa iweze kutumika ndani ya Taifa hili. Kwa hiyo, Ofisi

ya Waziri Mkuu tumejipanga tunadhani ni wakati muafaka wa hayo kuyafanya kwa sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini Wabunge hapa wameomba sana ile fedha tunayopewa kwaajili ya *skills development* iongezeke wamegundua kwamba imepungua. Nakubaliana nao kwamba tunatakiwa kuiongeza ila sisi tumepata *challenge* katika utoaji wa mafunzo hayo ya ujuzi. Tumefanyakazi nzuri sana na wajumbe wamesema Wabunge wamesema na ripoti ya kamati imeeleza eneo hili limeweza kufanyiwaje kazi vizuri lakini tumeanza kujitafiti na sisi hivi ni kweli mafunzo ya ujuzi tunayoyatoa sasa kila siku tunasema watu wafundishe *masonry* sijui wafundishwe ushonaji, sijui wafundishwe mambo hayo ambayo ni *skills* ambazo zimezoeleka kila siku.

Mheshimiwa Spika, lakini tunajua sasa hivi mageuzi makubwa ya uchumi yanakwenda kwenye *green economic*, *blue economic* na *TEHAMA*. Kwa hiyo, kuna haja ya mafunzo haya tutakayoanza kuyatoa kwa bajeti ya kuanzia mwezi wa saba tunafikiri sasa yaende huko kwenye *green economic*, kwenye *blue economic* na kwenye *TEHAMA*. Tukifanya hivyo tunaweza tukasaidia sana Taifa letu na sisi likapiga hatua kwa haraka. Kwahiyo tunadhani ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo tutaliwekea mkazo sana ni eneo la *local content* tuna mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania kama tukijipanga vizuri kwenye *local content* watanzania watafaidika sana kwenye mradi huu wa bomba la mafuta. Lakini vile vile lhata hii miradi mingine ya kimkakati tunadhani sasa ni kipindi ambacho ni lazima tusimame imara kwenye dhana ya *local content* watanzania wengi waweze kufaidika na miradi hii ya kimkakati. Kwahiyo nadhani haya yote yatatusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo labda nikilisema kwa haraka ni hili la sekta ya hifadhi ya jamii, kwanza naomba tu nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu

thamani ya mifuko yote ukijumuisha mifuko yote *Worker's Compensation, NHIF, NSSF* na *PSSSF* mpaka sasa thamani ya mifuko hii imeishafika trilioni 11.510 kwa hiyo, thamani imeendelea kuongezeka. Lakini ninachotaka kusema hapa ni nini. Historia ya sekta ya Hifadhi ya Jamii toka tulipopata uhuru imekuwa ikibadilika kulingana na wakati na hali halisi ya mazingira. Hata tunachokifanya sasa ni muendelezo wa mabadiliko hayo hayo ya sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetuagiza mambo ya kufanya lakini baada tu ya Uhuru unaona mwaka 1964 Serikali ilianzisha Mifumo ya Hifadhi ya Jamii kwa mfano NPF ilianzishwa mwaka huo, lakini mwaka 1999 ilianzishwa NSSF, mwaka 2006 -2012 tulibadilisha mfumo wa LAPF na mfumo wa GPF, ka hiyo mwaka 2018 tumefanya mageuzi mengine makubwa.

Mheshimiwa Spika, Lengo la mageuzi haya ni kufanya sekta iwe *sustainable*, kwa hiyo, hata sheria hizi tulivyobadilisha na ku-*merge* hii mifuko lengo letu ni kufanya mifuko hii iwe endelevu na iwe imara iweze kutusaidia. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge baada ya kumaliza *actuarial* tukishapata *actuarial* ripoti ya PSSSF, tukapata *actuarial* ripoti ya NSSF ninawahakikishia Serikali itakuwa imejipanga kumaliza matatizo ya mifuko hii na hasa mfuko wa PSSSF ambao sasa tunataka kuupa kikokotoo kitakachoweza kuwa *sustainable* kwa faida ya wanachama lakini na uhimilivu wa mfuko na uendelevu wa mfuko. Kwa hiyo, sisi tunapokea mawazo yenu yote lakini tukipata *actuarial* ripoti itatusaidia sana kufanya maamuzi endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi kweli ambayo kidogo ilikuwa inasuasua, naomba niwahakikishie kwamba tumejipanga kuhakikisha miradi hiyo haiendelei kuleta hasara. Serikali ya Awamu ya Tano iliikuta miradi hiyo imeanza kutekelezwa, ilichokifanya ni kufanya maamuzi magumu ya kufanya miradi hiyo isiwe ni hasara lakini iendelee na kujenga faida kwa wanachama na kwa mfuko kwa ujumla.



Mheshimiwa Spika, tunayo miradi mingi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu yeye mwenyewe yuko mstari wa mbele kuratibu miradi yote ambayo iko ndani ya Ofisi yetu. Mmeona tumeratibu kuhamishia Serikali Dodoma, watumishi takribani elfu kumi na nane wameshahamia hapa. Pia mmeona ameratibu mazao ya kimkakati kahawa, chikichi, chai, vyote ameviratibu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie kuna miradi mingine mikubwa miwili sasa hivi tunaendelea kuiratibu. Mradi wa kutengeneza mnyororo wa thamani kutosheleza mahitaji ya mbegu nchini ambayo utatolewa taarifa na Wizara ya Kilimo unaratibiwa na Ofisi yetu na mradi wa uvuvi ambao unakwenda kununua meli nne za uvuvi Tanzania Bara na meli nne za uvuvi Tanzania Visiwani ambao nao utaratibiwa na Ofisi yetu. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri na tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaratibu suala la lishe kuhakikisha tunaondoa utapiamlo nchini. Hapa naomba nimpongeze sana Mbunge mwenzetu Neema Lugangila, kwa kweli huyu ni Balozi wa Lishe. Nampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya. Vilevile, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza ile Kamati ya Wabunge ya Masuala ya Lishe na yenyewe imetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda vizuri kwenye suala zima la lishe bora Tanzania. Kama Ofisi ya Waziri Mkuu tunaliratibu hilo lakini bado kuna mikoa inafanya vizuri kwenye uzalishaji wa chakula lakini kiwango cha utapiamlo na udumavu kipo juu. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa hali bado siyo nzuri, kiwango cha kitaifa ni asilimia 40 lakini Iringa wamefika asilimia 47.1 na Songwe pia wamefika asilimia 43.3. Kwa hiyo, ni lazima tuende na mikakati ya pamoja ili kuhakikisha kwamba tunasaidia mikoa hiyo waweze kufanya vizuri kwenye suala la lishe ili kuondoa udumavu. Tukijipanga vizuri kwenye elimu na kila kitu tusipoondoa udumavu tutakuwa na watoto ambao bado hawafanyi vizuri katika masomo yao darasani. Kwa hiyo, hilo nalo tunaliratibu na tunakwenda nalo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeratibu masuala ya uchaguzi na tutatoa maelezo vizuri kwenye taarifa yetu na majibu ya hoja tutakayoyatoa. Uratibu wa uchaguzi uliofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu umepelekea Serikali kuwa madarakani na sisi Wabunge kuwa humu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya vizuri kuratibu tatizo la dawa za kulevya nchini. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu mpaka sasa asilimia 90 ya dawa za kulevya zilizokuwa zinaingia kutoka nje ya Tanzania sasa hazilingii tena na tutaendelea kusimama vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna mambo mengi ya kujibu lakini basi itoshe kwa haya machache ambayo nimeyasema. Nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja asilimia mia moja na tutaleta majibu kwa maandishi ili kuweza kutosheleza kiu ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama. Tunawashukuruni sana timu nzima kwa kutengeneza mapito ili sasa mtoa hoja ambaye ni Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aweze kuja kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana kwenye Kikao hiki cha Kumi na Moja cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili kwa ajili ya kuhitimisha mjadala kuhusu Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe, Mheshimiwa Naibu Spika kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa mwenendo mzima wa majadiliano ya Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa

mwaka 2021/2022. Nazipongeza na kuzishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri na michango yenye tija kwenye Hoja ya Waziri Mkuu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa sekta ambao pia wamekuwa hapa wakisikiliza hoja hizi mbalimbali na Naibu Mawaziri lakini pia kupitia vipindi vya maswali na majibu wamekuwa wakijibu maswali na hoja kadhaa wamekuwa wakizipitia na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali. Kadhalika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu wa pamoja na ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha mjadala wa bajeti hii yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenu ambayo ni muhimu katika kuisaidia Serikali kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nawasilisha Hoja siku ya tarehe 13 nilianza maelezo ya utangulizi mazuri ambayo sitaraji kuyarudia tena yaliyogusa maeneo mengi. Sasa tunaendelea na hoja ile ile ya kufafanua hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wote hapa wakati wa mjadala wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mjadala wa Hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2021/2022 umeenda vizuri sana na umethibitisha uimara na umakini wa Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba kwa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu. Serikali, imepokea maoni na ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na wakati wote tutauzingatia katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala hapa tulikuwa na Wabunge waliochangia 121 kati yao Waheshimiwa 109 walipata nafasi ya kusema moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 12 walichangia kwa njia ya maandishi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba uridhie nisiwataje na kwamba majina yao yaingizwe moja kwa moja kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mjadala huu, Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wameendelea kujibu hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Kutokana na ufinyu wa muda hoja zitakazosalia zitajibiwa kwa maandishi. Vilevile, Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kuwasilisha hoja zao kwenye sekta zao watatoa ufafanuzi wa yale yote yaliyogusa sekta zao. Walikuwa hapa wame-*take note* yale yote wanayopaswa kujibu na bajeti yao itakapokuja mbele ya Bunge lako Tukufu kila mmoja atalazimika kufafanua yale yote yanayogusa sekta yake.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano kuhusu Hoja ya Waziri Mkuu yako masuala mengi na muhimu yameibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, wakati wote wa Hoja ya Waziri Mkuu tumekuwa na mjadala wa kina na wenye msisitizo wa kiwango cha juu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kujenga hoja zenye ubora na umakini unaliostahili unaofanya Serikali kuweza kuzingatia kwa umakini kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, nikiri kuwa hoja nyingi zilizoibuliwa zina uhusiano wa moja kwa moja na utendaji kazi wa Serikali. Aidha, masuala muhimu hususan vibali vya kazi kwa wageni na uwekezaji kwa kiasi kikubwa yamekuwa kitovu cha mjadala na michango ya Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia hii Hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Hii ni kwa sababu eneo la Uwekezaji ndiyo ambalo sasa tunaitegemea kukuza uchumi wa nchi hasa kwenye sekta

mbalimbali ikiwemo kilimo, madini, maliasili, maji na sekta nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, naomba uridhie japo kwa uchache nitoe ufafanuzi kuhusu baadhi ya masuala yaliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye Hoja ya Waziri Mkuu hususan eneo la uwekezaji na vibali vya kazi pamoja na kwamba Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi wameeleza maelezo ya awali.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 6 Aprili 2021, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wakati akiwaapisha Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa baadhi ya Taasisi za Serikali aliweka msisitizo masuala mbalimbali ikiwemo uwekezaji na vibali vya kazi ikiwa ni maeneo ambayo yamekuwa na changamoto nyingi katika utowaji wa vibali hasa kwenye uwekezaji. Mheshimiwa Rais alielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuimarisha Huduma za Pamoja (*One Stop Centre*), kushughulikia malalamiko yote kuhusu kodi, kuondoa vikwazo katika uwekezaji, kuhamasisha uwekezaji kupitia mazungumzo, ushawishi, kudhibiti rushwa na kuondoa urasimu kwenye maeneo yote ya uwekezaji ikiwemo na maombi ya vibali vya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais yenye kujali maslahi mapana ya nchi hii yalikuwenda sambamba na uamuzi wake wa tarehe 31 Machi 2021 wa kuunda rasmi Wizara ya Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kuwa Wizara hiyo inasimamia kikamilifu masuala ya uwekezaji hapa nchini, kikanda na kimataifa. Majukumu mengine ni kuratibu majadiliano ya uwekezaji wa miradi ya kimkakati, mikutano ya majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ndani na nje ya nchi lakini pia kubuni na kutekeleza mikakati ya kujenga sekta binafsi ya hapa Tanzania iliyo imara na yenye ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuona ushindani huu unaanza kukuwa na utatuletea manufaa makubwa. hatua

hiyo, itawezesha kuvutia wawekezaji wengi kutoka nje ya nchi kuja hapa nchini lakini pia hata Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza nao sasa wanapata fursa ya wazi ya kuanza kuwekeza mitaji yao teknolojia na ujuzi ili kuongeza ukuaji wa uchumi kwa kasi na upatikanaji wa ajira na maendeleo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uamuzi wa kurejesha jukumu la uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ni ishara ya wazi kuhusu imani kubwa aliyonayo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Nami napenda kumhakikishia kuwa sitamuangusha, nitasimamia sekta hii ili iweze kuleta mafanikio hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tayari hatua mbalimbali za utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais zimeanza kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na moja kuandaa Muundo wa Wizara ambao utaainisha majukumu na mgawanyo wa Idara na Taasisi zitakazokuwa chini ya eneo hilo la uwekezaji. Mbili, kupitia upya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ili kubainisha maeneo yenye kuhitaji maboresho ambapo tayari tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 imekamilika. Tatu, tunaandaa sasa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji ili kuimarisha uratibu, usimamizi, uhamasishaji na ufuatiliaji wa masuala ya uwekezaji katika sekta zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa hatua hizo kutaiwezesha Serikali kutekeleza masuala muhimu kama yafuatayo. Moja, ni kushiriki kikamilifu katika mikutano na majadiliano ya Jumuiya za Kikanda yanayohusu masuala ya uwekezaji ikiwemo maandalizi ya Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, utungaji wa Sera za Uwekezaji kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Itifaki ya Uwekezaji ya Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Mbili, ni kujenga mazingira rafiki ya uwekezaji

na uchumi shindani nchini kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kusisitiza kwa kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha mazingira hayo wezeshi. Tunataka biashara ishamiri na yeyote anayekuja kuwekeza nchini apate fursa hiyo ya kuwekeza kwenye sekta yoyote ile ambayo tunayo. Tuna uhakika atapata huduma zilizo sahihi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wawekezaji kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Nchi alivyokuja kueleza hapa mbele yetu. Nne, kutatua changamoto za wafanyabiashara kupitia Baraza la Taifa la Biashara ambalo sasa tunaliunda kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na Taifa ambako Mheshimiwa Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo la Biashara la Taifa lenye malengo ya kuratibu majadiliano ya sekta za umma na sekta binafsi. Eneo hili tutalisimamia ili sekta binafsi nayo ipate nafasi ya kuishauri Serikali kwa ajili ya utekelezaji au uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, tano, kutoa elimu na hamasa kuhusu huduma zitolewazo kwenye Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja (*One Stop Facilitation Centre*), fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta mbalimbali nazo pia ziweze kuibuliwa na kuelimisha wananchi namna ya kupata wabia na kushirikia nao katika kuanzisha na kuendeleza miradi yao kupitia Taasisi yetu ya Uwekezaji Tanzania (*TIC*). Sita, tunataka tuimarisha mifumo ya usajili wa miradi na kutoa Cheti cha Vivutio (*Certificate of Incentives*), kuunganisha mifumo inayotumika *TIC* na makao makuu ya Taasisi na kuboresha mfumo wa kuchakata rufaa za vibali vya kazi na ukaazi kwa njia ya mtandao ambapo kila mmoja atakuwa anaweza kuufika popote alipo ndani au nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii tena kuwakumbusha watendaji wenzangu wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kuhakikisha kuwa muundo na mifumo ya masuala ya uwekezaji inakamilika ndani ya muda ulioelekezwa na Mheshimiwa Rais. Natoa maelekezo kwa Wizara na taasisi zote zinazohudumia wawekezaji kuhakikisha

wanawezesha uwekezaji katika maeneo yao kwa kutoa huduma stahiki na taarifa muhimu kwa wakati zipatikane lakini pia kuondoa usumbufu ukiwa unaambatana na maombi ya rushwa lakini na urasimu kama nilivyoeleza awali, hili nalo tutalisimamia.

Mheshimiwa Spika, aidha, nasisitiza kuwa watendaji wajjepushe na haya ambayo nimeyaeleza ya uombaji wa rushwa na urasimu usiokuwa wa lazima katika kuhudumia wawekezaji ili kujenga imani baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ili tuweze kuzungumza lugha moja. Mwaka ujao wa fedha 2021/2022, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji ikiwemo kuainisha ardhi ya uwekezaji (*land bank*) na kuendeleza miundombinu muhimu ya uwekezaji katika mikoa yote ili kuvutia uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limeibua mjadala mkubwa wakati uchangiaji wa hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu ni vibali vyenyewe vya kazi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi hapa ameeleza lakini changamoto kubwa iliyozungumziwa ni kuhusu kubanwa na masharti mbalimbali dhidi ya ajira za wageni ikiwemo la kwanza ukomo wa mwombaji kuishi nchini kwa muda usiozidi miaka mitano. Huu nao umekuwa kikwazo pale anapowekeza mradi mkubwa unaohitaji kuusimamia zaidi ya miaka 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mahitaji ya elimu, uzoefu au ujuzi wake wa mwombaji ili aweze kupewa kibali. Hapa pia kuna mgogoro mkubwa. Tunadai mtu awe na *degree* lakini pia *degree* hiyo aweze kuifanyia kazi kwenye sekta hiyo. Kwa hiyo, tutaangalia zaidi uzoefu na ujuzi alionao, elimu itakuwa ni kitu ambacho kinasaidia ujuzi na uzoefu alionao katika kufanya kazi. Hili nalo tutaliangalia ili kurahisisha kupata watu ambao wanaweza kufanya kazi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tatu kigezo cha mwombaji kupata uthibitisho wa cheti chake kutoka *NECTA*. Mtu kasoma Norway tunataka alete cheti ili aweze kuajiriwa hapa nchini kwa kupeleka cheti hicho *NECTA*, *NACTE* au *TCU*. Nalo hili



tutaliangalia tena vizuri kwa sababu limekuwa likikwaza kupata wawekezaji wanapokuja kuwekeza hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo ndiyo yenye mgogoro zaidi katika suala la utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni. Hivyo basi, Serikali inafanyia kazi changamoto hizo kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, tayari nimetoa maelekezo kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kushirikiana na Wizara zote za kisekta pamoja na watendaji wa Wizara zote za kisekta katika kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinafanyiwa kazi kwa haraka zaidi ili kuweza kuuweka uwekezaji katika sura inayotuletea watu wengi zaidi na kujenga imani ya uwekezaji hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mbali ya uwekezaji, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Mwaka 2020, naomba nitumie nafasi hii pia kuendelea kufafanua hoja nyingine ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wote wa mjadala kama ifuatavyo. Tulikuwa na hoja ya kuitaka Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba utekelezaji wa vipaumbele ulenge zaidi katika kuwatengenezea wananchi wa kawaida fursa za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inalo jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutekeleza vipaumbele vya Sera na miongozo mbalimbali ya Serikali ili kumletea maendeleo mwananchi kulingana na fursa zilizopo katika maeneo husika miongoni mwa maeneo ya kimkakati ya utekelezaji wa jukumu hilo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni kuwajengea wananchi uwezo kwa kutambua fursa zinazowazunguka na kuzitumia kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Kwa mfano, utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali, uanagenzi, urasimishaji ujuzi, kurahisisha upatikanaji mitaji na taarifa za masoko, ni miongoni mwa mkakati wa Serikali kuwafanya Watanzania wajue fursa zinazowazunguka

Mheshimiwa Spika, pili, kuratibu ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya kiuchumi ili kuwawezesha Watanzania kunufaika na fursa zilizopo katika maeneo yao, mathalani ujenzi wa njia za usafirishaji kama vile njia ya anga, njia za maji, barabara, pia ujenzi wa madaraja makubwa, masoko, vituo vya mabasi, miundombinu ya umwagiliaji kwenye Sekta ya Kilimo, usambazaji wa umeme na pia kuimarisha mawasiliano ndani ya nchi. Haya yote ni yale ambayo tunayasimamia.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuratibu na kufuatilia ushiriki wa Watanzania katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati kupitia mpango wa *local content*. Lengo ni kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika na utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na uwekezaji mkubwa ulifanywa na Serikali kwenye maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano wa miradi hiyo ni ujenzi wa reli ambao sasa unaendelea ambayo ni *SGR*, ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere ambao pia unaendelea, bomba la kusafirisha mafuta litakaloanza hivi karibuni linalotoka Uganda mpaka hapa Tanzania, kuna suala la uchimbaji wa madini hususan uchimbaji mdogo mdogo nao tumeimarisha, ujenzi wa barabara za vijijini na barabara kuu pamoja na madaraja makubwa ambayo pia yanaunganisha eneo moja na eneo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja ya Wizara ya Fedha inayotaka ihakikishe inatoa fedha kwa wakati ili kuwawezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuteleza majukumu yake ya kusimamia changuzi ndogo zinazoendelea kujitokeza kwa mujibu wa sheria. Haya yote yanaendelea kutekelezwa na tunazingatia sana sheria, Kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (Sura 343) na Kifungu kidogo cha (120) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa (Sura 292).

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatekeleza hili kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba chaguzi hizi zinaendelea kufanyika kama ambavyo zinaendelea. Kwa

sasa tunayo maeneo mawili ya yanayoendesha uchaguzi mdogo kule Buhigwe pamoja na Kibondo ambapo pia uratibu wake umeshanza kuratibiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu iwe na mfumo mzuri utakaohakikisha Makao Makuu ya Nchi Dodoma yanaendelezwa. Hili nataka nilileleze vizuri kwa kuwaondolea mashaka au wasiwasi Watanzania wakifikiri kwamba mkakati wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma kuwa sasa hautaweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mfumo mzuri sana wa kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Nchi yanaendelezwa kwa kujenga na kuendelea na mipango ya maendeleo ya Jiji la Dodoma. Mfumo huo unahusisha kikosi kazi cha Taifa cha kuratibu Mpango wa Serikali kuhamia hapa Dodoma ambacho kinajumuisha Wajumbe kutoka Wizara na Taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo hii watumishi wote wapo hapa Dodoma, shughuli zote za Serikali zinafanywa hapa Dodoma na ujenzi wa miundombinu mbalimbali unaendelea hapa Dodoma. Natumia nafasi hii kuwakaribisha wawekezaji, wale wote ambao wanaotamani kufanya kazi hapa Dodoma, waje. Nataka niendeleo kurudia kusema kwamba Makao Makuu ya Dodoma bado itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki kikozi kazi kina jukumu la kushauri namna moja ya kupanga na kuendeleza Mji wetu wa Dodoma na utekelezaji huo unahusisha zaidi miradi mbalimbali ikiwemo na kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa miradi ya maji, tupate maji ya kutosha, tunajenga kiwanja cha ndege kikubwa zaidi ya hiki tulichonacho, barabara na utoaji wa huduma za jamii nao unaimarishwa na kujenga kituo cha reli kikubwa kuliko vituo vyote nchini kitajengwa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Watanzania wote kuwa Dodoma inaendelea vizuri na wale wote wanaotamani

kuja, waje, fursa zipo na njia za usafiri zote zipo za barabara na anga.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine inasema Serikali iendelee miradi yote ya awamu zilizopita ambayo inaendelea kutekelezwa na utekelezaji wake uweze kusimamiwa. Serikali tumeahidi kutekeleza ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni ya Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani ya CCM ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya kipaumbele iliyoainishwa kwenye Ilani ambayo imeanza kutekelezwa na ile ambayo bado haijatekelezwa, yote itatekelezwa ili kuhakikisha kwamba tunafikia malengo ya Chama cha Mapinduzi kupitia Serikali yake kwa kutelekeza na kusimamia miradi yote hii ya kimkakati.tuna Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao umeweka kipaumbele cha kuendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hilo halina matatizo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ipo mbele yetu na imejadiliwa sana ni ile ya Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuboresha utaratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwepo na mfumo mmoja wa vyanzo vya fedha. Hatua hiyo iweze kuandamana na kuongeza usimamizi wa udhibiti wa marejesho ya fedha hizo za mikopo ambazo zinatolewa na hiyo mifuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyofafanua katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2021/2022 Serikali itathimini kwa kina utendaji na ufanisi wa mifuko yote ya uwezeshaji kwa wananchi kiuchumi ikiwemo Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana ili kuona kuwa kuna umuhimu wa kufuta baadhi ya mifuko kuunganisha au kuanzisha mifuko mipya kwa kuzingatia mahitaji ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati wote mchakato huu ukiendelea, taratibu za kuratibu marejesho ya fedha za

mikopo hiyo zitakuwa zinaendelea kuratibiwa ili fedha hizi zinazokopeshwa ziweze kurudi halafu ziwe endelevu kuwakopesha vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilikuwa imezungumzwa kwenye mijadala hapa, ni mfuko wa uwezeshaji wa vijana wa Halmashauri kwamba uongezewe fedha kutoka 4% mpaka asilimia 10. Kama nilivyotangulia kueleza, Serikali inafanyia tathmini mifuko yote ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kutaka kujua kiwango cha mikopo chenyewe kinachotolewa ikilinganishwa na mahitaji, riba za mikopo yenyewe na ufanisi wa mifuko hiyo katika kukuza uchumi wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hiyo, taarifa rasmi itatolewa na maombi haya yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na ushauri wao tutauzingatia kulingana na uwezo wa mfuko wenyewe kadiri tunavyoendesha ndani ya Serikali. Mfuko huu wa Halmashauri kwa sasa unaendelea kutoa 4% ya vijana, asilimia 4% kwa wanawake na 2% kwa wenye mahitaji maalum au walemavu.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo muhimu yaliyojadiliwa kama hoja ikiwemo uboreshaji wa huduma za maji, elimu, lakini pia suala *TARURA* limezungumzwa sana, Sekta ya Mafuta nayo imejadiliwa sana, uimarishaji wa bandari umeungumzwa na suala la madini hasa kule Mererani imepata nafasi kubwa ya kuzungumzwa. Masuala haya yote yataratibiwa vizuri sana kupitia Wizara husika kama ambavyo nimeeleza na watafika mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa ufafanuzi wa kila hoja ambayo pia imeweza kuchangiwa hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hoja za Muungano zimejadiliwa sana, nazo pia zitapata ufafanuzi kupitia bajeti ya hotuba ya Makamu wa Rais. Hoja ya mfumo kununua mazao (*TMX*) imezungumzwa pia na Wizara ya Kilimo itazingatia hili, kwa sababu mkakati wetu sasa ni kukuza ushirika.

Mheshimiwa Spika, ushirika ni wana ushirika, tutaendelea kuwapa nafasi wanaushirika kusimamia ushirika ili tuufanye ushirika huu uweze kuwa endelevu. Mifumo mingine yote itabuniwa na kuanzishwa na Wizara yenyewe ya Kilimo inayosimamia ushirika ambayo pia inajua mwenendo wa uanzishaji wa ushirika mwenendo wa uanzishaji wa mifumo mingine inayotakiwa kusimamiwa hapo. *TMX* kwa sasa ni ya Wizara ya Fedha na tunaisihi Wizara ya Fedha ijiimarisha na mfumo huu, itutafutie masoko ya nje zaidi kwa mazao yaliyoko hapa ndani ili tuweze kuyauza na wanunuzi kutoka nje huko waweze kununua kwa mfumo huo wa *TMX*.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mahusiano ya Vyama vya Siasa au Chama Kimoja na Serikali, imefafanuliwa vizuri na Waziri wa Nchi. Jambo hili litaangaliwa na linaendelea kuangaliwa, lakini mahusiano yetu bado ni mazuri kwa sababu tunashirikiana kwa pamojo, licha ya kuwa kuna kasoro mbalimbali ambazo pia nazo huwa zinapata ufumbuzi kupitia Baraza la Vyama vya Siasa ambapo pia huwa tunakaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni migogoro ya ardhi na mipaka ya utawala kwenye maeneo mbalimbali nchini. Tuna migogoro kati ya vijiji na vijiji, migogoro kati ya Wilaya na Wilaya, hata Mkoa na Mkoa, ukiwemo ule mgogoro wa Wilaya ya Kiteto na Kilindi ambao pia tulishautafutia ufumbuzi. Nilitoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya, nitoe wito tena kwa Wakuu wa Mikoa ya Manyara na Tanga; na Wilaya za Kiteto na Kilindi, wamalize huo mgogoro kabla sjarudi tena huko ili ufumbuzi upatikane na wananchi waweze kufanya mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa nahitimisha, nimesikiliza na kufuatilia kwa umakini sana mjadala huu kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 mpaka 2025 itatatekelezwa vyema chini ya Jemedari wetu,

Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Saluhu Hassan.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakati wote tunakuwa katika Vikao vya Bunge, tutakuwa tunaendelea kushauriana na pia kuona namna nzuri ya kutekeleza maeneo haya kupitia ushauri wenu na namna ambavyo mnaweza kuisimamia Serikali yetu kupitia Kamati zetu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanayo imani kubwa sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kufuatia mafanikio makubwa yaliyopatikana na mwanzo mzuri aliouonyesha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, imani hiyo ya wananchi haina budi kuwa chachu kwetu katika kuwatumikia kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine mwelekeo wetu ni mzuri, suala la msingi lililo mbele yetu ni kuongeza umakini na kasi ili malengo yote tuliyojiwekea ambayo dhamira yake ni kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla yaweze kufikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 7 Aprili, mwaka huu 2021 tuliadhimisha kumbukumbu ya miaka 47 ya kifo cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na tarehe 12 Aprili mwaka huu, 2021 tuliadhimisha kumbukumbu ya miaka 37 ya kifo cha Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunaendelea kuwakumbuka viongozi hawa kwa mchango wao mkubwa katika kutetea wanyonge na kudumisha misingi ya Imani, mshikamano na umoja wa Kitaifa ambao tunao. Ntoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, turejee kauli ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa wakati huu tuendeleo kushikamana, kusimama na kuwa wamoja katika Taifa, kuonyesha upendo wa undugu, kudumisha amani yetu,

kuenzi utu wetu, uzalendo wetu, Utanzania wetu na kutazama mbele kwa matumaini na kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu siyo wakati wa kuonyesheana vidole, bali ni wakati wa kushikana mikono na kusonga mbele. Kwa msingi huo, tuendeleo kudumisha na kuilinda amani ya nchi yetu ikiwa ni sehemu ya kuenzi jitihada za waasisi wa Taifa hili. Tutumie muda mwingi kwa kazi zaidi na kujipatia kipato na kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja kulliko vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nawakumbusha Waheshimiwa Mawaziri, Viongozi na Watendaji wote waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi, mnalo jukumu kubwa sana kuwahudumia wananchi na kuhakikisha mnasimamia ipasavyo miradi iliyoanzishwa kwenye maeneo yenu na kushughulikia changamoto zote katika maeneo yenu na pia kusikiliza kero za wananchi kwenye maeneo yenu.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanayoendana na thamani ya fedha za walipa kodi. Ndiyo namna bora ya kurudisha shukrani kwa wananchi waliotupa ridhaa ya kuwatumikia.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kusisitiza kuwa tukiwa watumishi wa Umma, tunao wajibu wa kuwapokea, kuwasiliza na kuwahudumia wananchi waliotupa dhamana hii ya uongozi. Kwa hiyo, tufanye kazi, tena kwa bidii zaidi, tuache mazoea ya kiurasimu ili kazi iendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutumia nafasi hii kuwatakiwa Waislamu wote nchini mfungo mwema na wenye mafanikio wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulioanza katikati ya wiki hii. Natoa rai kwamba tutumie kipindi hiki kumwomba Mwenyezi Mungu aendeleo kuibariki nchi yetu, aendeleo kuwalinda viongozi wetu na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, tumwombe Mwenyezi Mungu awajaalie wote kwa hekima na busara ili tuendeleo



kuliongoza Taifa letu kwa haki kujenga umoja na mshikamano kudumisha amani katika nchi yetu pamoja na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nihitimishe kwa kutoa tena shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, timu yote ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge, Watanzania kwa ujumla, ndugu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, napenda mtambue kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu muda wote ipo wazi, iko tayari, kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia. Tunaendelea kushirikiana na kila mmoja kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa naliomba sasa Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili tuweze kuchapa kazi, taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge letu Tukufu kama nilivyowasilisha katika hoja yangu ya tarehe 13 mwezi huu wa Nne 2021 ili tuchape kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwa)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Ahsante sana kwa kweli Mheshimiwa Mkuu kwa kutukaribisha wewe pamoja na Waheshimiwa Mawaziri katika ofisi yako na Manaibu Waziri, maana tumezungumza hapa siku nne, mambo ni mengi, lakini mmejitaahidi, hoja nyingi mmezipitia tena vizuri na nyingine mmetuahidi kwamba mtatuletea katika utaratibu wa maandishi baadaye. Tunawashukuru sana.

Nami nachukua nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote, kukushukuru na kukutia moyo sana Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo umekuwa ukifanya. Pamoja na kazi zake ambazo ni *specific* Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini ofisi hii ni ya uratibu wa shughuli za Serikali nzima. Kwa kawaida, kufanya kazi ya uratibu ni ngumu sana, lakini mmeifanya vizuri, tunawapongeza. (*Makofi*)

Nasi Bunge mnatupa kila aina ya ushikirikiano, tunasema ahsante sana. Kwa sababu shughuli zetu hapa Bungeni bila Ofisi ya Waziri Mkuu haziweze kwenda. Maana ndiyo *link* yetu kwa Serikali. Kwa pamoja, ndiyo maana mnaona hata shughuli za Bunge zinaweza kwenda. Pia tunakushukuru kwa kutuomba bajeti ya Bunge. Maana bajeti yetu ipo kwenye maombi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ndiyo maana tuna Waziri katika Baraza la Mawaziri ambaye yuko Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini ni Mbunge ambaye ni Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tunasema ahsante sana kwa kazi kubwa ambayo umekuwa ukiifanya. (*Makofi*)

Sasa hoja hii ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuungwa mkono, tutaiamua tutakaporudi saa kumi ambapo tutakuwa na nafasi ya kupitia fungu kwa fungu na baadaye tutamaliza utaratibu kufuatana na kanuni zetu zinavyotaka. Maana kwa muda uliobaki hatuwezi kufika popote tukisema tuyaanze yale mafungu kwa sababu ni mengi kidogo. Kwa hiyo, nitawaomba saa kumi turudi na tutajitahidi tumalize mapema kadri tutakavyoweza, ni vizuri turudi. Hata wale wenye swaumu kidogo, ni vizuri ukirudi, maana hapa kuna kiyoyazi kidogo na nini, saa zinakwenda kidogo haraka. (*Kicheko*)

Pamoja na shukrani hizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, tunalo tatizo katika nchi yetu kwa ujumla wake tu la uaminifu. Sasa sijui hili tulifanyaje? Wawekezaji wengi wamekuwa wakilalamikia uaminifu wa vijana hasa wa Kitanzania. Ukishawekwa mradi, basi vijana uaminifu unakuwa mdogo katika sekta hii na hii, mtu atajikuta amefilisika tu asipoangalia. Yaani eneo hili sijui dawa yake nini?

Waheshimiwa Wabunge, basi mtakapokuwa mnachangia ni moja ya eneo la kulitazama. Kiwango cha uaminifu ni kikubwa kiasi gani? Nadhani hili linahitaji *consulted effort* ya viongozi wetu wa dini na madhehebu mbalimbali kuongeza kuhubiri kuhusiana na uaminifu; mashuleni kupitia mitaala yao na wazazi naomba tujenge jamii ambayo ni ya waaminifu, wasiokuwa na tamaa. Nafikiri naeleweka.

Mtu akianzisha labda tuseme *Super Market*, nisikilizie kama utamkuta bado yuko barabarani miaka mitatu ijayo. Ataibiwa pale si kawaida. Yaani hata wewe wekeza, halafu njoo Bungeni hapa, umewaachia miezi sita hujawatembelea na nini, subiri siku utakayoenda upige mahesabu. Utakuta umepigwa. Ndiyo uaminifu ninaozungumza huo, nafikiri naeleweka. Ni kwamba humwachii shughuli mkakubaliana kwamba iende hivi halafu usipigwe, ni kwa sababa ya uaminifu. Sasa hili eneo linahitaji sijui namna gani tulifanyie kazi, lakini naona ni kama eneo ambalo linahitaji sana kufanyiwa kazi. Kiwango cha uaminifu wetu ni kidogo sana. *(Makoff)*

Wakati tunasoma zamani hizo, nilikuwa kwenye nchi fulani, sasa nikashangaa kwenye *library* ya *University* ile hakuna *Librarian* na viko vitabu vizuri, mambo mazuri mle kwenye *library* kubwa ya kisasa. Sasa tukawa tunashangaa, jamani hapa vipi? Basi wengine miongoni wanafunzi kutoka Afrika ikawa ni kuchukua tu vitabu. Inatakiwa mwenyewe uandikishe mahali kwamba nimechukua kitabu fulani, halafu siku ya kurudisha, unaandika tena na unarudisha kwenye *shelf* lake na kadhalika. Sasa akichukuwa vitabu saba au nane, mtu anaandikisha viwili, hivi vitano wala hajaandikisha. Ni kiwango cha uaminifu.

Baadaye tukaja kugundua siku ya mwisho mzigo wa vitabu hivyo utawekwa kwenye begi gani? Hizo kilo haziwezekani kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, siku ya mwisho ile, vitabu vinawekwa kwenye meza ambavyo havikuwa kwenye rekodi ya kuchukuliwa kabla. Sasa tukawa tunacheka huko nje kwamba jamani, mnaona tunavyoumbuka Waswahili kwamba siyo waaminifu? *(Kicheko)*

Ipo mifano ya mingi ya kiwango cha uaminifu ambacho wenzetu wanacho na ambavyo sisi huku ni kidogo. Kijana akiwa na fursa kama hiyo akaachiwa asimamia biashara asikuibie, wenzake mtaani watasema mjinga sana yule. Alipewa goli liko wazi, kaliacha! Mh, mjinga kweli! Jamaa mwaka mzima yuko Bungeni kule wala hasimamii, yeye kakaa tu! Unaona sasa! Yaani hiyo! *(Makofi)*

Uaminifu unalipa sana katika maisha. Ukiaminiwa katika kidogo, anayekuamini anaweza akakuamini katika kikubwa zaidi na akakuamini katika kikubwa zaidi na zaidi, nawe ukawa ni sehemu ya mafanikio makubwa zaidi, lakini sisi kidogo kile kile, pale pale, hawafanyi makosa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili tutendelea kushauriana, ni mojawapo ambalo na mie nimeona nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuona ni namna gani tunaweza tuka-*instill* uaminifu miongoni wa vijana wetu wa Taifa letu.

Basi kwa vile tutakutana saa kumi kwa ajili ya kupitia mafungu ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambamo na mafungu yetu yamo, basi nitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na Kikao chetu cha mchana cha Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Kumi na Moja.

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kwa wale ambao mnakwenda na *tablets*, kwenye sanduku linalohusika vimeandikwa vitabu vya mpango na bajeti. Mkitafuta pale ndiyo mnaweza mkaona kinachoendelea; vitabu vya mpango na bajeti.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, Mheshimiwa Cecilia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ambavyo umetuelekeza hapo, ukifungua kwenye *tablets* zetu hizo *Votes* hazina viwango vya fedha kwa pembeni, imeainishwa *votes, sub votes* lakini hakuna fedha ambazo zinaombwa kwa pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Wakati wataalam wetu wanaangalia, tuendeleo kidogo, tuanze na lile la masuala ya sera ambalo lina mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuendeleo, Katibu.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*.....Sh. 4,953,194,000/=

**MWENYEKITI:** Majina tayari ninayo ya wale ambao wanataka ufafanuzi wa masuala ya kiseru kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika eneo zima la Sera ya Uwekezaji katika tasnia ya michezo na sanaa, kumekuwa na ukiritimba mkubwa sana kiasi kwamba tunashindwa kuchochea uwekezaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mifano; katika upande wa sanaa, mwanamuziki *Diamond Platinumz* alikuwa ameshaleta wawekezaji mara kadhaa kwa ajili ya kujenga *arena* kubwa ya muziki lakini mambo haya hayatokei. Pia ukija kwenye upande wa michezo, hasa mpira wa miguu, kwenye Klabu ya Simba sasa ni takribani mwaka wa tatu, mamlaka za Serikali zimekuwa hazioneshi ari ya kutaka uwekezaji ufanyike na kuifanya michezo ichangie katika pato la Taifa. Naibu

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha kwamba tasnia ya michezo na sanaa inajengewa uwezo wa kiuwekezaji ili kukuza mnyororo wa ajira na kukuza uwekezaji hapa nchini. Kama majibu yatakuwa hayaridhishi, nakusudia kushika shilingi kutoka kwenye mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kushukuru kwa maswali ya Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo. Kuhusiana na masuala ya Sera ya Uwekezaji, sera hii iko wazi, inaruhusu uwekezaji kwenye sekta zote. Hata Kituo chetu cha Uwekezaji kinaruhusiwa kusajili miradi ya uwekezaji ya sekta zote, lakini pia na kutoa vivutio kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya chaguo la mwekezaji mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka sera wezeshi na kama tulivyosema, kama kutakuwa na changamoto, basi mapitio ya sera ambayo yanafanywa sasa hivi tutaweza kujumuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mifano miwili aliyoitoa; sina kumbukumbu binafsi kuhusiana na mradi ambao ndugu yetu Naseeb Abdul (*Diamond*) alikuwa amepanga kuweza kuutekeleza. Bahati nzuri kabla ya majukumu haya niliyokuwa nayo nilikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji na sikumbuki kama Naseeb Abdul aliwahi kuja Kituo cha Uwekezaji kuomba kusajili mradi wake na Serikali tumsaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu kwa kuwa sasa mimi ndio msimamizi wa hiyo sekta kisera, pale ambapo Mheshimiwa Naseeb Abdul atakuwa na dhamira hiyo, basi tutamsaidia ipasavyo kwa sababu ni nia ya Serikali kujenga fursa mbalimbali kama nilivyozungumza ili vijana wetu waweze kupata ajira, kipato na tuvutie teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la uwekezaji katika Klabu ya Simba, sheria ambayo inafuatwa hapa ni Sheria ya BMT (Baraza la Michezo Tanzania) ambayo imetoa maelekezo ya namna ya vilabu kuanzisha makampuni na kuvutia wawekezaji kwenye hizo kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachotokea kwenye upande wa Klabu ya Simba ni kwamba klabu hiyo ilifanya mabadiliko ya mfumo wake wa uendeshaji na mwaka 2018 ikawa na Katiba mpya ambayo ilionesha kwamba kutaundwa na kampuni na wakatoa hisa asilimia 49 kwa mwekezaji na asilimia 51 zikabaki ndani ya Simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika ni kwamba kulikuwa na makampuni manne na mtu binafsi mmoja ambao walitengenezwa kuweza kutengeneza huo mchakato. Sasa Tume ya Ushindani ambayo kisheria inatakiwa ipewe taarifa kuhusiana na muunganiko wa hayo makampuni kutengeneza kitu kimoja ambacho kipo kwenye mchakato, Tume ya Ushindani walitakiwa wapewe hiyo taarifa na walipopewa taarifa wakaja kubaini kwamba ule mchakato kwenye kuanzisha na kuunganisha yale makampuni haukufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri walifungua kesi na kuwaambia Simba watoe maelezo. Bahati nzuri sana baada ya kukaa awamu ya kwanza wakakubaliana kwamba badala ya kuwa kesi, basi ili kufanikisha ibadilike iwe ni *settlement*, sasa sijui kwa Kiswahili tunaitaje, maridhiano, kwamba hawakutimiza baadhi ya vipengele, basi kuwe na maridhiano tu ambayo Simba wenyewe walipewa nafasi kuwasilisha namna ambayo unaweza kurekebisha ule mchakato ili kuendelea kutimiza matakwa ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi ninavyozungumza mchakato upo na hivi karibuni, nafikiri kesho au wiki ijayo, watakutana mara ya tatu waweze kukaa na kupitia upya maeneo yale ambayo ambayo wamekubaliana kuweza kufanya mchakato. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwamba Serikali iko kwenye kuwezesha michakato hiyo na Klabu yoyote ambayo inataka kufanya hivyo, Serikali itaunga mkono ili tuweze kuwezesha vilabu vyetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, unaridhika na maelezo hayo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kabisa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono tujadili hili jambo kwa kina kwa sababu inaonekana sera haziko vizuri katika Wizara ambayo anaiongoza.

**MWENYEKITI:** Fafanua kitu gani hasa ambacho hujaridhika nacho.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sijaridhika kwa namna alivyoeleza kwamba vilabu vya michezo vinasajiliwa BMT, nakubali, hilo halina wasiwasi. Hata hivyo, hapa tunazungumza suala zima la uwekezaji. BMT imeanzishwa miaka mingi iliyopita ambapo wakati huo hakukuwa na uwekezaji, vilabu vilikuwa vinaendeshwa kwa ridhaa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ulimwengu umebadilika na tunataka kupeleka kwenye uwekezaji. Kwa hiyo tunataraji kwamba tukiendelea kutumia Sheria ya BMT ambayo imeundwa kwa ajili ya michezo ya kiridhaa maana yake tutazidi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho nataka kumkubalia ni kwamba akiri kabisa kwamba Sera ya Uwekezaji ambayo tunaitaka sasa, siyo hii ya zamani ambayo ilikuwa inaandaa michezo ya kiridhaa, ndiyo ambayo itakuja kuwa mwarobaini wa hili suala. Kwa kuwa mamlaka za Kiserikali ndizo zinazokwamisha huu mchakato, basi ifanyike jitihada ya makusudi ili Simba iwe mfano wa vilabu vingine kuingia katika uwekezaji na tuondokane na huu mpira wa ridhaa ambao ndiyo unarudisha Taifa letu nyuma katika michezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Michezo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kukiri *concern* ya Mheshimiwa Shangazi kwamba ipo fursa kubwa katika kuwekeza katika Tasnia ya Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwondoa wasiwasi, Serikali tayari jambo hili tumelitazama. Kwa mfano, kwa upande wa michezo kupitia Baraza la Michezo Tanzania kwenye kifungu cha 18A ili kuvutia uwekezaji katika michezo, kifungu hiki kinasema mwekezaji anaweza akawekeza kwenye Klabu kwa asilimia zisizopungua 49 za hisa. Kwa hiyo hata kwa upande wa Simba tumetumia sheria hii katika kuratibu mazungumzo ambayo yanaendelea na taarifa nilizonazo ni kwamba Jumatatu *FCC* pamoja na Simba wataendelea kukaa ili kuangalia namna ya ku-*facilitate* uwekezaji katika Klabu ya Simba. Kwa hiyo, napenda kumwondoa wasiwasi Mheshimiwa Shangazi na Watanzania kwamba, Serikali inayo dhamira ya kuhakikisha uwekezaji unakwenda kwenye tasnia zote ikiwemo ya michezo na sanaa. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, unarudisha shilingi sasa?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya ya Mheshimiwa Waziri wa Michezo kwa sababu ndiyo mwenye eneo lake na namwona amelizungumza kwa wivu mkubwa kwamba atasaidia hili jambo likamilike, basi nawarudishia shilingi yao waendeleo na kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, tukiendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri kama jambo linachukua miaka inakuwa haipendezi. Inatakuwa ndugu zetu wa *FCC* watoke wazi wawe wanaeleza ni kitu gani kinachoendelea, hii ni Klabu kubwa Afrika. Sasa hatuwezi kuwa tunataka kwenda nusu fainali Afrika tuchukue kombe, halafu hapa nchini sasa kuna vyombo vingine vinarudisha nyuma miguu, inakuwa haipendezi, au siyo Waheshimiwa. Ili ikiwezekana basi wale rafiki zetu nao waige. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la sera kwa Waziri Mkuu.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nakusudia kuondoa shilingi kama majibu ya Mheshimiwa Waziri hayatajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu tunazo changamoto mbalimbali kwenye Sera yetu ya Uwekezaji. Sasa napenda zaidi kupata ufafanuzi ili kuhakikisha kwamba Sera ya Uwekezaji inaendana na mahitaji ya sasa. Tunafahamu vipo vyombo vingi ambavyo vinatakiwa vichukue hatua mbalimbali zitakazoweza kusaidia, hasa taasisi kama *OSHA*, *WCF* na nyingine zinazofanana ili ziweze kuchangia vizuri kwenye sekta hii na hasa kwenye Sera ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuwe na uwekezaji salama na pia kusaidia makundi mengi zaidi ya vijana ikiwezekana yaweze kukopa na kuwekeza hapa nchini ili

tuone tija halisi ya uwekezaji kwa wazawa. Je, ni nini na mkakati gani sasa Serikali imechukua kuhakikisha kwamba taasisi hizi na zenyewe zinakuwa ni sehemu ya kuchangia Sera hii ya Uwekezaji ili iwe bora zaidi na kuwezesha haya yote. Nakushukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye suala zima la uwekezaji ni shirikishi, linashirikisha sekta nyingine za ziada kwa sababu unapozungumza masuala ya uwekezaji unazungumza masuala pia ya utengenezaji wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia masuala ya utengenezaji wa ajira, ni lazima utakutana na taasisi ambazo zinaongozwa na mikataba tuliyoridhia ya Shirika la Kazi Duniani na sera ambazo zinasimamia ustawi wa wafanyakazi. Kwa hiyo sera zinazosimamia ustawi wa wafanyakazi ambazo zinatungiwa sheria ni pamoja na sheria zilizoanzisha hizo taasisi zinazoweza kufanya kazi kwenye maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane naye kwamba, sheria hizi zimekuwa zikitungwa na zikichukua sura tofauti na leo asubuhi mmemsikia vizuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba ni lazima tufanye mapitio ya sheria tulizonazo kuhakikisha kwamba pamoja na mikataba tunayoridhia ya Shirika la Kazi Duniani, pamoja na sera tunazotunga ambazo zinatakiwa kulinda pia ustawi wa wafanyakazi, lazima sera na sheria tunazozitunga zisiwe zinakinzana na mwelekeo na maagizo ya Serikali na hata Mheshimiwa Rais ameshayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa mfano hapa wa Mfuko wa Fidha kwa Wafanyakazi. Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Fidha wa Wafanyakazi inawataka waajiri kwenye *private sector* na *public sector* kuchangia Mfuko huo. Kwa mujibu wa sheria *private sector* wao wanachangia asilimia moja ya mshahara wa mfanyakazi lakini kwenye *public sector* ni 0.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumejifunza baada ya *application* ya hiyo sheria, tumegundua kwamba *private sector* hawako *comfortable* na *ratio* hiyo ya uchangiaji kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Kwa hiyo tulichokifanya ni kufanya *actuarial valuation* tena, utathmini wa Mfuko huo wa Fidua kwa Wafanyakazi na tayari tumeshaleta mapendekezo sasa kuondoa hicho kikwazo ili *private sector* wasikwazwe kwenye uwekezaji kwa sababu ya Sheria hiyo ya Fidua kwa Wafanyakazi. Pia wakati huo huo tuendeleo kulinda wafanyakazi kwa sababu Mfuko huo una kazi nzito sana ya kuwahudumia wafanyakazi wanapoumia kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo tuendeleo kulinda wafanyakazi kwasababu mfuko huo una kazi nzito sana ya kuwahudumia wafanyakazi wanapoumia kazini. Pia OSHA na *Workers Compensation* ni kama mtu na dada yake, kuna mmoja kazi yake ni kulinda wafanyakazi wasingie kwenye magonjwa ya *Occupation Health* kwenye magonjwa yanayotokana na kazi na kuna mwingine kazi yake ni kuwatibu pale inaposhindikana na magonjwa yametokea. Kwa hiyo, sasa huyu OSHA wajibu wake ni *ku-protect* akifanya kazi nzuri ya ulinzi hata hawa *Workers Compensation* hawi na kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulichokifanya, tulikuja kugundua kwamba baada ya kujitathimini OSHA na kwa kweli hapa naomba niwashukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria. Walipitia tozo zote ambazo zinatozwa na OSHA na tukagundua kuna tozo nyingine sio rafiki na ni tozo za makusudi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano labda hapa nitaomba uniruhusu nirudi kwenye misaafu yangu kidogo, kwa mfano OSHA walikuwa wanatoza tozo ya mafunzo, kwamba wao wanatakiwa kuwafundisha waajiri kuhusu umuhimu wa ulinzi wa afya za wafanyakazi lakini wanapoenda kuwafundisha waajiri wanaenda tena kuwa toza wale waajiri walipe tena tozo kwa kwenda kuwafundisha wafanyakazi wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mshiriki ukimuita OSHA kwenye taasisi yako ya kazi kila mshiriki atakayehudhuria mafunzo yale alikuwa anatakiwa alipe 250,000/=, wakati huo hao OSHA wamelipwa mshahara na Serikali kufanya kazi hiyo ya kufundisha. Kwa hiyo, tukawaambiwa kwamba jambo hilo haliwezekani. Eneo jingine yapo maeneo mengi kama kumi na kitu lakini nitasema machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano eneo jingine kukitokea ajali kwenye eneo la kazi OSHA kazi yao ni kwenda kuchunguza chanzo cha ajali wanawajibu wa kufanya hivyo na wanalipwa na Serikali yetu kwa kazi hiyo, lakini ilikuwa wakifika pale wanaenda tena kumtoza mwajiri shilingi 500,000 kwa kila mtaalam atakayekuwa ameenda kufanya uchunguzi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukaona kwamba hizo Tozo kwa kwakweli sio rafiki ama ili mwajiri ajisajiri alikuwa anatakiwa kulipa 50,000 mpaka 1,800,000 kwa hiyo, tuliwaagiza OSHA watoe hizo tozo ambazo zilikuwa ni tozo zinazozuia uwekezaji kukua nchini na wameziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maagizo yetu kwa OSHA tumewaambia waendeleo kufanya tathimini ya tozo zilizobaki ambazo sio rafiki kwa mfano walikuwa wanatoza tozo ya uwepo vifaa Kinga vya moto wakati kazi hiyo inatakiwa ifanywe na Mamlaka ya *Fire* sio kazi yao, tumewaambia waiondoe na wabaki na zile tozo ambazo...toka tumefanya hivyo *compliance* mwaka 2020 imeongezeka kwa usajili wa maeneo ya waajiri 26,740 ukilinganisha na waajiri 11,963 kwa mwaka 2018. Kwa hiyo tunazingatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula

**MHE. STANLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa majibu ya kina sana ya Mheshimiwa Waziri na hakika hivi vyombo viwili vimekuwa na changamoto kubwa sana hasa OSHA na kama haya aliyoyasema Mheshimiwa Waziri yatafanyiwa kazi sawa sawa hakika OSHA

atakuwa ni mlezi na atakuwa ni suluhisho na muhimili wa kusimamia sera nzuri zitakazosaidia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimeridhika na majibu narudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa, kwenye mchango wangu mbali na mambo mengine nilizungumzia Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo tuliipisha mwaka 2018 na wewe ni shahidi uliona taharuki iliyotokea baada ya mambo fulani fulani wafanyakazi na wastaafu wa nchi hii kutoridhika nayo. Wewe ulikuwepo wakati Rais ameingilia kati na kuona ni namna gani wafanyakazi wanatarajiwa wapewe kile ambacho walikuwa wanakiomba kwasababu walieza tangu awali tunahitaji kikokotoo chetu kiwepo kwenye sheria kisiwepo kwenye *regulation*. Matokeo yake yakafanyika ndivyo sivyoyote na kikaja kikokotoo kibaya zaidi cha 1/580 tofauti ya kile ambacho walipendekeza 1/520 au walau kingebaki kile cha 1/540. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini? Hivi tunavyozungumza baada ya Mheshimiwa Rais Hayati kusitisha kulikuwa kuna wimbi la watu ambao wanastaafu kwa hiari waone bora hebu tumalize tuchukue chetu maana hatujui 2023 kitatokea nini, lakini matokeo yake mbali na kustaafu kwa hiari bado hawapati hayo mafao yako kwa wakati kwasababu vile vile wanakutana na changamoto ya mifuko haina pesa za kutosha. Lakini vile vile hivi tunavyozungumza hata hawa wanaofanya kazi kwa uaminifu, kwa uadilifu, kwa jasho na damu mbali ya mazingira magumu, mishahara midogo bado hawajui hatma yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Bunge na hapa hatuhitaji kufanya mabadiliko ya sheria nzima tunahitaji kufanya mabadiliko madogo ili wafanyakazi wetu *wa-relax*, wajue tukimaliza utumishi wetu kuna sheria inatulinda,

tumeshirikishwa vyema na tutahitaji tupate stahiki zetu. Sikupata majibu ya kutosha, tunahitaji *commitment* ya Serikali lini, lini wataleta msawaada tufanye marekebisho wastaafu wetu wawe na uhakikia baada ya utumishi wao wanapata kitu wanachostahiki na nisiporidhika naondoa shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**, Ufafanuzi wa jambo hili Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* ya Mheshimiwa Ester Bulaya ndio *concern* ya Serikali. Ninashukuru alitambua pia kazi nzuri iliyofanywa na Hayati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia jambo hili na hiyo ilionyesha kwamba tu kunijali wafanyakazi. Lakini nadhani mmesikia Mheshimiwa Rais wetu mama Samia na yeye anakwenda hukuhuko na hata alipokuwa anaapisha Makatibu Wakuu alizungumza jambo hilo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimwambie kwanza tu kiujumla niseme kwamba Serikali yetu inatambua ni lazima wastaafu, wastaafu wanapokwisha kustaafu wasihangaishwe waweze kupata mafao yao katika viwango ambavyo wameridhika navyo. Wakati Hayati Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 28 Desemba, 2018 alipokuwa anatoa maelekezo kwangu aliyaleta maelekezo kwangu kusimamia *transition period* ambayo itatupeleka kwa miaka kadhaa ili tuweze kufikia muafaka na makubaliano ya kina kati ya wafanyakazi na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo imekwisha kuanza kufanyika na imeshafika asilimia sabini ya kazi nzima iliyotakiwa kufanyika na ninataka kusema nini, kwanza kabisa ilikuwa ni kuzingatia mahitaji ya wafanyakazi katika kutengeneza mustakabali mpya wa kuwa na hicho kikotoo rafiki ambacho kitakubaliwa na wafanyakazi lakini na Serikali lakini kikiwa na mwelekeo wa kuhakikisha kwamba mifuko hii pia inakuwa *sustainable* na bahati nzuri kamati ambayo tumeiunda tena *technical committee* ya kufanya kazi ya

jambo hili wajumbe wake asilimia 75 wanatoka kwenye vyama hivyo vya wafanyakazi wenyewe kusudi tuwape *morals authorities* ya kujadili jambo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kazi hiyo imekwishakufanyika siwezi tu *ku-disclose* kile kilichokwisha kufanyika mpaka sasa kwa sababu bado kinatakiwa kirudishwe kwenye *Steering Committee*, na *Steering Committees* sasa itaunganisha vyama vya wafanyakazi wote, vyama vya wafanyakazi vyote na baada ya hapo tutakuwa sasa na mjalada wa pamoja na tukimaliza ule mjadala wa pamoja kusudi tufikie muafaka ambao utakuwa ni muafaka shirikishi kati yetu sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huwezi kwenda na jambo hili na ukafanikiwa *option* ndio zimeshatengenezwa na zimeshawekwa vizuri lakini lazima uzi-*test*, unazi-*test* vipi kwenye *sustainability* ya mfuko kama hujamaliza kufanya *actuarial*. Sasa *actuarial* nimesema hapa asubuhi kwamba imeshakamilika na sasa hivi sasa inafanyika upembuzi wa hiyo ripoti kuiona imekaaje ili sasa uweze *ku-test* kila jambo lililotukia na utathimini ambao umekwishakufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli wala siwezi kwenda ninavyoamini kwa ushirikiano tunaopata kwenye vyama vya wafanyakazi siamini kama jambo hili tunaweza tukavuka nalo sana mpaka mwakani, ninaamini kabisa mwaka huu jambo hili tunaweza tukamalizana nalo. Na tukimalizana nalo tutakuwa tuko ndani ya muda miaka miwili kabla hata ya muda ule ambao ulikuwa umepangwa. Muda ilikuwa uende mpaka 2023 lakini tunaamini kabisa ndani ya mwaka huu jambo hili tutakuwa tumelimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo miongozo kutoka kwa Mkuu Wangu wa Kazi Mheshimiwa Waziri Mkuu na Miongozo hiyo yote hiyo nimeshaifanyia kazi na *document* zote zinazotakiwa zimekwisha kuandaliwa. Kwa hiyo, naomba niwape *comfort* wafanyakazi watulie. Wafanyakazi wenzao waliowaleta wao wenyewe wasimamie jambo hili



wanalisimamia vizuri na ninaamini *this time around* tutakuja ndani ya Bunge na ripoti ambayo itakuwa *so friendly* ambayo inamilikiwa na wafanyakazi wenyewe. *This is my commitment*, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa hiyo *commitment* yake lakini cha kusisitiza tunapozungumza kila siku unakuwa unaniambia tunafanya tathimini, tunafanya tathimini sasa hii tathimini tangu 2018 haijakamilika sasa nafikiri ni vyema wote sisi Wabunge na Serikali tutimize wajibu wetu. Raisi *ali-risk situation*, alikuwa amesitisha tu ule mjalada aliokoa jahazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuokoa jahazi kwake yeye hatukufanyi sisi tutimize wajibu wetu wa kutunga sheria nzuri kwa wafanyakazi, ameokoa jahazi, Mama Samia naye amesema hivyo hivyo lakini wale ni viongozi sisi kazi yetu ya Bunge ni kutunga sheria, kwa sababu *commitment* yako umesema mwaka huu hauishi dada yangu nakurudishia shilingi yako nenda kaendeleo na majukumu yako leta huo Muswada tulinde maslahi ya wafanyakazi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya AG shughuli hiyo. Mwaka huu utuletee Muswada. Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nina swali la kisheria au la kisera kubwa kwa DPP katika baadhi ya makosa hasa yale ambayo yana-follow kwenye uhaini, ugaidi, *money laundry na* uhujumu uchumi. Sheria hii iliyopo kwa kweli inampa DPP muda mfano anaotaka katika kuendesha kesi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo utakuta watuhumiwa wanakaa magereza kwa muda mrefu, miaka saba, miaka nane, miaka kumi bila kesi zao kukamilika. Sasa tunaomba, tunataka *commitment* ya Serikali lini italetwa

Muswada angalau uwe na muda maalum ya kuchunguzwa kesi hizi mpaka kufikia muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu bila hivyo inawaumiza sana watuhumiwa, kifamilia leo kuna familia wake wanadai takala waume zao wakiwa magerezani. Uchumi katika familia na mambo kama hayo kwa hivyo tunaomba *commitment* ya Serikali ili haki za binadamu mtu kama ana kosa litambulike ahukumiwe na ahesabu hukumu yake kwa miaka yake kuliko kuwa imekaa tu hivi bure bure. Ahsante nakusudia kama sikupata majibu ya kutosha basi na mimi nishike shilingi. *(Makofi)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa alikuwa anafikiria mume yuko jela halafu mke anadai talaka sasa inakuwaje hapo, talaka inapita dirishani inapita wapi ni AG au nani atajibu hili, naam, ndio Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado mwongozo wako kwenye *Vote* hii 37 ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haya siyo majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na masuala ya kisera kwenye *Vote* hii yanatakiwa yawe ni masuala ya kisera yanayohusiana na shughuli ambazo zipo ndani ya Waziri Mkuu. Lakini Kanuni zetu pia haziruhusu kuwaisha shughuli kwasababu masuala ya Utawala Bora yatawasilishwa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sijui kwa mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa jitetee bwana.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ni *overall* kwa kweli kila jambo ambalo linahusu Serikali basi Waziri Mkuu ni mhusika mkubwa kwa hivyo mambo haya nafikiri tusiyakwepe tuyaogelea tu ili tupate jawabu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye *overall* na msimamizi wa ujumla wa Serikali lakini wako wasimamizi wa kisekta ambao ni Waheshimiwa Mawaziri na hawa Waheshimiwa Mawaziri huwa wanapewa *instrument* na Mheshimiwa Rais inayo waeleza mambo mahsusi wanayopaswa kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge amezungumzia masuala ya *DPP*, masuala ya mwenendo wa kesi za jinai na mambo yanayofanana na hayo haya yote yako katika sheria ambazo zipo chini ya uangalizi na usimamizi wa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa hiyo, muda muafaka wa kuyaibua haya au kuyaleta ni wakati Wizara ya Katiba na Sheria inawasilisha bajeti yake hapa. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakubaliana na ushauri huo kwa hiyo Mheshimiwa Khalifa haina shida liko mbele siku ya Katiba na Sheria basi ulikumbuke. Kwenye mshahara wa Profesa. Tunaendelea na wa mwisho Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii pia natarajia kwamba nisiporidhika na maelezo ya waziri basi nitashika shilingi kwenye mshahara wake kwasababu suala la lishe ni suala muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba suala hili linapewa kipaumbele ikiwemo kwamba chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuna Kamati ya Kitaifa ya Lishe ambao wajumbe ni Makatibu Wakuu kutoka Wizara nane pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI lakini kwa kawaida huwa Makatibu Wakuu hawashiriki kwenye mkutano huo muhimu badala yake mara

nyingi anakuwepo Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na Katibu Mkuu wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linakwenda kuffisha jitihada kubwa za Serikali katika kuhakikisha kwamba tunatokomeza udumavu na aina zote za utapia mlo. Kwa hiyo, ningependa kufahamu Serikali inajipanga vipi katika suala hili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Makatibu Wakuu hawakai.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikuwa na mpango jumuiishi wa masuala yanayohusiana na lishe kuondoa udumavu nchini, ukondefu na uzito uliokithiri ili kufanya Taifa letu la Tanzania liwe na Afya lakini kikubwa ilikuwa ni kuboresha afya za watoto chini ya miaka mitano, akinamama wajawazito na vijana balehe na hasa wasichana wanaotarajia kuingia kwenye umri wa uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti Mpango wa kwanza wa miaka mitano wa kuhakikisha kwamba tunapambana na tatizo hili la lishe nchini ulianza mwaka 2015/2016 na unatarajia kuisha mwaka huu wa 2021. Lakini tunajipanga kuwa na mpango mwingine wa kuhakikisha tunapambana na tatizo la lishe kuanzia Juni, 2021 mpaka Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza kusema hivyo, nimesema hayo kwasababu ndani ya Mpango huo wa Taifa wa miaka mitano jumuisho kupambana na tatizo la lishe nchini ndio unaweka pamoja ikiwemo Makatibu Wakuu kwenye wizara zinazohusika, Mawaziri wote kwenye wizara zinazohusika na wadau wengine wakiwemo taasisi binafsi na Taasisi za Kimataifa na kama nilivyosema hapa asubuhi Taasisi ya *AGRO-THAMANI* ambayo ipo chini ya Mheshimiwa Neema kwa kweli imekuwa inatoa mchango mkubwa sana kwenye mapambano haya ya kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la lishe nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimuhakikishe Neema yafuatayo:- Kwanza baada ya kuona kwamba mikakati na mipango iliyopita imelegalega kama mtamkumbuka Waheshimiwa Wabunge kwenye Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano suala la lishe sasa limeingizwa rasmi na liweze kusimamiwa vizuri na kila mwaka itakuwa ni fursa yetu kama Bunge kuhoji sasa kila mpango mmoja wa utekelezaji wa bajeti tumetelekezaje hili suala la lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano unatokana na Ilani ya uchaguzi, Ilani ya Uchaguzi kwa mara ya kwanza imezungumza suala la lishe kwenye Ilani ya Uchaguzi ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na afya bora. Lakini kuna maendeleo ambayo yamejionyesha. Kwa mfano tumekuwa tukipambana sana na suala la udumavu tulikuwa tunataka kuhakikisha tunauondoa udumavu nchini kutoka asilimia 34 ya Watoto chini ya miaka mitano lakini tumeweza kufika asilimia 32 kwa mwaka 2018 toka mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa tuliyobakia nayo ni kuondoa uzito uliokithiri na Mheshimiwa Nyongo asubuhi hapa amesema magonjwa yasiyoambukiza ndiyo yanayoendelea kuwa mengi kwa sasa hivi. Taarifa tulizonazo sasa mwaka 2014 watoto wa kike waliofikia umri wa kuzaa walikuwa na uzito uliokithiri kwa asilimia 29 lakini ilivyofika mwaka 2018 kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa kike wanaofikia umri wa kuzaa mpaka asilimia 31.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba viliba tumbo yaani vitambi kwa wanawake na wanaume vinaendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa na hiyo kwa kweli ni hatari. Lakini tunaompango mwingine wa kuhakikisha tunatumia virutubishi kwenye vyakula na ninaamini tukifanya hivyo Mheshimiwa dada yangu Neema na kuwasimamia hao Makatibu Wakuu na kuweka kwenye mpango wa miaka mitano, mpango wa mwaka mmoja mmoja nadhani sasa kila mmoja atawajibika na tunaweza tukafika hatua nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema umeridhika?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika na majibu mazuri na ahadi alizotoa Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nitarudisha shilingi. Hata hivyo, katika yote aliyoyasema naomba kuongezea pia suala la upungufu wa nguvu za kiume kwa vijana. Kwa sababu nayo imethibitika ...

**MWENYEKITI:** Hilo unapaswa kuomba ruhusa. Haya nakupa ruhusa sasa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nimesema kwa vijana kwa sababu nakumbuka hata dada yangu Mheshimiwa Umyy Mwalimu alivyokuwa Waziri wa Afya aliweza kuthibitisha kwamba kuna ongezeko kubwa la tatizo la nguvu za kiume kwa vijana na hiyo inatokana na lishe duni. Kwa hiyo nalo, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu inashughulika na masuala ya vijana, basi naomba hilo nalo liongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kila la kheri dada yangu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge wanaume mnalalamika nini? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa tungeanza *test* kwanza humu humu.

**MWENYEKITI:** Mnapopata ushauri huo kutoka kwa wadau sasa mnalalamika kitu gani? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye *test*.

**MWENYEKITI:** Tukirudi kwenye lishe Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Iringa tuliambiwa hapa asubuhi kwamba ndiyo mnaongoza katika lishe duni. Nadhani ni sawa kwa Mkoa wa Iringa?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Udumavu.

**MWENYEKITI:** Ooh ni udumavu. Mkoa mwingine kutoka chini ni upi? Ni lringa na wapi na wapi?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa yote ambayo inazalisha chakula kwa wingi yaani *food basket* inaongoza kwa tatizo la udumavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Eeeeh! Mheshimiwa Waziri Songea imo. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, lringa inaongoza kwa asilimia 47 na kitu inafuatiwa na Songwe asilimia 43, inafuatiwa na Ruvuma asilimia 41, kwa hiyo, mikoa mitatu hii ndio hasa inaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya kufanya kitu na suala kubwa ni kwamba mikoa hii inazalisha chakula kwa wingi lakini haijui namna ya kukitumia chakula hicho kwa kukiandaa ili iwe mlo kamili. Pia nadhani na matatizo mengine kama ulevi uliokithiri na vitu vya namna hiyo kuna haja ya kuangalia.

**MWENYEKITI:** Watoto badala ya kupewa chakula wanapewa ulanzi, kindi, kimpumu. Katibu tuendeleo, tumeshamaliza wale wa maswali ya sera.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – Finance and Accounts Units.....	Sh.1,359,714,000
Kifungu 1003 – Policy and Planning Unit.....	Sh.655,318,000
Kifungu 1004 – Internal Audit Unit.....	Sh.358,348,000
Kifungu 1005 – Government Communication Unit.....	Sh. 228,905,000

Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.333,456,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.205,800,000
Kifungu 1008 – <i>Management Information System Unit</i> .....	Sh.229,622,000
Kifungu 2001 – <i>Civil Affairs and Contingencies</i> .....	Sh.2,627,101,000
Kifungu 2002 – <i>National Festivals</i> .....	Sh.588,314,000
Kifungu 3001 – <i>Parliamentary and Political Affairs</i> .....	Sh.550,753,000
Kifungu 4001 – <i>Private Sector Development and Economic Empowerment</i> .....	Sh.2,275,850,000
Kifungu 5001 - <i>Coordination of Government Business</i> .....	Sh.769,931,000
Kifungu 6001 - <i>Investment Development Division</i> .....	Sh.152,820,000
Kifungu 7001 – <i>Government Printer</i> .....	Sh.2,543,134,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **FUNGU 11 – UWEKEZAJI**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh.1,464,640,000
Kifungu 2001 - <i>Investment Services</i> .....	Sh.5,553,573,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **FUNGU 15 – TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh.1,456,096,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.92,760,000
Kifungu 1003 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i> .....	Sh.169,986,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.138,020,000
Kifungu 1005 – <i>Information, Communication and Technology Unit</i> .....	Sh.236,781,000



Kifungu 1006 – <i>Procurement Management</i>	
<i>Unit</i> .....	Sh.130,150,000
Kifungu 2001 – <i>Mediation</i> .....	Sh.806,400,000
Kifungu 2002 – <i>Arbitration</i> .....	Sh.843,232,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **FUNGU 25 – OFISI BINAFSI YA WAZIRI MKUU**

Kifungu 1001- <i>Administration and Human</i>	
<i>Resources Management</i> .....	Sh.11,090,619,000

*(Kifungu kilichotahwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **FUNGU 27 – OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Kifungu 1001- <i>Administration and Human</i>	
<i>Resources Management</i> .....	Sh.713,974,350
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.243,991,643
Kifungu 1003 - <i>Planning, Monitoring, Evaluation and</i>	
<i>Research</i> .....	Sh.193,715,421
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit</i> .....	Sh.171,980,279
Kifungu 1005 – <i>Procurement Management</i>	
<i>Unit</i> .....	Sh.145,615,724
Kifungu 1006 - <i>Information and Communication</i>	
<i>Technology Unit</i> .....	Sh.209,471,292
Kifungu 1007 – <i>Communication and Civic</i>	
<i>Education Unit</i> .....	Sh.128,281,965
Kifungu 1008 – <i>Registration &amp; Monitoring of Political</i>	
<i>Parties Division</i> ... ..	Sh.235,169,357
Kifungu 1009 - <i>Election Expenses and</i>	
<i>Grants Division</i> .....	Sh.17,748,889,253
Kifungu 1011 - <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh. 208,706,712

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resources Management Division</i> .....	Sh.11,402,130,500
Kifungu 1002 – <i>Library and Research Division</i> .	Sh.501,776,000
Kifungu 1003 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh.1,198,105,500
Kifungu 2001 – <i>Budget Division</i> .....	Sh.2,556,398,000
Kifungu 2002 – <i>Table Office Division</i> .....	Sh.82,903,793,000
Kifungu 2003 – <i>Parliamentary Committee Division</i> .....	Sh.11,573,666,000
Kifungu 2004 – <i>Hansard Unit</i> .....	Sh.904,352,000
Kifungu 2005 – <i>Legal Services Division</i> .....	Sh.2,044,288,000
Kifungu 3001 – <i>Private Office of the Speaker</i> .....	Sh.1,134,271,000
Kifungu 3002 – <i>Private Office of the Deputy Speaker</i> .....	Sh.801,672,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3003 – <i>Office of the Leader of Opposition</i> .....	Sh.185,260,000
--	----------------

**SPIKA:** Nilikuwa najjuliza cha nini hiki?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo iko wapi? *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3004 - <i>Private Office of the Clerk</i> .....	Sh.1,057,602,000
Kifungu 3005 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.824,942,000
Kifungu 3006 - <i>Communication and International Relations Unit</i> .....	Sh.2,506,911,000
Kifungu 3008 – <i>Internal Audit</i> .....	Sh.452,056,000
Kifungu 3009 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.603,543,000
Kifungu 3010 – <i>Defense and Security Unit</i> .....	Sh.996,740,000

Kifungu 3011- <i>Estate Management</i> .....	Sh. 0
Kifungu 3012 – <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh.228,400,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 61 – TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.3,719,821,000
Kifungu 1002 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Division</i> .....	Sh.538,927,000
Kifungu 1003 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.541,169,100
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 401,365,000
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Shs. 469,675,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management and Logistics Unit</i> .....	Sh. 539,325,000
Kifungu 1007 – <i>Zanzibar Office</i> .....	Sh. 329,900,000
Kifungu 2001 – <i>Election Management Division</i> .....	Sh. 719,636,000
Kifungu 2002 – <i>National Voters Registration and ICT Division</i> .....	Sh. 815,504,000
Kifungu 2003 – <i>Voters Education and Public Information Division</i> .....	Sh. 713,028,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 65 – OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMEVU**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resources Management</i> .....	Sh. 2,087,495,612
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 314,426,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.382,787,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit</i> .....	Sh.181,757,500
Kifungu 1005 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 220,273,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*  
Kifungu 1006 – *Government Communication*  
*Unit.....Sh.*  
50,652,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho cha 1006 kasma ya 22003 kwenye *fuel, oil; and up country*. Naona *this time* hawajatengewa kabisa. *So, I just wondering*, hawa watu hawahitaji hizo *service?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya matumizi hayo imetengwa kwenye fungu la utawala, kule ambako tumetoka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1007 – *Information and Communication*  
*Technology Unit.....Sh. 243,143,000*  
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit.....Sh. 155,788,000*  
Kifungu 2001 – *Labour.....Sh. 4,936,678,262*  
Kifungu 2002 – *Employment Division.....Sh. 502,189,000*  
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions.....Sh. 89,124,000*  
Kifungu 2004 – *Arusha Regional Labour Office.....Sh. 18,655,000*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa sasa mvumilie maana tunaenda mkoa kwa mkoa.

Kifungu 2005 – *Dodoma Regional Labour Office..Sh. 17,405,000*  
Kifungu 2006 – *Geita Regional Labour Office....Sh. 14,955,000*  
Kifungu 2007 – *Iringa Regional Labour Office.....Sh. 19,755,000*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 2008 – Kagera Regional Labour Office....	Sh. 11,205,000
Kifungu 2009 – Kigoma Regional Labour Office...	Sh. 9,455,000
Kifungu 2010 – Kilimanjaro Regional Labour Office.....	Sh. 10,805,000
Kifungu 2011 – Lindi Regional Labour Office.....	Sh. 9,855,000
Kifungu 2012 – Manyara Regional Labour Office...	Sh. 7,400,000
Kifungu 2013 – Mara Regional Labour Office.....	Sh.10,305,000
Kifungu 2014 – Mbeya Regional Labour Office....	Sh. 15,505,000
Kifungu 2015 – Morogoro Regional Labour Office.....	Sh. 18,505,000
Kifungu 2016 – Mtwara Regional Labour Office....	Sh. 15,600,000
Kifungu 2017 – Mwanza Regional Labour Office.....	Sh. 15,940,000
Kifungu 2018 – Njombe Regional Labour Office....	Sh. 8,635,000
Kifungu 2019 – Pwani Regional Labour Office.....	Sh.15,700,000
Kifungu 2020 – Rukwa Regional Labour Office....	Sh. 8,000,000
Kifungu 2022 – Ruvuma Regional Labour Office...	Sh. 10,145,000
Kifungu 2023 – Shinyanga Regional Labour Office .....	Sh.10,115,000
Kifungu 2025 – Singida Regional Labour Office....	Sh. 10,502,500
Kifungu 2026 – Tabora Regional Labour Office.....	Sh. 11,082,500
Kifungu 2027 – Tanga Regional Labour Office.....	Sh.18,755,000
Kifungu 2028 – Temeke Regional Labour Office....	Sh. 10,630,000
Kifungu 2029 – Kinondoni Regional Labour Office.....	Sh. 10,710,000
Kifungu 2030 – Ilala Regional Labour Office.....	Sh. 17,100,000
Kifungu 2031 – Social Security Division.....	Sh. 502,983,036
Kifungu 2032 – Youth Development.....	Sh. 824,658,000
Kifungu 2033 – Employment Services Unit.....	Sh. 763,959,000
Kifungu 2034 – Persons with Disability Unit.....	Sh. 1,290,780,000
Kifungu 2035 – Productivity Promotion Unit.....	Sh. 269,747,090

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**FUNGU 91 – MADAWA YA KULEVYA**

Kifungu 1001 – Administration & Human Resources Management.....	Sh. 8,529,797,000
--	-------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 92 – TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA  
(TACAIDS)**

Kifungu 1001 – <i>Policy, Planning and Research</i> ...	Sh. 196,720,000
Kifungu 1002 – <i>Finance, Administration &amp; Resource Mobilization</i> .....	Sh. 868,552,000
Kifungu 1003 – <i>Monitoring &amp; Evaluation</i> .....	Sh. 211,896,000
Kifungu 1004 – <i>Advocacy and Information Unit</i> .....	Sh. 299,728,000
Kifungu 1005 – <i>National Response</i> .....	Sh. 599,456,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 170,852,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 152,749,000
Kifungu 1008 – <i>Management Information Systems Unit</i> .....	Sh. 81,180,000
Kifungu 1009 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 149,861,000
Kifungu 1010 – <i>Special Programs Unit</i> .....	Sh. 142,334,000
Kifungu 1011 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 55,020,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 27 – MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa 29, Fungu 27.

**MBUNGE FULANI:** Aliongea nje ya microphone.

**MWENYEKITI:** Ongeeni kwenye chombo.

**MBUNGE FULANI:** Mtandao uko chini.

**MWENYEKITI:** Aah, mtandao uko chini! Basi nisikilizeni mimi.

Twende Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management.....*Sh. 2,000,000,000

**MWENYEKITI:** Hii ni ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa upande wa maendeleo. Shilingi bilioni mbili – ni masuala ya Office Building.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu tuendelee.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**  
Tunakwenda ukurasa wa 65.

### FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa 65, fungu 37 kwenye Kitabu cha Maendeleo. Twende Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management.....* Sh. 1,500,000,000

Kifungu 5001 – *Coordination of Government Business.....*Sh. 3,521,344,000

Kifungu 7001 – *Government Printer.....*Sh. 2,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**  
Tunakwenda ukurasa wa 79.

**FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE**

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resource Management</i> .....	Sh. 3,720,000,000
Kifungu 1003 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2001 – <i>Budget Division</i> .....	Sh. 1,997,471,000
Kifungu 3004 – <i>Private Office of the Clerk</i> .....	Sh. 1,280,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Nakwenda ukurasa wa 154.

**MWENYEKITI:** Tume ya Uchaguzi, ukurasa wa 154, Fungu 61.

**FUNGU 61 – TUME YA UCHAGUZI**

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Kifungu 2001 – <i>Election Management Division</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2002 – <i>National Voters Registration and ICT Division</i> .....	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Tume ya Uchaguzi wao hawana fedha za maendeleo kwa mwaka huu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Tunakwenda ukurasa wa 171.



**FUNGU 65 – OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA  
NA WENYE ULEMAVU)**

**MWENYEKITI:** Kazi na ajira, Ofisi ya Waziri Mkuu.  
**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh. 23,000,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Division</i> .....	Sh. 188,500,000
Kifungu 2001 – <i>Labour</i> .....	Sh. 115,000,000
Kifungu 2002 – <i>Employment Division</i> .....	Sh. 9,598,000,000
Kifungu 2031 – <i>Social Security Division</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2032 – <i>Youth Development</i> .....	Sh. 1,802,030,000
Kifungu 2033 – <i>Employment Services Unit</i> .....	Sh. 87,500,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**  
Tunakwenda ukurasa wa 370, Fungu 92.

**FUNGU 92 – TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (TACAIDS)**

**MWENYEKITI:** Tuendeleo Katibu, *TACAIDS*, ukurasa wa 370.

Kifungu 1001 – <i>Policy, Planning and Research</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1002 – <i>Finance, Admin. &amp; Resource Mobilization</i> .....	Sh. 1,000,000,000
Kifungu 1003 – <i>Monitoring and Evaluation</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1004 – <i>Advocacy and Information Unit</i> .....	Sh. 225,038,000
Kifungu 1005 – <i>National Response</i> .....	Sh. 164,432,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1008 – <i>Management Information Systems Unit</i> ...	Sh. 0
Kifungu 1009 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1010 – <i>Special Program Unit</i> .....	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Sasa tumeshamaliza hiyo hatua ya Kamati ya Matumizi. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri ili atupatie taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Juni, 2020 na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu na imekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 – Ofisi ya Waziri Mkuu yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hasa wale wapya, tunapokuwa tunapitisha haya mafungu mwishoni, ninapowahoji ndiyo au siyo, mtaona natumia neno "nadhani walioafiki wameshinda." Kwa nini nasema "nadhani"? Kwa sababu ya sauti, pia inawezekana Mbunge akaona hapana, kutokana na sauti hizi Spika amekosea. Kwa hiyo, Mbunge anaweza akasimama mahali pake akasema Mheshimiwa Spika, mimi nataka tuhesabiwe. Kwa hiyo, ikikubalika namna hiyo na Spika akikubali, basi zoezi la kupiga kura linaanza kuhusu mafungu hayo yapite kwa kuita jina la Mbunge hadi Mbunge mpaka mwisho. Ndiyo sababu yake hiyo.

La pili, Mheshimiwa Waziri anapotoa hoja, wanaotakiwa kuunga mkono kwa kawaida ni Serikali. Wengine siyo sana. Sababu yake ni kulithibitishia Bunge kwamba anachokisema Waziri ndicho walichokubaliana Serikalini. (*Makofi*)

Maana yake katika historia huko nyuma inawezekana aliwahi kuja Waziri akasema yake, siyo yale ya Serikali. Sasa ili Bunge; Spika na ninyi muwe na uhakika kwamba hoja aliyoitoa Mheshimiwa Waziri kweli ni ya Serikali, basi Mawaziri wenzake wanasimama kushuhudia kwamba alichokisema kweli ni chetu. Kwa hiyo, wao watasimama, ninyi wengine ni raha mustarehe. Hata hivyo, kama ni jambo la heri na lina uungwaji mkono mkubwa wala halina ubaya. Ndiyo tafsiri za mambo hayo.

Basi baada ya maneno hayo kwa kweli, tuko kwenye Mwezi Mtukufu na bahati nzuri leo tumemaliza kazi yetu mapema. Napenda kuwashukuru tena na kuwatakiwa kila la heri katika weekend hii inayokuja. Nawakumbusha tu kwamba keshokutwa siku ya Jumapili mchana saa 5.00 au saa 6.00 mabasi yatakuwa yanaondoka hapa kuelekea *UDOM* kwenye Mkutano wa Viongozi wa Kidini ambapo Waheshimiwa Wabunge wote tumealikwa na mgeni rasmi atakuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Kwa hiyo, tumealikwa wote. Naomba mahudhurio yetu yawe mazuri, kuna mengi ya kusikiliza na kujifunza kwenye mkutano huo. Kwa wale ambao watakuwa na udhuru, basi mkutano huo utarushwa na vyombo vingi vya Habari, tunaweza kufuatilia pale tutakapokuwa.

Halafu Waheshimiwa Wabunge safari hii kadi za futari bado hazijaanza kutoka. Watu wamebanisha tu mpaka sasa hivi, namna gani? Maana yake iko na futari ya Spika lakini nasubiri kidogo. Pia kuna futari muhimu zaidi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa anasubiri mafungu. Sasa Waheshimiwa si mmeshatimiza wajibu wenu! Mafungu mmeshampa! Sasa tunasubiri futari. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli huwa tuna utamaduni wa kualikana. Basi utamaduni wetu huo ni mzuri, unatuweka pamoja. Basi yule anayepata nafasi, siyo mbaya sana akatualika huko. Tunasubiri mama yetu Mheshimiwa Salma Kikwete na Waheshimiwa mbalimbali watualike. *(Makofi/Kicheko)*

Basi baada ya maneno hayo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 19 Aprili, 2021 saa 3.00 asubuhi.

Ahsanteni sana.

*(Saa 11.27 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 19 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*